MKENGEUKO WA UTAMADUNI WA WASWAHILI KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI ZAMA ZA UTANDAWAZI: MIFANO KUTOKA RIWAYA TEULE

DEBORA BABILAS MASIMO

SHAHADA YA UMAHIRI YA SANAA KATIKA FASIHI YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA DODOMA

JULAI, 2023

MKENGEUKO WA UTAMADUNI WA WASWAHILI KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI ZAMA ZA UTANDAWAZI: MIFANO KUTOKA RIWAYA TEULE

NA

DEBORA BABILAS MASIMO


TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UMAHIRI YA SANAA KATIKA FASIHI YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA DODOMA

JULAI, 2023

IKIRARI NA HAKIMILIKI


Mimi, **Debora Babilas Masimo**, ninathibisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada inayofanana na hii au nyingine yoyote.

Saini…

Hairuhusiwi kuzalisha, kunakili au kusambaza sehemu ya tasnifu hii bila kibali au idhini kutoka kwa mwandishi wa tasnifu au Chuo Kikuu cha Dodoma.

ITHIBATI YA WASIMAMIZI

Waliotia saini hapa chini wanathibitisha kwamba wamesoma tasnifu hii inayoitwa **Mkengeuko wa Utamaduni wa Waswahili katika Riwaya ya Kiswahili Zama za Utandawazi: Mifano kutoka Riwaya Teule**. Wamejiridhisha kuwa ni kazi halisi ya Debora Babilas Masimo na wamependekeza kuwa inafaa kukubaliwa na Chuo Kikuu cha Dodoma kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Umahiri ya Sanaa katika Fasihi ya Kiswahili.

Saini  Tarehe 17 JULAI 2023

Dkt. Aginiwe Sanga

Msimamizi (Na1)

Saini  Tarehe17 JULAI 2023

Dkt. Emmanuel Kilatu

Msimamizi (Na 2)

SHUKURANI

Kwanza kabisa, ninamshukuru Mungu mwingi wa rehema na fadhili nyingi kwa kunijalia afya njema kipindi chote cha masomo yangu. Ninamshukuru zaidi kwa kunisaidia katika uandishi wa tasnifu hii, kwa kuwa haikuwa kazi rahisi. Hakika amekuwa nami tangu mwanzo mpaka mwisho. Kila nilipokutana na changamoto, niliendelea kutumaini ahadi zake na kujipa nguvu ya kusonga mbele. Sikuacha kukumbuka neno lake kutoka katika Biblia takatifu, Yoshua 1:9 linalosema, “Je si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa usiogope wala usifadhaike, kwa kuwa BWANA, Mungu wako yu pamoja nawe kila uendako”.

Pili, ninatoa shukurani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt. Aginiwe Sanga na Dkt. Emmanuel Kilatu kwa kuwa mstari wa mbele katika kunipa mwongozo na ushauri katika kufanikisha tasnifu hii. Licha ya majukumu mengi ya kiofisi waliyokuwanayo, walihakikisha wanatenga muda kwa ajili ya kunipa mwongozo na kusoma kazi hii. Hakika Mungu wa mbinguni asiwapungukie, bali awabariki kadri ya mapenzi yake na kuwajalia afya njema.

Tatu, napenda kutoa shukurani kwa Dkt. Zuhura Badru, Dkt. Stella Faustine, Dkt. Getruda Shima, Dkt. Abdulmalick Feruzi, Dkt. Rafiki Sebonde, Dkt. Adria Fuluge na Hassan Hassan. Pamoja na majukumu mengi ya kiofisi waliyonayo, hawakusita kutoa ushauri katika kufanikisha tasnifu hii. Asanteni sana kwa kujitoa kwenu, Mungu awabariki na kuwapa mafanikio tele.

Nne, ninawashukuru wanafunzi wenzangu wa Shahada ya Umahiri ya Sanaa katika Fasihi ya Kiswahili wa mwaka 2020 hadi 2022 ambao ni Eva Zabroni na Gabriella Nchimbi. Hakika walinitia moyo nilipoonyesha hali ya kukata tamaa katika zoezi zima la utafiti. Waswahili husema “umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, na kidole kimoja hakivunji chawa”. Hakika ushirikiano wao umekuwa chachu ya mafanikio katika kazi yangu. Mungu awabariki na kuwafanikisha katika kazi zao.

Tano, kipekee napenda kuwashukuru wazazi wangu kwa kuwa nami katika harakati za kusomea Shahada yangu ya Umahiri ya Sanaa katika Fasihi ya Kiswahili. Hakika wamekuwa tunu bora katika maisha yangu. Sina cha kuwalipa, lakini nawaombea maisha marefu.

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mama yangu kipenzi Bi. Penuel Alson Semoka, kwa kuwa mshauri bora kipindi chote cha masomo yangu. Hata nilipokutana na magumu nilikimbilia katika mikono yako kupata faraja bora. Ulinitia moyo na kunisisitiza kufanya kazi kwa bidii. Hata pale nilipohitaji msaada, uliutoa kwa moyo. Hakika wewe ni mama bora kwangu na hazina iliyositirika katika moyo wangu. Nakupenda sana mama, asante kwa kuwa nami katika hali zote kila wakati.

IKISIRI

Tasnifu hii ni matokeo ya utafiti uliofanywa kuhusu “Mkengeuko wa Utamaduni wa Waswahili katika Riwaya ya Kiswahili Zama za Utandawazi”. Riwaya zilizochunguzwa ni miongoni mwa zilizoandikwa katika zama za utandawazi ambazo ni: *Rais Anampenda Mke Wangu* na *Almasi za Bandia*. Pia, utafiti ulichunguza riwaya zilizoandikwa kabla ya utandawazi ili kupata picha ya jinsi utamaduni wa Waswahili ulivyokuwa kwa wakati huo. Riwaya hizo ni: *Mirathi ya Hatari na Kurwa na Doto*. Utafiti huu ulichunguza namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya teule za Kiswahili tofauti na vyanzo vingine kama redio, televisheni na mitandao ya kijamii kwa kuwa riwaya hizo zimesawiri kwa uhalisia mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili. Utafiti uliongozwa na malengo mahususi matatu: Mosi, kubainisha vipengele vya utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule za Kiswahili kabla ya utandawazi. Pili, kufafanua namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya teule za zama za utandawazi. Tatu, kutathimini athari za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi. Utafiti uliongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya Sosholojia na nadharia ya Ubaada Ukoloni. Nadharia ya Sosholojia ilitumika kuchunguza vipengele vya utamaduni wa Waswahili vilivyopo katika riwaya teule. Pia, nadharia ya Ubaada Ukoloni ilitumika katika kuangalia mabadiliko yaliyochangiwa na taathira za ukoloni katika nchi zilizotawaliwa na wakoloni. Njia zilizotumika kukusanya data ni usaili na uchanganuzi matini. Njia ya usaili ilitumia sampuli ya wanafunzi na wahadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma kulingana na mwongozo wa maswali ya utafiti huu. Pia, uchanganuzi wa matini ulipitia riwaya teule za Kiswahili ambazo zilichanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti. Utafiti ulifanyikia katika mkoa wa Dodoma. Data zilikusanywa katika Chuo Kikuu cha Dodoma katika Ndaki ya Insia na Sayansi za Jamii. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwapo kwa mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika vipengele vya lugha, ndoa, imani za kidini, kifo, maadili na mavazi. Utafiti huu umetoa mchango mpya kwa jamii kwa kuonyesha namna riwaya ya Kiswahili inavyokuwa wakala mmojawapo wa kukengeusha utamaduni wa Waswahili katika zama za utandawazi mbali na vyanzo vingine kama filamu, mitandao ya kijamii, redio na televisheni ambavyo vinachangia kumomonyoa maadili katika jamii.

YALIYOMO

IKIRARI NA HAKIMILIKI i
ITHIBATI YA WASIMAMIZI ii
SHUKURANI iii
TABARUKU iv
IKISIRI v
YALIYOMO vi
ORODHA YA VIAMBATISHO x
UFAFANUZI WA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA xi

SURA YA KWANZA 1
UTANGULIZI WA JUMLA 1
1.1 Utangulizi 1
1.2 Ufafanuzi wa Istilahi na Dhana Muhimu 1
1.2.1 Riwaya 1
1.2.2 Riwaya ya Kiswahili 2
1.2.3 Mswahili 2
1.2.4 Mkengeuko 2
1.2.5 Utamaduni 3
1.2.6 Utandawazi 3
1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti 3
1.4 Tamko la Tatizo la Utafiti 8
1.5 Malengo ya Utafiti 8
1.5.1 Lengo la Jumla 9
1.5.2 Malengo Mahususi ya Utafiti 9
1.6 Maswali ya Utafiti 9
1.7 Umuhimu wa Utafiti 9
1.8 Mawanda ya Utafiti 10
1.9 Muhtasari wa Sura ya Kwanza 10

SURA YA PILI 11
MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA 11
2.1 Utangulizi 11

2.2 Mapitio ya Maandiko 11
2.2.1 Maandiko Kuhusu Utamaduni wa Waswahili 11
2.2.2 Maandiko Kuhusu Utandawazi 13
2.2.3 Maandiko Kuhusu Riwaya ya Kiswahili 14
2.2.4 Mapengo Yaliyohitaji Kuzibwa 15
2.3 Kiunzi cha Nadharia 16
2.3.1 Nadharia ya Sosholojia 16
2.3.1.1 Misingi ya Nadharia ya Sosholojia 17
2.3.1.2 Namna Nadharia ya Sosholojia Ilivyotumika 17
2.3.2 Nadharia ya Ubaada Ukoloni 18
2.3.2.1 Misingi ya Nadharia ya Ubaada Ukoloni 18
2.3.2.2 Namna Nadharia ya Ubaada Ukoloni Ilivyotumika 19
2.4 Muhtasari wa Sura ya Pili 19

SURA YA TATU 21
METHODOLOJIA YA UTAFITI 21
3.1 Utangulizi 21
3.2 Usanifu wa Utafiti 21
3.3 Mkabala wa Utafiti 22
3.4 Eneo la Utafiti 22
3.5 Walengwa wa Utafiti 22
3.5.1 Wango Tafitiwa 22
3.5.2 Usampulishaji 23
3.5.3 Sampuli ya Watafitiwa 23
3.6 Ukusanyaji wa Data 25
3.6.1 Njia na Zana za Kukusanyia Data 25
3.6.1.1 Usaili 26
3.6.1.2 Uchanganuzi wa Matini 26
3.7 Uchanganuzi wa Data 27
3.8 Uzingatizi wa Maadili ya Utafiti 27
3.9 Uhalali na Uthabiti wa Utafiti 28
3.10 Changamoto za Utafiti na Utatuzi Wake 28
3.11 Muhtasari wa Sura ya Tatu 29

SURA YA NNE..... 30
UWASILISHAJI WA DATA NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI 30
4.1 Utangulizi..... 30
4.2 Muhtasari wa Riwaya Teule..... 30
4.2.1 Riwaya ya *Kurwa na Doto*..... 30
4.2.2 Riwaya ya *Mirathi ya Hatari*..... 31
4.2.3 Riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu*..... 31
4.2.4 Riwaya ya *Almasi za Bandia*..... 32
4.3 Vipengele vya Utamaduni wa Waswahili katika Riwaya Teule..... 33
4.3.1 Lugha..... 33
4.3.2 Imani za Dini..... 40
4.3.3 Milo na Vinywaji..... 45
4.3.4 Ndoa..... 48
4.3.5 Sanaa..... 56
4.3.6 Kifo..... 60
4.3.7 Mavazi..... 64
4.4 Mkengeuko wa Utamaduni wa Waswahili katika Riwaya Teule..... 66
4.4.1 Lugha..... 66
4.4.2 Ndoa..... 73
4.4.3 Kifo..... 78
4.4.4 Maadili..... 81
4.4.5 Imani za Kidini..... 83
4.4.6 Mavazi..... 85
4.5 Athari za Mkengeuko wa Utamaduni wa Waswahili katika Riwaya Teule..... 87
4.5.1 Athari Chanya..... 87
4.5.1.1 Kuleta Upya katika Riwaya ya Kiswahili..... 88
4.5.1.2 Kusambaa kwa Ujumi wa Tamaduni za Kigeni..... 89
4.5.1.3 Upanuzi wa Hadhira..... 91
4.5.1.4 Kuongezeka kwa Watunzi..... 92
4.5.1.5 Ongezeko la Maarifa Mapya..... 93
4.5.2 Athari Hasi..... 94
4.5.2.1 Kuharibu Historia ya Utamaduni wa Waswahili..... 94
4.5.2.2 Mtazamo Hasi Juu ya Utamaduni wa Waswahili..... 95

4.5.2.3 Kupotea kwa Thamani ya Lugha ya Kiswahili 96
4.5.2.4 Kuharibu Thamani ya Utamaduni wa Waswahili 98
4.5.2.5 Kuimarisha Utamaduni wa Kimagharibi 99
4.5.2.6 Mmomonyoko wa Maadili katika Jamii 100
4.5.2.7 Kupotea kwa Utambulisho Kupitia Utamaduni wa Waswahili 101
4.5.2.8 Kupoteza Mvuto wa Kiujumi wa Kiafrika 102
4.6 Muhtasari wa Sura ya Nne 103

SURA YA TANO 104
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 104
5.1 Utangulizi 104
5.2 Muhtasari wa Tasnifu 104
5.3 Hitimisho la Tasnifu 105
5.3.1 Utoshelevu wa Nadharia Zilizotumika 105
5.3.2 Mchango Mpya wa Utafiti Huu 106
5.4 Mapendekezo 106
5.4.1 Mapendekezo ya Utafiti Huu kwa Wadau Mbalimbali 107
5.4.2 Mapendekezo Kuhusu Tafiti Zijazo 107
5.5 Muhtasari wa Sura ya Tano 108
MAREJELEO 109
VIAMBATISHO 118

ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatanisho A: Miongozo ya Ukusanyaji Data..... 118
Kiambatanisho B: Orodha ya Watafitiwa Kutoka Chuo Kikuu Cha Dodoma- Idara ya Kiswahili 121
Kiambatanisho C: Vibali vya Ruhusa vya Utafiti..... 123

UFAFANUZI WA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

Bi	Bibi
Bw	Bwana
C.B.S.L	College of Business Studies and Law
C.H.S.S	College of Humanities and Social Sciences
Dkt.	Daktari
Juz	Juzuu
Ktj	Keshatajwa
Ltd	Limited
M.A	Master of Arts
Na	Namba
Pg	Page
Ph.D	Doctor of Philosophy
Tol	Toleo
TPH	Tanzania Publishing House
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
UDOM	University of Dodoma
Uk.	Ukurasa
Vol.	Volume
Www	World Wide Web

SURA YA KWANZA
UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Utangulizi

Utafiti huu ulikusudia kuchunguza Mkengeuko wa Utamaduni wa Waswahili katika Riwaya ya Kiswahili Zama za Utandawazi. Katika sura hii mambo mbalimbali yaliyojadiliwa ni ufafanuzi wa istilahi na dhana muhimu zilizotumika katika utafiti huu, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mawanda ya utafiti.

1.2 Ufafanuzi wa Istilahi na Dhana Muhimu

Sehemu hii inafafanua istilahi na dhana mbalimbali zilizotumika katika utafiti. Mtafiti amefafanua istilahi na dhana hizo kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali, pia, amefafanua istilahi na dhana hizo kulingana na mwelekeo wa utafiti uliofanyika kwa lengo la kutoa mwongozo kwa wasomaji kuelewa muktadha wa matumizi ya istilahi na dhana hizo katika utafiti huu. Istilahi na dhana zilizofafanuliwa ni Riwaya, Riwaya ya Kiswahili, Mswahili, Mkengeuko, Utamaduni na Utandawazi.

1.2.1 Riwaya

Masebo na Nyangwine (2007) wanaifasili riwaya kuwa ni hadithi ndefu ya kubuni yenye mawanda mapana, lugha ya kinathari, mchanganyiko wa visa na dhamira, wahusika kadhaa na matukio yaliyosukwa kimantiki yenye kufungamana na maisha halisi. Hata hivyo, fasili hii haijabainisha ni mawanda kiasi gani yanayomaanishwa. Mtu anaweza kujiuliza, mawanda mapana ni yapi na yanapatikana wapi? Naye Senkoro (2011) anaelezea zaidi kuwa riwaya ni kisa ambacho urefu wake unakiruhusu kitambe na kutambaa mahali pengi katika vizingiti vingi vya maisha kama apendavyo mwandishi wake. Anaendelea kueleza kuwa riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye visa vingi, wahusika zaidi ya mmoja na yenye mazungumzo na maelezo yanayozingatia kwa undani upana wa maisha ya jamii. Katika fasili hii Senkoro (ktj) hajabainisha riwaya inatakiwa kuwa na urefu upi, jambo linaloleta mkanganyiko katika maana hii.

Kwa mujibu wa utafiti huu, riwaya ni utungo wa kibunifu ulioandikwa kwa kutumia lugha ya kisanaa na uliobeba visa na matukio changamani. Utanzu huu hueleza

mambo kwa kina yenye kusawiri hali halisi ya maisha kulingana na wahusika katika mazingira yao.

1.2.2 Riwaya ya Kiswahili

Mlacha na Madumulla (1991) wanaelezea riwaya ya Kiswahili kuwa ni ile inayofungamana na utamaduni wa jamii ya Waswahili. Naye, Madumulla (2009) anaongezea kuwa riwaya ya Kiswahili ni ile ambayo inafungamana na utamaduni wa jamii ya Waswahili katika lugha ya Kiswahili.

Hivyo, kwa mujibu wa utafiti uliofanyika, riwaya ya Kiswahili ni ile iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili na kufungamana na utamaduni wa Waswahili. Aidha, utamaduni huo unaweza kuwa umekengeuka au haujakengeuka katika riwaya hiyo. Maana hii ndiyo itakayorejelewa katika utafiti huu kwa sababu riwaya zilizotumika katika utafiti huu zipo katika makundi mawili ambayo ni riwaya zilizosawiri utamaduni wa Waswahili na zile zilizokengeuka katika kuusawiri utamaduni huo.

1.2.3 Mswahili

Ponera (2010) anaeleza kuwa Mswahili ni mtu mwenye kiwango kikubwa cha umilisi wa lugha ya Kiswahili. Anaelezea zaidi kuwa “Mswahili ni mtu ambaye amefungamana sana na mila na desturi za jamii ya watu watumiao lugha ya Kiswahili kiasi hata cha kumuathiri kifikra, kimtazamo na kiitikadi”.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika, Mswahili ni mtu mwenye umilisi wa kutumia lugha ya Kiswahili na amefungamana na utamaduni wa jamii ya Waswahili. Maana ya Mswahili iliyofafanuliwa hapo juu ndio itakayorejelewa katika utafiti huu kwa sababu imeendana na muktadha wa utafiti uliofanyika.

1.2.4 Mkengeuko

Mkengeuko umepambanuliwa na wataalamu mbalimbali katika nyanja ya kimawasiliano, kiujumi, kifalsafa, kiuchumi na kisosholojia. Kwa mujibu wa BAKITA (2016) mkengeuko ni tabia katika jamii ambayo tukio moja linachukua kasi na kulifanya tukio la awali lililokuwapo kusahaulika.

Kwa mujibu wa utafiti huu, mkengeuko ni hali ya jamii kujitenga na utamaduni wake asilia. Hali hii inatokana na athari za utandawazi. Istilahi hii imetumika katika utafiti

huu kuchunguza namna riwaya teule zilizoandikwa kipindi cha utandawazi zinavyojitenga na utamaduni asili wa jamii ya Waswahili kutokana na athari za utandawazi.

1.2.5 Utamaduni

Ramadhani (2013) anasema kuwa utamaduni ni mfumo au utaratibu wa maisha ambao jamii inaufuata katika maisha yake ya kila siku ikijumuisha mila na desturi, miiko, matambiko, jando na unyago. Kwa mujibu wa utafiti huu, utamaduni ni mwenendo wa maisha ya jamii, mitazamo yao na taratibu zao za kuendesha maisha zinazowatofautisha na jamii nyingine.

1.2.6 Utandawazi

Kwa mujibu wa Little (1996), utandawazi ni hali ya kifikra, mipango ya kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni inayopaswa kuandaliwa kwa kuondoa mipaka ya taifa moja ili kutanda dunia nzima. Naye, Beerkens (2006) anaongezea zaidi kuwa utandawazi ni jumla ya harakati na taratibu za kimageuzi zenye kuwafanya watu kuunganishwa katika dunia kuwa kama kijiji.

Hivyo, katika utafiti huu tunauchukulia utandawazi kuwa ni mwingiliano uliopo kati ya nchi za Kiafrika na mataifa mengine katika mambo ya kiuchumi, kiutamaduni, kielimu na kijamii unaoifanya dunia kuwa kama kijiji.

1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Utanzu wa riwaya kidunia hauna historia ndefu tukilinganisha na tanzu nyingine za fasihi kama tamthiliya simulizi na ushairi. Hii ni kwa sababu utanzu wa riwaya ulitegemea maendeleo katika taaluma ya uandishi tofauti na tanzu nyingine zilizowasilishwa kwa njia ya usimulizi. Kwa mfano, katika bara la Ulaya, nchini Uingereza, riwaya ya kwanza kuandikwa iliitwa *Robinson Crusoe* (1719) iliyoandikwa na Daniel Defoe, ikifuatiwa na *Pamela* (1740) iliyoandikwa na Samuel Richardson na kufuatiwa na *Joseph Andrews* (1742) iliyoandikwa na Henry Fielding. Uandishi wa riwaya hizo za Kiingereza ulileta mapinduzi makubwa kwa kuwa riwaya hizo zilisawiri hali halisi ya maisha kwa kutumia lugha iliyozoeleka katika jamii. Hata hivyo, inasemekana kuwa riwaya ya Uingereza ilipata ukomavu wa haraka tangu kuanza kwake. Hii ilitokana na mambo mbalimbali yaliyokuwapo

katika jamii hiyo kama vile, maendeleo ya kiuchumi, elimu, sayansi na teknolojia. Pia, huko barani Asia, katika India ya kale, inasadikika kulikuwa na masimulizi yaliyoitwa *Masaibu ya Wana Kumi wa Mfalme* yaliyoandikwa na Dandin karne ya saba ambayo yalifananishwa na riwaya. Masimulizi haya yalihusu maisha ya watoto kumi wa mfalme huku yakisawiri utamaduni wa watu wa India (Madumulla, 2009).

Mwanzo wa riwaya huhusishwa na mitazamo mbalimbali kwa mujibu wa wataalamu ambayo ipo katika makundi makuu mawili. Kundi la kwanza ni wataalamu wenye mtazamo unaohusisha mwanzo wa riwaya na fani simulizi tangulizi zilizokuwapo katika jamii kama vile, visasili, romansi na tawasifu. Riwaya zilizoibuka katika mkondo wa fani simulizi zilisawiri hali ya maisha ya wakati huo (Mlacha na Madumulla, 1991; Mulokozi, 1996; Njogu na Chimerah, 1999; na Madumulla, 2009). Kundi la pili, ni wale wanaohusianisha mwanzo wa riwaya na ubepari uliosababishwa na mapinduzi ya viwanda huko Ulaya. Mapinduzi ya viwanda yalileta mabadiliko makubwa katika jamii kama kukua kwa matabaka, unyonyaji na ufedhuli. Hivyo, riwaya ilihitajika ili kusawiri mambo yaliyokuwa yanatokea katika jamii (Senkoro, 1977). Nchi za Kiafrika nazo hazikuwa nyuma kwani zilitumia kazi za fasihi ikiwamo riwaya katika kusawiri nyanja za kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa kuonesha uhalisia wa maisha ya bara hili.

Licha ya kuwapo kwa fani simulizi kwa muda mrefu barani Afrika, riwaya ya Kiswahili ilianza na kuendelezwa kupitia shughuli mbalimbali zilizoendeshwa na watawala wa kikoloni katika bara hili, ikiwamo elimu ya Kimagharibi iliyosambaa katika maeneo ya Afrika Kusini, Magharibi, Mashariki na Afrika ya Kati. Kuimarika kielimu katika Afrika kuliibua waandishi wengi wakiwamo Amos Tutuola, Chinua Achebe na Alex la Guma ambao waliandika kazi za riwaya. Riwaya za mwanzo katika Afrika Mashariki zilikuwa katika lugha ya Kiswahili na lugha za wenyeji katika maeneo ambayo Kiswahili kilipata upinzani. Kwa mfano, katika nchi ya Uganda lugha ya Kiswahili ilihusishwa na uislamu pamoja na Waarabu, hivyo, wananchi hawakuipokea. Badala yake lugha ya Luganda ilitumika katika uandishi wa riwaya za mwanzo ambazo zilisawiri maisha ya Wabaganda. Baadhi ya kazi hizo ni vitabu vya Apolo Kagwa: *Entalo za Buganda* (Vita vya Buganda) na *Basekabaka be Buganda* (Wafalme wa Buganda) zilisawiri mila na desturi za Wabaganda (Madumulla, 2019).

Nchini Tanzania, maandiko ya hadithi fupi yaliyokuwa katika lugha ya kigeni yalitafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Mifano ya hadithi fupi hizo ni kama vile *Alfu lela Ulela* (1928), *Mashimo ya Mfalme Suleiman* (1929) na *Safari za Gulliver* (1932). Maandiko haya yaliletwa na wageni lakini yalikuwa msingi na chachu ya kuibua waandishi wenyeji kuandika riwaya zenye kusawiri maisha ya Waswahili. Senkoro (1976) anasema kuwa riwaya ya kwanza ya Kiswahili ni ya *Uhuru wa Watumw*a (1934) iliyoandikwa na James Mbotela. Riwaya hii ilikuwa na mandhari ya Afrika Mashariki, wahusika walikuwa Waswahili, maudhui yake yaliwahusu Waswahili na mwandishi mwenyewe alikuwa Mswahili. Andiko hili liliwavutia waandishi kutoka nchini Tanzania kuweza kuandika riwaya ya Kiswahili kwa kusawiri utamaduni wa jamii hiyo. Pia, kulikuwa na wimbi kubwa la waandishi lililoibuka kutokana na mashindano yaliyoambatana na tuzo katika masuala ya fasihi.

Mashindano ya kiuandishi kwa kutumia lugha ya Kiswahili yaliibua waandishi kama Saleh Farsy, Aniceti Kitereza na Shaaban Robert. Hawa waliandika kazi za riwaya kama vile, *Kurwa na Doto* (1960), *Bwana Mnyombokere na Bibi Bugonoka* (1980) na *Adili na nduguze* (1952) mtawalia. Kazi hizi zilisawiri hali ya maisha ya jamii na utamaduni wa Waswahili (Ndungo na Mwai, 1991; Mulokozi, 1996; na Njogu & Chimerah, 1999). Riwaya za mwanzo zilikuwa na sura ya kifasihi simulizi, na zilichukua mambo mengi kutoka katika jamii ya Kiafrika. Kwa mfano, riwaya za kipindi cha uhuru zilisifia uhuru na kushangilia mashujaa waliopambania uhuru, na za kipindi cha Azimio la Arusha zilisawiri falsafa ya ujamaa iliyowataka watu kuishi pamoja na kwa kujitegemea katika maisha yao ya kila siku (Beja, 1988; Samwel, 2015). Riwaya hizo zilisawiri mfumo wa maisha ambao uliwaunganisha Waswahili kuishi kwa umoja na kushirikiana katika shughuli mbalimbali za kuleta maendeleo kwa jamii (Akida, 1977; Mbaabu, 1985). Riwaya za mwanzo za miaka ya 1970 kurudi nyuma zinaonekana kusawiri maisha ya jamii katika nyanja ya kiutamaduni, kiuchumi, kielimu na kisiasa, jambo ambalo linazitofautisha riwaya hizo na riwaya za sasa ambazo zina sifa ya kuandika masuala ya kijamii kwa kujikita katika utamaduni wenye sura ya kiutandawazi.

Baadhi ya riwaya za miaka ya 1980, 1990 na 2000 katika mkondo wa riwaya pendwa zimebeba sura mpya ya kitandawazi inayozitofautisha na riwaya za mwanzo zilizokuwa na sifa ya kutumia lugha yenye maadili na iliyobeba maudhui ambayo

yalisawiri hali halisi ya maisha ya jamii ya wakati huo. Kwa mfano, riwaya kama *Mtu ni Utu, Ndoto ya Ndaria, Siku ya Watenzi Wote* na *Njozi za Usiku* zilibeba maudhui kama vile ya ujenzi wa jamii mpya, malezi bora, umoja na mshikamano, bidii na umuhimu wa kazi. Maudhui haya yalikuza, kujenga na kudumisha utamaduni wa Waswahili. Riwaya za kipindi cha utandawazi, mkondo wa riwaya pendwa zimetajwa na baadhi ya wachambuzi wa fasihi ya Kiswahili kuwa zina sifa ya kutumia lugha ambayo inakiuka maadili ya Waswahili. Pia, masuala ya mapenzi ambayo yalikuwa yakizungumzwa kwa faragha kwa sasa yanaanikwa wazi. Zaidi ya haya, riwaya za sasa zimeonekana kuja na maudhui mageni ambayo yanasawiri hali ya ulimwengu wa sasa kama vile masuala ya uvutaji bangi na madawa ya kulevya, ugaidi, ndoa za jinsia moja na biashara haramu (Khamis, 2007; Selemani, 2012 na Kalegeya, 2013). Baadhi ya waandishi wa riwaya wa sasa, wameathiriwa na tamaduni za kigeni zilizoletwa na utandawazi. Hali hii inaonekana kuathiri moja kwa moja utamaduni wa jamii ya Waswahili katika riwaya zinazoandikwa katika kipindi cha utandawazi. Waandishi wa riwaya ya Kiswahili wanaonekana kuandika riwaya zenye kubeba mwigo wa nchi za Kimagharibi ambazo huwa kama sinema zinazoonyesha matukio ya kigeni kwa kutumia wahusika, lugha na mandhari ya Kitanzania (Madumulla, 1995).

Kihistoria, utamaduni wa Waswahili unatofautiana na utamaduni wa maeneo mengine kama Marekani, Ulaya na China. Waswahili wanaongozwa na mambo ya kitamaduni yanayopatikana katika jamii zao kama vile imani zao kupitia dini, mavazi, ndoa, maadili, kifo, malezi, vinywaji, lugha na ujumi. Mambo haya yameipa thamani jamii ya Waswahili kupitia mafunzo yaliyokuwa yanatolewa kwa jamii. Utamaduni husaidia kuitambulisha, kuiunganisha na kuiongoza jamii (Geertz, 1973, Sengo, 1992; Mwansasu, 2005 na Bakari, 2009). Utamaduni wa Waswahili umebeba mila na desturi ambazo zimekuwa zikitumika kama sheria ya kuwaongoza wanajamii kutenda matendo yanayopaswa kutendeka katika jamii. Mwalimu Julius Nyerere mwaka 1992 katika hotuba yake kuhusu utamaduni alitamka wazi kuwa utamaduni ni roho ya taifa na kwamba nchi inayokosa utamaduni wake ni sawa na mkusanyiko wa watu usiokuwa na roho. Utandawazi umeleta mwingiliano kati ya nchi moja na nyingine katika masuala ya kiuchumi, kijamii na kimaendeleo. Maendeleo hayo yameambatana na viashiria vya matumizi ya utamaduni wa kigeni katika jamii kama

matumizi ya lugha ya Kiingereza, mitindo ya mavazi na vyombo vya habari kama televisheni na simu ambavyo vimeathiri utamaduni wa Waswahili (Otokhine, 2000 na Suakei, 2003). Utandawazi umefungua mipaka ya watu na kuingiza tamaduni za kigeni katika nchi nyingine kama za Afrika. Jambo hili linazifanya nchi za Kimagharibi zenye nguvu kiuchumi na kiteknolojia, kusambaza utamaduni wao kwenda katika nchi nyingine hasa za Afrika.

Wataalamu wa nyuga mbalimbali ikiwa ni pamoja na elimu jamii, saikolojia, falsafa, mawasiliano, uchumi, siasa na theolojia wanatanabahisha bayana kuwa utandawazi una athari za moja kwa moja katika tamaduni za jamii za Kiafrika wakiwamo Waswahili. Wade (1997), Yakubu (1999) na Jean (2002) wameeleza namna mitandao ya kijamii inavyochangia kuharibu tamaduni za Kiafrika, ambapo mamlaka za udhibiti na walezi wanakosa udhibiti wa moja kwa moja kutokana na uhuru katika kuifikia mitandao hiyo. Kwa mfano, mijongeo ya taarifa kupitia satelaiti, programu za televisheni, filamu na miziki imechangia uibukaji wa masuala mapya kama vile, mitindo mipya ya maisha, ndoa za jinsia moja na matabaka katika jamii. Waters (1995), Wilfred (1997) na Oni (2005) wanashadidia kuwa ukoloni, elimu na mwingiliano wa kijamii vinachangia kukengeusha dini, lugha, mavazi, mila na desturi, vyakula na ndoa za Waafrika. Kabiru (2013) ameelezea kuwa Umagharibi ndio chanzo cha uharibifu wa mifumo ya familia za Waafrika.

Mwingiliano wa Waswahili na wageni umechangia kuharibu thamani ya maadili yaliyomo katika jamii ya Waswahili kwa kuthamini mambo mapya yaliyoletwa na wageni. Nyonje (2006) na Mwakabwale (2017) wanajadili zaidi jambo hili kwa kueleza kuwa vijana wapo katika hatari ya kupoteza utambulisho kwa kuiga tabia na mienendo ya Kimagharibi ambayo ni tofauti na utamaduni wa jamii. Pia, familia za Waswahili katika kipindi cha utandawazi zipo katika njia panda ya kuacha utamaduni wao na kuthamini mambo ya kigeni yanayoonekana kuwavutia. Athari hizo za utandawazi hazijaishia tu katika maisha ya kila siku ya jamii, bali hata katika kazi za fasihi ya Kiswahili zikiwamo tamthiliya na riwaya (Suakei, 2003; Sanga, 2018; Mwagosi na Wenzake, 2020).

Wataalamu mbalimbali tuliowataja hapo juu ambao mawazo yao yalihusu utandawazi katika utamaduni wa jamii za Kiafrika, wamebaini mambo kadhaa

yanayokengeusha utamaduni wa Kiafrika. Mambo hayo ni pamoja na mitandao ya kijamii, ukoloni, elimu, dini na mwingiliano wa kijamii. Mabadiliko yaliyoletwa na utandawazi katika jamii yanaonekana kusawiriwa katika riwaya ya Kiswahili kwa namna ambavyo inaonekana kuathiri utamaduni wa Waswahili. Jambo hili lilimpa msukumo mtafiti wa kuchunguza na kutathimini mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili ili kuonesha namna riwaya zinazoandikwa zama hizi za utandawazi zinavyoakisi mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili.

1.4 Tamko la Tatizo la Utafiti

Kuingia kwa utandawazi katika jamii nyingi za Kiafrika wakiwamo Waswahili kulitoa msukumo kwa wataalamu wa nyuga mbalimbali kama vile sosholojia, saikolojia, anthropolojia, malezi, na sanaa kuchunguza namna utandawazi unavyoathiri utamaduni kupitia mawakala mbalimbali. Wataalamu hawa wanabainisha mawakala mbalimbali wanaochangia kuharibu utamaduni wa Waswahili kama vile, simu za mkononi, mitandao ya kijamii, lugha za kigeni na mwingiliano wa mataifa (Chachage 2002; Mbele 2002; Khamis 2007; Munyoki 2015; Mwagosi, Maguo na Ngenzi 2020).

Mabadiliko yaliyoletwa na utandawazi katika jamii yanaonekana kusawiriwa katika riwaya kwa namna ambayo inaathiri utamaduni wa Waswahili. Jambo hili linaonekana bado halijachunguzwa kwa kina katika riwaya ya Kiswahili. Kutochunguzwa kwa kina kwa jambo hili kumeleta athari kwa jamii. Athari hizo ni pamoja na jamii ya Waswahili kukosa utambulisho wake kupitia riwaya, pia, kutojulikana kwa namna ambavyo riwaya inaweza kuwa wakala mmojawapo wa kuchangia kukengeusha utamaduni wa Waswahili.

Hivyo, utafiti huu umekusudia kuchunguza mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi ili kuonyesha namna riwaya zinazoandikwa zama hizi za utandawazi zinavyosawiri mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili.

1.5 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na lengo la jumla moja na malengo mahususi matatu.

1.5.1 Lengo la Jumla

Lengo la jumla la utafiti huu ni kuchunguza namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya ya Kiswahili ya zama za utandawazi.

1.5.2 Malengo Mahususi ya Utafiti

i) Kubainisha vipengele vya utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule za Kiswahili za kabla ya zama za utandawazi.
ii) Kufafanua namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya teule za Kiswahili za zama za utandawazi.
iii) Kutathimini athari ya mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili ya zama za utandawazi.

1.6 Maswali ya Utafiti

i) Je, ni vipengele gani vya utamaduni wa Waswahili vinavyosawiriwa katika riwaya teule za Kiswahili za kabla ya zama za utandawazi?
ii) Mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unajitokezaje katika riwaya teule za Kiswahili za zama za utandawazi?
iii) Je, mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili una athari gani katika riwaya teule ya Kiswahili ya zama za utandawazi?

1.7 Umuhimu wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yameleta manufaa mbalimbali kwa jamii katika mambo yafuatayo: Mosi, yamesaidia kudokeza kwa wasomaji namna mbalimbali ambazo riwaya ya Kiswahili imekuwa wakala wa kukengeusha utamaduni wa Waswahili kupitia vipengele vya utamaduni vilivyosawiriwa kinyume na utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili. Vipengele hivyo ni kama vile: ndoa, maadili, mavazi, lugha, kifo na imani za kidini. Pili, utafiti huu umeonesha umuhimu kwa wataalamu na jamii kwa ujumla kuweza kukabiliana na changamoto za utamaduni wa Waswahili katika zama hizi za utandawazi. Tatu, utafiti umetoa mwanga kwa waandishi wa zama za utandawazi wa kazi za kifasihi wakiwamo wa riwaya kutunga kazi zinazotambulisha thamani ya utamaduni wa Waswahili. Nne, kutoa fursa kwa watafiti wengine kuchunguza mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili zama hizi za utandawazi katika tanzu zingine za fasihi andishi kama tamthiliya na ushairi. Kwa

ujumla, utafiti huu una mchango wa kiuchambuzi katika kuendeleza mambo mazuri yaliyopo katika utamaduni wa Waswahili.

1.8 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kuchunguza mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili Zama za Utandawazi. Utafiti umeshughulikia riwaya teule ambazo ni riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* (2003) iliyoandikwa na Erick Shigongo na *Almasi za Bandia* (2010) iliyoandikwa na Seithy Chachage. Riwaya hizi zimetumika kama sampuli ya riwaya pendwa zenye mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili zilizoandikwa zama za utandawazi. Pia, mtafiti ametumia riwaya ya *Kurwa na Doto* (1960) iliyoandikwa na Saleh Farsy na *Mirathi ya Hatari* (1977) iliyoandikwa na Claude Mung'ong'o. Mtafiti alitumia riwaya hizi kama sampuli ya riwaya zilizofungamana na masuala ya utamaduni wa Waswahili. Mkoa wa Dodoma ni eneo ambalo utafiti ulifanyika hususani katika Chuo Kikuu cha Dodoma katika Ndaki ya Insia na Sayansi za Jamii ambapo mtafiti alipata data za uwandani na maktabani. Utafiti huu ulijikita uwandani kwa ajili ya kukusanya data kutoka kwa watafitiwa na maktabani vilisomwa vyanzo mbalimbali vya maarifa vinavyoendana na mada iliyofanyiwa utafiti.

1.9 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura hii imefafanua mambo mbalimbali yanayohusiana na utafiti huu. Istilahi na dhana muhimu zilizotumika katika utafiti huu zimefafanuliwa. Vipengele vingine vilivyofafanuliwa ni usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mawanda ya utafiti. Sura inayofuata inahusu mapitio ya maandiko na kiunzi cha nadharia.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia mapitio ya maandiko kuhusiana na Mkengeuko wa Utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili Zama za Utandawazi. Pamoja na kuwasilisha mapitio ya maandiko, sura imebainisha mapengo yaliyojitokeza ambayo yamezibwa na utafiti huu. Aidha, sehemu hii imefafanua kiunzi cha nadharia kilichotuongoza katika kukamilisha utafiti huu.

2.2 Mapitio ya Maandiko

Kipengele hiki kimebainisha maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada iliyofanyiwa utafiti na kuibua mapengo kutoka katika maandiko tangulizi. Maandiko tuliyoyapitia yamegawanyika katika makundi matatu: Kundi la kwanza linahusu maandiko kuhusu utamaduni wa Waswahili. Kundi la pili, linawasilisha maandiko yanayohusu utandawazi, na kundi la tatu, ni maandiko kuhusiana na riwaya ya Kiswahili.

2.2.1 Maandiko Kuhusu Utamaduni wa Waswahili

Sehemu hii inahusu maandiko ya utamaduni wa Waswahili yaliyofanyiwa tafiti na wataalamu mbalimbali kama ifuatavyo:

Isack (2020) amechunguza kuhusu utamaduni wa Waswahili juu ya mambo yanayohusu dini, chakula na desturi za mavazi. Anafafanua kuwa utamaduni wa Waswahili unadhihirika kwa namna wanavyoishi, majina ya vyakula vyao, adabu katika chakula, namna ya mapishi na desturi za mavazi kwa kuzingatia jinsia na rika. Pia, mambo ya adabu na yale yasiyofaa kitamaduni kwa upande wa mavazi. Vilevile, anaelezea vazi la khanga ambalo ni maarufu, na kwamba ni kitambulisho kimojawapo cha Waswahili. Utafiti wa Isack ulichunguza mambo ya Waswahili yanayopatikana katika utamaduni wa Waswahili ambapo umekuwa kama mwongozo kwa mtafiti kuchunguza masuala kama hayo katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa kabla ya zama za utandawazi ili kubaini namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili ulivyojitokeza katika riwaya ya Kiswahili zama hizi za utandawazi.

John (2018) ameandika kuhusu jinsi utamaduni wa hadhira lengwa unavyosawiriwa katika riwaya zilizotafsiriwa kwa Kiswahili. Anaeleza jinsi riwaya zilizotafsiriwa zinavyosawiri utamaduni wa hadhira lengwa. Pia, mtafiti anashauri kuwa wafasiri wanaoshughulikia matini za kifasihi, wazingatie nadharia ya mifumo fungamani inayohimiza utamaduni wa hadhira lengwa ili kuleta ushikamano wa matini lengwa. Utafiti wa John umekuwa chachu kwa mtafiti kuchunguza vipengele vya utamaduni wa Waswahili jinsi vinavyosawiriwa katika riwaya ya kabla ya utandawazi.

Munyoki (2015) ametafiti kuhusu familia za Kiafrika kuwa zipo katika njia panda ya mitagusano na changamoto za usasa katika *Mhanga wa Nafsi Yangu*. Anaeleza kuwa familia za Kiafrika zimo katika njia panda kutokana na athari za Umagharibi kama anavyozipitia mhusika Afida huko peponi. Katika ufafanuzi wake amelitumia neno peponi kiistiari kuwaonya Waafrika ambao kwao, Afrika huitwa motoni ingawa ndiyo pepo yao. Andiko hili limempa mtafiti taarifa za jinsi utandawazi unavyoathiri familia za Kiafrika kupitia utanzu wa riwaya. Hata hivyo, utafiti huu umekusudia kuchunguza namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi.

Nyonje (2006) ametafiti kuhusu mwonoulimwengu wa Waswahili jinsi unavyojitokeza katika desturi za Waswahili. Anasisitiza kuwa Waswahili wanafasiri ulimwengu wao kwa mujibu wa asasi mbalimbali zinazojitokeza katika desturi zao. Asasi hizo ni kama vile ndoa na harusi, kuzaliwa kwa watoto, elimu, tohara, kazi zao na ujumi. Vilevile, anaeleza kuwa utamaduni huangazia mfumo mzima wa imani, mitazamo, ujumi, hisia, na shughuli zote za watu hao. Utafiti uliofanywa na Nyonje umempa mtafiti maarifa kuhusu upekee wa Waswahili katika kuuona ulimwengu wao kupitia asasi mbalimbali kama ndoa. Maarifa haya yalimwezesha mtafiti kufanikisha utafiti kuhusu mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi.

Sengo (1992) ameandika kuhusiana na utamaduni wa Waswahili wilaya ya Kusini Unguja. Katika utafiti wake, anavitaja vipengele anuwai vya utamaduni wa Waswahili wa Kusini Unguja. Baadhi ya vipengele hivyo ni ushirikina, mazishi, ndoa na harusi. Anaelezea kuwa desturi iliyoenea Uswahilini mwote ni wazazi kuwa washauri wakuu wa ndoa za watoto wao. Utafiti huu unausheheneza utafiti

uliofanyika kwa sababu umebainisha vipengele vya utamaduni wa Waswahili ambavyo ndio msingi wa utafiti wetu, ambao umechunguza namna utamaduni wa Waswahili ulivyokengeuka katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi.

2.2.2 Maandiko Kuhusu Utandawazi

Tafiti mbalimbali zimefanywa na wataalamu kuhusiana na utandawazi ulivyoakisiwa katika fasihi kama ifuatavyo:

Mwagosi, Maguo, na Ngenzi (2020) walitafiti namna utandawazi unavyoakisiwa katika fasihi ya Kiswahili katika utanzu wa riwaya. Katika uchunguzi wao wamebaini kuwa utandawazi unatumika kueleza mikabala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa inayosisitiza mwingiliano wa kukiuka mipaka ya taifa moja na jingine. Riwaya waliyoichambua imebainisha namna utandawazi unavyojitokeza katika riwaya ya Kiswahili na kusababisha madhara makubwa katika nchi zinazoendelea. Pia, utafiti uliofanywa na Mwagosi, Maguo na Ngenzi umempa mtafiti mwongozo wa namna utandawazi ulivyoakisiwa katika fasihi ambapo jambo hili lilimsaidia mtafiti katika kufanikisha utafiti kuhusu mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi.

Kevogo (2018) amehakiki kuhusu taswira ya utandawazi katika riwaya mpya ya Kiswahili ya *Dunia Yao*. Kevogo anatueleza kuwa mwandishi huchota fikra, maudhui, falsafa, itikadi, mtindo, maumbo na miundo lugha kwenye jamii ambayo inapokea mabadiliko ambayo huyaweka katika kazi za fasihi. Pia, riwaya mpya kwa kiasi fulani zinashughulikia matatizo ya jamii, lakini kwa kiasi kikubwa zimekiuka mipaka ya kitaifa na kieneo kwa kuangalia hali ya mataifa ya ulimwengu kuliko uhalisia wa jamii husika. Vilevile, riwaya mpya zina sifa za kimtindo na kimuundo ambazo zinakiuka sifa zinazohusishwa na riwaya ya jadi. Utafiti wa Kevogo umetupatia maarifa zaidi kuhusu sifa za riwaya ya kitandawazi yenye kukiuka riwaya jadi ambapo ulimsaidia mtafiti kuchunguza mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili zama za utandawazi katika riwaya teule.

Khamis (2007) katika uchunguzi wake amehoji kuwa ni utandawazi au utandawizi? Anachunguza jinsi lugha ya riwaya mpya ya Kiswahili inavyosawiriwa kipindi cha utandawazi. Pia, ameonesha matukio mbalimbali ambayo yanaletwa na utandawazi

katika jamii. Kwa mfano, mwingiliano wa utamaduni, kukua kwa sayansi na teknolojia na uchumi. Anaeleza kuwa fasihi ya Kiswahili inaendelea kuchukua dhima ya uchunguzi wa jamii lakini ikiwa imebeba silaha mpya za njia ya utunzi na fikra za majadiliano. Utafiti wa Khamis una mchango katika kusukuma mbele utafiti kuhusiana na mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi kwa sababu amechambua kipengele cha lugha kinavyoonekana katika riwaya mpya kipindi cha utandawazi.

2.2.3 Maandiko Kuhusu Riwaya ya Kiswahili

Sehemu hii imefafanua maandiko mbalimbali kuhusu riwaya ya Kiswahili kama ifuatavyo:

Jumanne (2016) amechunguza kuhusiana na mabadiliko ya vionjo vya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili. Katika uchunguzi wake, anabainisha kuwa uandishi katika riwaya ya Kiswahili umebeba mabadiliko kadhaa. Aidha, amebainisha mambo yanayochangia mabadiliko ya kiuandishi katika riwaya ya Kiswahili kama vile umajaribio, sayansi na teknolojia, ongezeko la wasomi na mabadiliko ya kijamii. Vilevile, andiko hilo limechambua vionjo mbalimbali vinavyotumiwa na waandishi katika utunzi wa riwaya ya Kiswahili. Utafiti wa Jumanne umetoa mwanga kwa mtafiti kuhusiana na mabadiliko yanayotokea katika riwaya ya Kiswahili na kumsaidia kuchunguza mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi.

Masingele (2012) amehakiki mabadiliko ya riwaya ya Kiswahili kidhamira kuanzia mwaka 1970 hadi 2011. Katika uhakiki wake, anaandika kuwa riwaya ya Kiswahili ina mabadiliko ya kidhamira kutokana na matukio yanayoibuka kupitia nyanja za kisiasa, kijamii na kiuchumi ambayo humkumba mwanadamu katika jamii kwa wakati fulani. Dhamira katika riwaya hubadilika kutokana na mabadiliko katika jamii kwa kupitia vipindi mbalimbali. Utafiti wa Masingele umeunufaisha utafiti wetu kwa kuwa unaonesha mabadiliko ya kidhamira yaliyopo katika riwaya ya Kiswahili, ambapo hili limesaidia kubainisha namna dhana nzima ya mkengeuko ilivyojitokeza katika utamaduni wa Waswahili kupitia riwaya ya Kiswahili.

Mayaka (2012) ametafiti kuhusiana na ukengeushi wa wahusika wasomi katika riwaya za Euphrase Kezilahabi. Katika utafiti wake, alichambua usawiri wa wahusika wasomi kwa lengo la kuainisha hali zinazosababisha ukengeushi huo. Pia, amechambua daraja mbalimbali za ukengeushi na kutilia mkazo nafasi ya wahusika katika kufanikisha dhana ya matendo kengeushi katika maisha ya kila siku. Vilevile, ameonesha wahusika waliokengeuka na mapendekezo kuhusu suluhisho la hali hiyo. Utafiti wa Mayaka umechunguza mkengeuko wa matendo ya wahusika katika maisha halisi na kumpa mwanga mtafiti kuchunguza mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi.

Libui (2012) alichunguza kuhusiana na riwaya mpya ya Kiswahili na masuluhisho ya changamoto ya utandawazi. Anaeleza kuwa riwaya mpya ya Kiswahili ina sura ya kitandawazi ambayo hukaribiana na riwaya za Kimagharibi. Pia, anatoa mapendekezo ya kukabiliana na changamoto za utandawazi ambazo zipo katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, kiteknolojia, kijamii na kiutamaduni. Utafiti wa Libui umetoa maarifa ya kubainisha changamoto za utandawazi katika riwaya mpya ya Kiswahili ambapo yalimsaidia mtafiti kuchunguza mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi.

Hart (2003) amehakiki kuhusu riwaya mpya ya Kiswahili na kuonesha namna riwaya hiyo inavyosawiri hali halisi ya maisha katika jamii. Anafafanua kuwa riwaya ya Kiswahili imepiga hatua muhimu katika maendeleo yake kwa kupata umbo jipya ambalo ni tofauti na umbo la riwaya za awali ambazo hufuata umbo la kijadi katika utunzi wake. Riwaya za jadi zina sifa ya kuwa na muundo ambao si tata, rahisi kuelewa, wahusika halisi pamoja na mandhari, jambo ambalo ni tofauti na riwaya mpya. Utafiti huu umetoa mwongozo kwa utafiti uliofanyika kwa kuonyesha tofauti kati ya riwaya za kijadi na za sasa ambazo mtafiti alichunguza utamaduni wa Waswahili unavyosawiriwa katika riwaya za kabla ya utandawazi.

2.2.4 Mapengo Yaliyohitaji Kuzibwa

Maandiko ya wataalamu na watafiti mbalimbali walioandika kuhusu utamaduni wa Waswahili, utandawazi na riwaya ya Kiswahili wameacha mapengo yaliyozibwa na utafiti huu. Kwa jumla kutokana na maandiko tangulizi tuliyoyapitia inaonesha wazi kuwa mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za

utandawazi, bado haujafanyiwa utafiti wa kutosha licha ya athari za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili kuwa katika riwaya ya Kiswahili. Hivyo, kutokana na maandiko tangulizi mapengo yafuatayo yalibainika: Mosi, kutokubainishwa kwa vipengele vya utamaduni katika riwaya ya Kiswahili ya kabla ya zama za utandawazi. Pili, kutowekwa wazi namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya ya Kiswahili. Tatu, kutooneshwa kwa athari ya mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi. Kimsingi, mapengo haya yametokana na maandiko hayo kutokusudia kuweka bayana namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi, ambapo utafiti huu umeziba mapengo hayo.

2.3 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili ambazo ni: Nadharia ya Sosholojia na nadharia ya Ubaada Ukoloni. Nadharia ya Sosholojia imetumika kulifikia lengo la kwanza na haikuweza kutumika katika malengo mengine ya utafiti huu. Hivyo, mtafiti alitumia nadharia ya Ubaada Ukoloni kukamilisha lengo la pili na la tatu katika utafiti huu. Kwa msingi huo, Pamoja na upungufu wa nadharia hizi, bado zimekamilishana na kuweza kumsaidia mtafiti kufikia malengo yote ya utafiti huu, kwa kutoa mwongozo katika uchanganuzi na uwasilishaji wa data za utafiti.

2.3.1 Nadharia ya Sosholojia

Nadharia ya Sosholojia huitazama fasihi kama kioo cha jamii ambayo mwandishi anatoka. Huziona kazi za fasihi kuwa zinaonesha uhalisia wa kimaadili, kihistoria na kitamaduni katika jamii husika. Nadharia hii ilianza mwanzoni mwa karne ya 19 na kuasisiwa na Hippolyte Taine (1828-1893). Wafuasi wengine wa nadharia hii ni Bronislaw Malinowski, Franz Boaz na Radcliffe Brown. Nadharia hii ilianzishwa kutokana na kuporomoka kwa uchumi huko Ulaya na kusababisha hali ngumu ya upatikanaji wa bidhaa. Njogu na Chimerah (1999) wanaelezea kuwa jamii na fasihi ni kiungo cha kuunganisha na kuimarisha mahusiano miongoni mwa wanajamii. Ntarangwi (2004) anasema kuwa mtunzi ni mwanajamii ambaye huwekwa katika tabaka fulani katika jamii yake, hivyo hawezi kukwepa athari zinazopatikana katika jamii ambayo imemzaa. Hii ina maana kuwa, fasihi ni taasisi ambayo hutumia lugha kuwakilisha maisha kwa upana kuhusu uhalisia uliopo katika jamii.

2.3.1.1 Misingi ya Nadharia ya Sosholojia

Njogu na Chimerah, (1999) wanabainisha misingi ya nadharia ya Sosholojia kama ifuatavyo:

i. Nadharia hii imejikita katika umahususi wa jamii. Nadharia ya Sosholojia hujikita kuiona jamii kwa upekee wake. Mambo yanayofanyika katika jamii moja hutofautiana na jamii nyingine. Kwa maana hiyo, kila jamii huwa na taratibu za kuiongoza.
ii. Mhakiki hawezi kuhakiki kazi ya fasihi pasipo kuzingatia muktadha na mazingira ya mwandishi wa kazi husika. Mhakiki wa kazi ya fasihi anapokuwa anahakiki huchunguza masuala mbalimbali kwa kuzingatia mazingira na muktadha ambao mwandishi wa kazi ya fasihi anatoka. Kazi ya fasihi haitoki katika ombwe, mwandishi huandika kazi hiyo kulingana na mazingira ya jamii ambamo anatoka.
iii. Fasihi ni dhihirisho la ujumi na ubunifu wa mazingira yaliyopo katika jamii. Hii ina maana kwamba kazi za fasihi husawiri masuala yanayopatika na katika jamii. Fasihi hubeba ubunifu ambao hauwezi kujitenga na jamii ila umithilishaji wa masuala halisi na kuyaweka katika ubunifu.

2.3.1.2 Namna Nadharia ya Sosholojia Ilivyotumika

Nadharia ya Sosholojia ilitumika kufanikisha lengo la kwanza lililohusu kubainisha vipengele vya utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule, kupitia misingi mbalimbali kama vile, umahususi wa jamii, mhakiki wa kazi za fasihi kuhakiki kwa kuzingatia muktadha na mazingira ambayo mwandishi anatoka, na kazi za fasihi hazitoki katika ombwe. Hii ni kwa sababu misingi ya nadharia ya Sosholojia imeathiriana kwa kiasi kikubwa na lengo hilo. Hivyo, basi nadharia hii ilitumika kuchambua data za riwaya teule na zile zilizokusanywa uwandani. Pia, ilisaidiana na nadharia ya Ubaada Ukoloni katika kumwongoza mtafiti kufanikisha lengo la pili na la tatu. Hii ilitokana na misingi ya nadharia ya Sosholojia kushindwa kutosheleza malengo yote matatu ya utafiti. Hivyo, mtafiti alitumia nadharia ya Ubaada Ukoloni kuweza kukamilisha malengo yaliyobakia.

2.3.2 Nadharia ya Ubaada Ukoloni

Nadharia ya Ubaada Ukoloni ilianzishwa mwaka 1950 hadi 1960 baada ya kuporomoka kwa mifumo ya kikoloni. Mwasisi wa nadharia hii ni Edward Said ambaye aliipa mashiko nadharia ya Ubaada Ukoloni kupitia kitabu chake cha *Orientalism*. Wafuasi wengine wa nadharia hii ni Frantz Fanon, Gayatri Chakravorty, Robert Young, Bill Ashcroft na Homi Bhabha. Njogu na Chimerah (2008) wanafafanua kuwa nadharia ya Ubaada Ukoloni inahusu uhusiano uliopo kati ya mataifa yaliyotawala na yaliyotawaliwa kipindi cha ukoloni na hali ya nchi zilizotawaliwa baada ya mifumo ya kikoloni kuanguka. Wataalamu hawa wanasisitiza kuwa nadharia hii hueleza athari za mifumo ya kikoloni katika nyanja ya kiutamaduni, kisiasa na kijamii hata baada ya nchi zilizokuwa zimetawaliwa kupata uhuru wa bendera. Fanon (1952) aliyeandika kitabu kiitwacho *Black Skins White Masks,* katika utangulizi wa kitabu hicho alionesha namna mtu mweusi anavyolazimishwa kujidunisha, kujichukia na kutamani kuwa mweupe. Pia, mwaka 1963 aliandika kitabu cha *The Wretched of the Earth* ambacho kilionyesha namna mataifa ya Kimagharibi yanavyowabagua mataifa yaliyokuwa yametawaliwa. Naye, Said (1978) anadai kuwa nchi za Kimagharibi zilitumia mabavu kutawala nchi za Kimashariki, hata semi ziliwadumaza watawaliwa. Maovu yaliyofanywa na wakoloni yanajidhihirisha hata baada ya kupata uhuru. Wamitila (2002) anafafanua kuwa picha hasi zilizotumiwa na mataifa ya Ulaya kwa nchi zilizokuwa zimetawaliwa ziliendelea kuwadunisha Waafrika ambapo hadi leo nchi zilizotawaliwa zinaendeleza ukoloni mamboleo katika maisha ya jamii hizo. Kwa ujumla, nadharia ya Ubaada Ukoloni inaonesha taathira mbalimbali zilizoachwa na wakoloni katika nchi zilizotawaliwa. Mabaki ya ukoloni yamesambaa katika nyanja mbalimbali kama kiutamaduni, kielimu, kisiasa na kiuchumi katika zama za utandawazi. Hivyo, nadharia hii imetoa mwongozo katika kuchunguza mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule ya Kiswahili.

2.3.2.1 Misingi ya Nadharia ya Ubaada Ukoloni

Njogu na Chimerah (2008) wamebainisha misingi ya nadharia ya Ubaada Ukoloni kama ifuatavyo:

i. Kuwapo kwa matumizi ya lugha za kigeni kama Kiingereza katika nchi za Kiafrika ni kuendeleza ukoloni mamboleo. Msomi wa Kiafrika ili aonekane

amekamilika sharti atumie lugha za kigeni. Hili kwa kiwango fulani hutweza lugha za mataifa yaliyotawaliwa na kukweza hadhi ya lugha za kigeni. Kipindi cha ukoloni kulijengeka imani kwa Waafrika kuwa lugha za kigeni zina nguvu kuliko lugha za asili zilizopatikana katika nchi zao. Watawaliwa walinyang'anywa lugha zao kwa kuendeleza matumizi ya lugha ya kigeni katika nchi zilizokuwa zimetawaliwa na ukoloni. Waafrika wakiwamo Waswahili wanakengeuka kwa kuacha lugha zao zinazoutambulisha utamaduni wao na kuendelea kutukuza lugha za kigeni.

ii. Nadharia hii huyaangalia masuala ya utabaka katika jamii kuwa kiini chake ni mahusiano yanayokuwapo kati ya watawala na watawaliwa. Nchi za Kimagharibi huona zimestaarabika katika nyanja za kimaisha kama kielimu, kiutamaduni, kisiasa na kiuchumi kuliko nchi za Kiafrika ambazo huonekana hazijastaarabika. Nchi za Kiafrika zinaendelea kudumisha vitu vilivyoletwa na watawala ikiwa ni ishara ya kustaarabika. Jambo hili linaendelea kuchochea kukengeuka kwa utamaduni asilia wa Waswahili.

iii. Utamaduni wa nchi zilizotawaliwa ni utamaduni mseto wa mataifa ya wakoloni na ya Waafrika. Ukoloni umeleta masalia ya kiutamaduni katika maisha ya Waafrika. Wakoloni walipokuja kutawala nchi za Kiafrika walikuja na mifumo ya tamaduni zao katika lugha, dini, ndoa, milo na vinywaji, mavazi na sanaa. Nchi zilizotawaliwa zilizopata uhuru, zilifinyanga masalia ya utamaduni wa kigeni, zikayaumba na kutokea utamaduni mseto.

2.3.2.2 Namna Nadharia ya Ubaada Ukoloni Ilivyotumika

Nadharia hii ya Ubaada Ukoloni ilitumika katika kuchunguza namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya teule na kutathimini athari za mkengeuko huo. Matumizi ya nadharia hii yalizingatia misingi kadha wa kadha ambayo kwa kiasi kikubwa imeathiriana na utafiti. Misingi hiyo ni kama matumizi ya lugha ya kigeni, matabaka na mwingiliano wa utamaduni kati ya wakoloni na watawaliwa. Hivyo basi, nadharia hii ilitumika katika kuchanganua data za maktabani na uwandani pamoja na, kuongoza mjadala wa matokeo ya utafiti.

2.4 Muhtasari wa Sura ya Pili

Sura hii imejadili mapitio ya maandiko yanayohusiana na mada iliyofanyiwa utafiti. Maandiko hayo yaligawanywa katika sehemu kuu tatu: Mosi, maandiko kuhusu

utamaduni, pili, maandiko kuhusu mabadiliko ya riwaya ya Kiswahili na tatu, maandiko kuhusu utandawazi. Vilevile, sura hii imeonesha mapengo yaliyobainishwa kutokana na maandiko hayo. Pia, sura hii imefafanua nadharia ya Sosholojia na Ubaada Ukoloni ambazo zilikuwa mwafaka katika utafiti huu kupitia misingi yake. Sura inayofuata inahusu methodolojia ya utafiti.

SURA YA TATU
METHODOLOJIA YA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Katika sura hii tumefafanua namna mchakato wa utafiti ulivyosanifiwa, kufanyika hadi kukamilika kwake. Vipengele vilivyoshughulikiwa katika sehemu hii ni: Usanifu wa utafiti, mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, usampulishaji, sampuli, ukusanyaji data, pamoja na njia na zana za kukusanyia data. Vipengele vingine ni mchakato wa ukusanyaji data pamoja na uchanganuzi wa data, uzingatizi wa maadili ya utafiti, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti, pamoja na changamoto za utafiti huu na namna zilivyotatuliwa.

3.2 Usanifu wa Utafiti

Kwa mujibu wa Creswell (2007) usanifu wa utafiti ni mpangokazi unaojielekeza katika namna mahususi ya kufanya utafiti. Hii ina maana kwamba usanifu wa utafiti hufafanua ni wapi, lini, kwa kiwango gani na namna gani utafiti unatakiwa ufanyike. Utafiti huu umeongozwa na usanifu wa kifenomenolojia kwa lengo la kusaka ukweli wa jambo linalochunguzwa kulingana na uzoefu wa maisha halisi ya jamii mahususi. Usanifu wa kifenomenolojia hujikita katika kusaka data za jambo linalotafitiwa kwa kujiegemeza katika uelewa, mitazamo na tajiriba za watafitiwa ili kupata data za kina na sahihi kuhusiana na jambo linalotafitiwa. Msingi wa usanifu wa kifenomenolojia ni uelewa na ufahamu wa jambo kutoka kwa watafitiwa. Data za kifenomenolojia hukusanywa kwa njia mbalimbali kama vile uchanganuzi wa matini, usaili, ushuhudiaji na majadiliano katika vikundi (Chuachua, 2016). Katika utafiti huu mtafiti alitumia njia ya usaili na uchanganuzi matini katika kupata data. Mtafiti alitumia usanifu wa kifenomenolojia kuwasaili watafitiwa kwa shabaha ya kupata data za kina kuhusu uelewa, mitazamo na tajiriba zao kuhusu mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili ya zama za utandawazi. Aidha, kupitia usanifu huu mtafiti aliweza kubainisha vipengele vya utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule. Vilevile, usanifu huu ulimwongoza mtafiti kutathimini athari za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili katika zama za utandawazi. Kupitia usanifu wa kifenomenolojia mtafiti alichambua data kutoka uwandani na maktabani ili kujibu maswali yaliyouongoza utafiti huu.

3.3 Mkabala wa Utafiti

Mkabala wa utafiti huu ni wa Kitaamuli. Utafiti ulitumia mkabala huu katika hatua ya ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti huu. Ponera (2019) anafafanua kuwa, mkabala wa kitaamuli ni uchunguzi wa kina wa kisayansi ufanywao kwa kutafakari na kuchanganua jambo maalumu kwa lengo la kupata maarifa mapya au kuongeza ufahamu. Utafiti huu, umefanyikia maktabani na uwandani ambapo data zilizokusanywa ni za mrengo wa kitaamuli kwa sababu zifuatazo: Mosi, utafiti umejikita katika ufafanuzi. Utafiti uliofanyika ulijikita katika ufafanuzi kuanzia katika hatua ya kukusanya data, uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Pili, utafiti huu uliegemea katika uzoefu wa watafitiwa kuhusiana na mada iliyofanyiwa utafiti. Watafitiwa walitoa uzoefu na uelewa wao kuhusiana na mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi kwa kurejea katika riwaya teule ambapo walinasibisha na maisha halisi ya jamii wanazoishi. Tatu, sampuli ndogo ilitumika kulingana na utoshelevu wa data. Utafiti huu ulitumia watu wachache ambao walitosheleza malengo ya utafiti kulingana na mada iliyofanyiwa utafiti. Nne, utafiti ulipokea mitazamo, mawazo na uelewa tofauti katika jambo moja kutoka kwa watafitiwa kuhusiana na mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi.

3.4 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyikia katika mkoa wa Dodoma kwa sababu mkoa huu umetumika kama sampuli inayowakilisha miji mingine ya Tanzania ambamo Mosi, ina mwingiliano wa watu kutoka katika maeneo mbalimbali. Pili, kuwapo kwa Chuo Kikuu cha Dodoma ambapo ndio watafitiwa walipatikana kulichochea kuteuliwa kwa mkoa huu. Watafitiwa hao ni wanafunzi na wahadhiri wa fasihi ya Kiswahili ikiwamo riwaya ya Kiswahili.

3.5 Walengwa wa Utafiti

Katika utafiti huu, walengwa wa utafiti wamegawanyika katika makundi mawili ambayo ni wango tafitiwa na sampuli ya watafitiwa.

3.5.1 Wango Tafitiwa

Kwa mujibu wa Ponera (2010) wango tafitiwa ni jumla ya watu na vitu vyote vinavyofaa kutafitiwa kadri ya mwelekeo wa mada ya utafiti ili kupata data

zinazohitajika. Wango tafitiwa huweza kuwa makundi ya watu, mimea, maumbile ya sura ya nchi na kazi za sanaa. Wango tafitiwa katika utafiti huu lilihusisha makundi yafuatayo:

i) Riwaya ya Kiswahili kwa kuwa uchunguzi wa mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili ulijiegemeza katika riwaya ya Kiswahili.
ii) Wahadhiri wa fasihi ya Kiswahili kwa kuwa hawa walisaidia kupatikana kwa taarifa kuhusiana na namna mkengeuko wa utamaduni unavyojitokeza na kutathimini athari hizo katika riwaya teule.
iii) Wanafunzi wa vyuo vikuu kwa kuwa hawa walitoa uelewa na ufahamu wao kuhusiana mada kuhusiana na mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule.

3.5.2 Usampulishaji

Usampulishaji ni kitendo cha kuteua sehemu ndogo ya wango kutoka kwenye kundi kubwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa litakalotumiwa katika kuchunguza na kupata majibu ya utafiti unaofanyika (Mligo, 2012). Ufafanuzi huu una maana kuwa mtafiti anachagua wawakilishi kutoka katika wango tafitiwa. Utafiti huu ulitumia usampulishaji lengwa kupata watafitiwa. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kuteua sampuli kwa kuelekeza fikra kwa baadhi ya watafitiwa kulingana na watakavyoweza kukidhi haja ya malengo ya utafiti huu. Hivyo, utafiti huu ulitumia mbinu za usampulishaji lengwa za aina mbili: Usampulishaji lengwa wa kipekee, ambapo watafitiwa walichaguliwa kutokana na maarifa na ufahamu walionao kuhusiana na masuala ya fasihi ya Kiswahili hususani riwaya. Mbinu hii ilitumika kwa wahadhiri na wanafunzi waliopatikana katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Vilevile, mbinu hii ilitumika kuchagua riwaya zilizokuwa na sifa kulingana na mada iliyokuwa inafanyiwa utafiti. Pili, usampulishaji lengwa kwa kutegemea fursa ambapo mtafiti alitumia usampulishaji huu kwa wahadhiri. Alijiegemeza katika nafasi iliyopatikana kutokana na majukumu ya kikazi.

3.5.3 Sampuli ya Watafitiwa

Sampuli ni sehemu ya wango ambayo imeteuliwa ili itumike kuwakilisha jamii katika kusaka majibu ya tatizo (Kothari, 2009). Utafiti huu ulitumia sampuli ndogo na idadi iliyowekwa katika sampuli haikuathiri chochote katika data na mchakato wa

kupata matokeo ya utafiti, ila ilisaidia kupanga bajeti na muda wa kuweza kupata data za utafiti huu. Utafiti huu uliongozwa na utoshelevu wa data na si idadi ya watafitiwa iliyowekwa. Sampuli ya utafiti huu ilichaguliwa kwa kuzingatia mada ya utafiti, malengo, maswali na ukubwa wa jamii ya watafitiwa. Hivyo, utafiti huu ulitumia sampuli lengwa ikiwa na jumla ya watafitiwa na vitafitiwa 23 ambavyo viligawanyika kama ifuatavyo:

i) Riwaya teule nne (4) ambazo ni: *Rais Anampenda Mke Wangu* na *Almasi za Bandia* zilizoandikwa na waandishi Erick Shigongo na Seithy Chachage mtawalia. Usampulishaji lengwa wa kipekee ulitumika katika kuchagua riwaya teule. Shabaha ya kuchagua riwaya hizi ni sampuli ya riwaya pendwa ambazo zimeandikwa kipindi cha utandawazi. Aidha, riwaya hizi zina mvuto na zinasomwa na watu wengi. Vilevile, zina mkengeuko wa masuala ya utamaduni wa Waswahili. Pia, riwaya hizi zilitarajiwa kutoa data toshelevu zilizohitajika katika utafiti huu. Mtafiti alichambua vipengele vya utamaduni wa Waswahili vilivyokengeuka katika riwaya teule. Pia, mtafiti alitumia riwaya ya *Kurwa na Doto* ya Saleh Farsy na *Mirathi ya Hatari* ya Claude Mung'ong'o ambapo riwaya hizi ni sampuli ya riwaya ambazo zimefungamana na masuala ya kitamaduni yanayopatikana katika jamii ya Waswahili. Riwaya hizi zimempa mtafiti data kuhusu vipengele vya utamaduni wa Waswahili ambavyo vilisaidia kujibu swali la kwanza la utafiti huu.
ii) Wahadhiri wanne (4) wa fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndaki ya Insia na Sayansi za Jamii. Sababu ya kuchagua sampuli hii ni maarifa waliyonayo kuhusiana na riwaya ya Kiswahili. Pia, ubobevu wao wa kitaaluma katika fasihi ya Kiswahili. Vilevile, ni kutokana na kujikita kwao katika uandishi wa kazi za fasihi. Data zilizokusanywa katika sampuli hii zilihusu kubainisha vipengele vya utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule, namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya teule na athari za mkengeuko wa utamaduni katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi.
iii) Wanafunzi kumi na mbili (12) wa Shahada ya awali ya Sanaa katika fasihi ya Kiswahili mwaka wa tatu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndaki ya Insia na

Sayansi za Jamii. Upatikanaji wao ulizingatia usampulishaji lengwa wa kipekee. Sababu ya kuchagua sampuli hii ilikuwa maarifa waliyonayo kuhusiana na masuala ya fasihi ya Kiswahili. Hapa tulikusanya data kuhusu vipengele vya utamaduni vilivyokuwapo katika riwaya teule, mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya teule ya Kiswahili na kutathimini athari za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi.

iv) Wanafunzi watatu (3) wa Umahiri katika fasihi ya Kiswahili mwaka wa pili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndaki ya Insia na Sayansi za Jamii. Upatikanaji wao ulizingatia kujikita kwao katika fasihi ya Kiswahili. Hawa walitoa data kuhusu vipengele vya utamaduni wa Waswahili vilivyomo katika riwaya teule ya Kiswahili kabla ya utandawazi. Walifafanua namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya teule ya Kiswahili zama za Utandawazi na walitathimini athari za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi.

Sampuli hizi tulizozitumia katika utafiti huu zimetosheleza malengo ya utafiti kwa kutupatia utoshelevu wa data kulingana na mwongozo wa malengo na maswali ya utafiti huu.

3.6 Ukusanyaji wa Data

Kipengele hiki kinaelezea njia na zana mbalimbali zilizotumika katika ukusanyaji data pamoja na mchakato wa uchanganuzi wa data.

3.6.1 Njia na Zana za Kukusanyia Data

Njia zilizotumika kukusanyia data ni usaili na uchanganuzi wa matini. Kwa mujibu wa Kothari (2004) mtafiti hutumia njia zaidi ya moja ili kupata data ambazo zisingepatikana kwa kutumia njia moja. Pia, mtafiti hutumia njia zaidi ya moja ili huthibitisha usayansi na usanaa wa utafiti wake. Alderson (1992) anaelezea kuwa hakuna mbinu iliyo bora katika utafiti ikitumika peke yake. Hivyo, kukusanya data kutoka katika njia mbalimbali ni vyema ili mtafiti aweze kuthibitisha matokeo ya utafiti wake. Katika utafiti huu mtafiti alitumia njia ya usaili na uchanganuzi matini ili kupata data ambazo zilikuwa zinahitajika kutoka kwa watafitiwa ili kufanikisha utafiti huu.

3.6.1.1 Usaili

Babbie (1992) anafafanua kuwa usaili ni mawasiliano ya moja kwa moja baina ya mtafiti na wahojiwa kwa ajili ya kupata data. Utafiti huu umetumia njia ya usaili kwa sababu zifuatazo: Mosi, ilimwezesha mtafiti kupata data ambazo ni vigumu kuzishuhudia. Pili, ilimsaidia mtafiti kutoa ufafanuzi wa maswali ambayo watafitiwa wake hawakuyaelewa, na tatu, ilimruhusu mtafiti kupata data za kina ambazo asingeweza kuzipata kwa njia nyingine. Ponera (2019) amegawa usaili katika aina tatu: usaili huria, usaili nusu huria na usaili funge. Utafiti huu umetumia usaili huria ambao ulimpa mtafitiwa uhuru wa kutoa maelezo ya kina kuhusiana na mada iliyokuwa inafanyiwa utafiti. Njia hii ilikuwa muhimu kwa kuwa mtafiti aliitumia kupata taarifa za kina na halisi kutoka kwa watafitiwa. Zana zilizotumika katika njia hii ni miongozo ya usaili iliyotumika kukusanyia data kwa watafitiwa, shajara na kalamu kwa ajili ya kuandikia data kutoka kwa watafitiwa. Vingine ni kinasa sauti kwa ajili ya kurekodia data, simu ya mkononi kwa ajili ya mawasiliano, kompyuta pakatwa kwa ajili ya kuandikia data kutoka uwandani na kinyonyi kwa ajili ya kuhifadhi na kuhamisha nyaraka. Njia hii ilitumika kukusanya data kwa watafitiwa wa aina tatu: Mosi, wahadhiri wa fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, pili, wanafunzi wa mwaka wa tatu wa Shahada ya Sanaa katika fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndaki ya Insia na Sayansi za Jamii, na tatu, wanazuoni wanaosoma Shahada ya Umahiri katika fasihi ya Kiswahili mwaka wa pili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Data zilizokusanywa kwa kutumia njia hii zilihusu malengo yote matatu.

3.6.1.2 Uchanganuzi wa Matini

Maxwell, (2013) anafafanua kuwa uchanganuzi wa matini ni njia ya kukusanya data ambapo taarifa hukusanywa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya maandishi. Katika utafiti huu, mtafiti alisoma kwa makini na kuchambua riwaya teule. Mtafiti alisoma na kuchambua kwa makini riwaya teule ambazo ni *Kurwa na Doto, Mirathi ya Hatari, Almasi za Bandia na Rais Anampenda Mke Wangu* kwa ajili ya kupata data zilizohitajika katika utafiti huu. Katika hatua hiyo, alikusanya kwa mara ya kwanza data za msingi zilizokuwa zinahusiana na malengo ya utafiti wake. Kwanza, alibainisha vipengele vya utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule. Pili, alichambua data kuhusu mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya

teule zama za utandawazi na kutathimini athari za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi. Mtafiti alitumia mwongozo wa uchanganuzi matini katika kufanikisha mbinu hii. Pia, zana kama kompyuta pakatwa, shajara na kalamu vilitumika katika kufanikisha njia hii. Kwa msingi huo, data zilizochambuliwa zilikuwa mahususi kwa ajili ya kufikia malengo yote ya utafiti huu.

3.7 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data ni hatua inayofuata mara baada ya kukamilika zoezi la kuzikusanya (Kothari, 2004). Baada ya mtafiti kukusanya data alizichambua na kuzipanga kwenye makundi kulingana na malengo ya utafiti. Kundi la kwanza, data zilihusiana na lengo la kubainisha vipengele vya utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili kabla ya zama za utandawazi. Kundi la pili, data zilihusiana na mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi. Kundi la tatu, data zilijikita katika kutathimini athari za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi. Baada ya hapo mtafiti alizifafanua data kwa kuzihusisha na mwoano wa kimaudhui kulingana na malengo ya utafiti kwa kuzingatia mwongozo wa nadharia ya Sosholojia na Ubaada Ukoloni.

3.8 Uzingatizi wa Maadili ya Utafiti

Maadili ni kapu la jumla la seti za miongozo ya namna ya kuishi na kukubalika katika jamii (Ponera, 2019). Utafiti huu umeongozwa kwa mujibu wa kanuni zinazoongoza mchakato mzima wa utafiti. Mtafiti alizingatia mambo mbalimbali katika hatua hii:

Mosi, mtafiti aliomba barua ya utambulisho kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Barua hiyo ilimtambulisha mtafiti kwa watafitiwa kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Kibali cha utambulisho wa kufanya utafiti kimemsaidia mtafiti kuweza kuaminika kwa watafitiwa, hivyo, kutoa data kuhusiana na mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule ya Kiswahili zama za utandawazi.

Pili, mtafiti aliomba ridhaa kwa watafitiwa ya kukusanya data kuhusu mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi, ili

waweze kutoa data kwa hiyari. Watafitiwa ambao hawakuwa tayari kwa sababu mbalimbali mtafiti hakuweza kuwalazimisha kutoa data za utafiti ila aliwaeleza umuhimu wa kushiriki zoezi hili. Jambo hili lilimsaidia mtafiti kuwa huru kuwafanyia usaili watafitiwa ambao walikuwa tayari.

Tatu, utunzaji siri wa taarifa ambazo zilipatikana uwandani. Mtafiti alipokuwa anakusanya data kwa watafitiwa aliwaambia taarifa wanazozitoa ni za siri baina ya mtafiti na mtafitiwa na hazitatumika nje ya malengo ya utafiti uliokusudiwa. Watafitiwa walikuwa huru kutoa taarifa kwa mifano kutoka katika jamii ambazo wanatoka na taarifa hizi zimetumika kwa kufanikisha malengo ya utafiti huu na sio vinginevyo.

3.9 Uhalali na Uthabiti wa Utafiti

Uhalali wa utafiti ni hali ya utafiti kuwa na uwezo wa kupima jambo au mambo yaliyotakiwa kupimwa au kutafitiwa tu. Uthabiti wa utafiti ni hali ya utafiti kutoa matokeo yanayowiana ikiwa utafiti utafanyika mahali pengine, wakati mwingine, au na mtu mwingine (Ponera, 2019). Utafiti uliosanifiwa vizuri huweza kuyafikia malengo ya utafiti kwa namna iliyo wazi na inayoeleweka. Ubora wa utafiti hutokana na sifa ya uhalali na uthabiti katika matokeo yake (Sanga, 2018). Hivyo, kwa kutekeleza hayo matokeo ya utafiti huu ni halali na thabiti kwa sababu mtafiti amezingatia yafuatayo: Mosi, mtafiti ametumia lugha nyepesi ya kueleweka katika miongozo ya kukusanyia data. Pili, kuweka bayana mipaka ya utafiti na malengo. Tatu, mtafiti ametumia njia mseto za kukusanyia data. Nne, mtafiti ametumia ithibati sahihi na za wazi katika ujenzi wa hoja katika tasnifu.

3.10 Changamoto za Utafiti na Utatuzi Wake

Katika kuendesha zoezi la utafiti huu, kuhusu mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za Utandawazi, changamoto kadha wa kadha zilijitokeza: Mosi, watafitiwa kutopatikana kwa urahisi kutokana na mwingiliano wa majukumu. Kwa upande wa wanafunzi mtafiti alipokuwa anakusanya data kilikuwa kipindi ambacho wanafunzi walikuwa katika harakati za kumalizia majaribio na kazi za darasani hivyo ilikuwa vigumu kuonana nao kwa muda uliopangwa. Vilevile, wahadhiri katika kipindi hicho walikuwa katika uandaaji wa mitihani**.** Changamoto hii ilitatuliwa na mtafiti kwa kutumia muda ambao

ulipendekezwa na watafitiwa kwa ajili ya kupata data zilizohitajika katika utafiti huu. Pili, baadhi ya watafitiwa hawakuwa radhi kutoa ushirikiano kwa mtafiti. Changamoto hii ilitatuliwa kwa kutoa elimu kuhusu umuhimu wa utafiti uliokuwa unafanyika kwa watafitiwa na kuwashawishi kushiriki katika zoezi hili. Tatu, wakati wa utafiti kulikuwa na upungufu wa kifedha kwa mtafiti. Changamoto hii ilitatuliwa kwa kufinya bajeti ya utafiti ili kuweza kufanikisha zoezi la utafiti huu.

3.11 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Sura hii imejikita katika kuelezea namna mchakato mzima wa utafiti ulivyofanyika mpaka kukamilika. Vipengele vilivyozingatiwa katika sura hii ni usanifu wa utafiti, mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti na njia na zana za kukusanyia data. Vipengele vingine ni uchanganuzi wa data, uzingatizi wa maadili ya utafiti, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti pamoja na changamoto za utafiti huu na namna zilivyotatuliwa. Sura inayofuata inawasilisha mjadala wa matokeo ya utafiti kuhusu mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI WA DATA NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Sura hii imewasilisha na kujadili matokeo ya utafiti kuhusu mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili Zama za utandawazi. Sura hii imegawanyika katika sehemu sita. Sehemu ya kwanza imejikita kutoa utangulizi wa jumla wa sura hii. Sehemu ya pili imetoa muhtasari wa riwaya teule zilizotumika katika utafiti huu. Sehemu ya tatu mpaka ya tano zinahusu mjadala wa matokeo ya utafiti, hivyo, sehemu ya tatu imebainisha vipengele vya utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya *Kurwa na Doto na Mirathi ya Hatari,* sehemu ya nne imefafanua namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya teule za Kiswahili zama za utandawazi kwa kutumia riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu na Almasi za Bandia,* na sehemu ya tano imetathimini athari za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule za zama za utandawazi. Sehemu ya sita imetoa muhtasari wa yaliyojadiliwa katika sura hii.

4.2 Muhtasari wa Riwaya Teule

Kabla ya kujikita katika mjadala wa matokeo ya utafiti, katika sehemu hii, mtafiti ametoa muhtasari wa riwaya teule ambazo ni *Kurwa na Doto*, *Mirathi ya Hatari, Rais Anampenda Mke Wangu* na *Almasi za Bandia*. Muhtasari huu umetolewa ili kudokeza na kutoa mwanga kwa wasomaji wa tasnifu hii kuhusu masuala mbalimbali yaliyojadiliwa katika riwaya hizo.

4.2.1 Riwaya ya *Kurwa na Doto*

Kurwa na Doto ni riwaya inayosawiri maisha ya watu wa Unguja kabla ya mwaka 1960. Riwaya hii imemzungumzia mke na mume ambao waliishi katika visiwa vya Azania vilivyokuwa kwenye bahari ya Ajeani karibu na bara la Dhulumati. Waliishi kwa muda mrefu bila kupata watoto na baadaye mke alipata mimba. Bwana na bibi walifurahi kwani walikuwa hawajawahi kupata mtoto. Hivyo, mimba iliengwaengwa na mpaka siku zikatimia, mke akazaa mapacha. Mtoto aliyetangulia aliitwa Kurwa na aliyefuata aliitwa Doto. Watoto walifanyiwa ada zote kama ilivyohitajika. Waliwakinga na mashetani wabaya, waliadhiniwa na kuvalishwa mvuje, vingwe na nyimbili. Watoto walipokua walipelekwa chuo kwa ajili ya kusoma masomo ya dini ambayo yaliwasaidia katika makuzi yao. Baada ya Kurwa na Doto kukua

walifundwa na kuchezwa ngoma ambazo ziliwafunza maadili mema yaliyowapa mwongozo wa kuishi katika jamii yao. Mwandishi Saleh Farsy, katika riwaya hii amejifungamanisha na utamaduni wa watu wa Unguja kwa kuonyesha maisha yalivyokuwa nyakati hizo na taratibu zilizokuwapo katika jamii kwa kusawiri masuala ya vifo, sanaa na lugha zilizokuwa zinatumika katika mazingira hayo.

4.2.2 Riwaya ya *Mirathi ya Hatari*

Riwaya hii imefungamana na utamaduni wa Waswahili kupitia kijiji cha Kitelevadzi kilichopo katika mkoa wa Njombe nchini Tanzania. Mzee Kazembe na Nyamidze (mke wake) walibahatika kupata watoto kumi na moja, kati ya hao, walioishi walikuwa watoto watatu ambao ni Rafaeli, Gusto na Nandi. Wengine walikufa mfululizo kila walipokaribia umri wa miaka mitano. Nyamidze (mama yake Gusto) alikuwa mchapakazi. Alilima mazao kama mahindi, pareto na njegere. Mara nyingine, alijishughulisha na kusiriba nyumba na kufinyanga vyungu. Watu wa kijijini walieneza sifa za Nyamidze kama moto katika nyasi kavu. Mwandishi wa riwaya hii anamtumia mhusika Gusto ambaye alirithishwa mirathi ya hatari na mzee Kazembe baada ya kufariki. Licha ya Gusto kurithi uchawi kutoka kwa baba yake, familia yake iliamini katika dini ya Ukristo ambayo ilikuwa ikipatikana katika jamii yao. Urithi wa mirathi ya hatari aliorithi Gusto, ulisababisha visasi katika jamii yao na kupelekea vifo vya watu mbalimbali kama vile, Kapedzile, Dina, Nandi na Mama yake Gusto jambo ambalo lilikuwa pigo katika maisha yake. Katika riwaya hii Mung'ong'o pia amesawiri vinywaji, matumizi ya lugha, sanaa na mavazi katika jamii ya Wabena ambayo ni sehemu ya utamaduni wa Waswahili.

4.2.3 Riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu*

Riwaya hii inamhusu Derrick ambaye ni kijana mchapakazi kutoka katika jiji la Shuntown. Alijulikana sehemu mbalimbali katika jiji la Shuntown kutokana na mali alizokuwa anamiliki. Siku zilivyokwenda Derrick alitamani kuoa mwanamke kutoka kijijini kama alivyomwahidi marehemu mama yake. Derrick alifunga safari kurudi kijijini kwa ajili ya kumueleza babu kuhusiana na hitaji lake. Alipokuwa njiani alikutana na msichana mrembo aliyeitwa Kabula. Alivutiwa naye na kuamua kwenda kumtolea posa kwa wazazi wake. Waliandaa harusi kijijini na baadaye alikwenda naye mjini kuendelea na maisha yao. Walipofika mjini, alimtafutia watu wa

kumpamba ili afanane na watu wa mjini. Walimpaka dawa kwenye nywele, wanja katika nyusi na rangi katika midomo yake. Alionekana mwanamke mrembo sana.

Siku zilipita, Derrick aliandaa sherehe ambayo aliwaalika watu kutoka katika maeneo mbalimbali. Miongoni mwa wageni walioalikwa alikuwa Rais wa jamhuri ya Sokomoko aliyeitwa Gabriel. Rais huyo alipomuona Kabula alimtamani na kuahidi kumpata. Baada ya sherehe kuisha, Derrick na Kabula walipata mwaliko kutoka ikulu kwa ajili ya kupata chakula cha jioni. Wakiwa katika maongezi, Rais aliahidi kumpeleka Kabula kusoma Uingereza na kumsaidia kulipa gharama zote zilizohitajika. Hapo ndipo ulikuwa mwanzo wa usaliti baina ya Kabula na Derrick. Kabula alikwenda kusoma Uingereza. Rais alipata nafasi ya kumtembelea huku Derrick akizuiliwa kutoka nje ya nchi. Siku zilipita Kabula alibeba mimba ya Rais Gabriel na kufanikiwa kupata mtoto mmoja aliyeitwa Cythia. Huo ndio ulikuwa mwisho wa mapenzi ya ukweli kati ya Derrick na Kabula. Mwandishi Shigongo amesawiri mavazi, vinywaji, lugha na dini jinsi vilivyo katika kipindi hiki cha utandawazi.

4.2.4 Riwaya ya *Almasi za Bandia*

Riwaya hii iliandikwa mwaka 2010 na Seithy Chachage akiwa na lengo la kuangazia bara la Ulaya na Afrika kwa ujumla. Merton, Zambe na Yakini walipata bahati ya kwenda kusoma barani Ulaya. Wanapofika Ulaya, wanakutana na matatizo kama vile, ubaguzi wa rangi, unyanyasaji wa kijinsia na kutokukubalika kwa wenyeji. Vijana hawa kila ilipofika jioni walipendelea kutembelea sehemu za starehe kama baa ya Wenches ambayo walikutana na wanawake wa kizungu waliotoa huduma katika baa hiyo, wakiwa katika mavazi ya chupi na sidiria ambayo yalikuwa kivutio kikubwa cha watu kutoka bara la Afrika. Katika kumbi hizo za starehe, ilipigwa miziki mbalimbali kama *reggae*, *calypso*, *rumba* na *buffalo soldier*. Kila mmoja alitafuta mwanamke wa kizungu wa kucheza naye. Mwandishi wa riwaya hii anamtumia mhusika Merton ambaye alikuwa mtu bandia katika kila jambo alilolifanya. Alijipa wadhifa mkubwa katika chama kuficha wizi, ubadhirifu wa mali aliokuwa anaufanya na kaka yake Inspekta Gordon. Aliwatumia wanawake kwa ajili ya kujistarehesha akijidai ni mtu mkubwa kwenye chama. Mwisho, ukweli unakuwa wazi. Wizi na ubadhirifu wa almasi uliofanywa na Merton kwa kushirikiana na Inspekta Gordon na Wahindi unafichuka. Mwandishi anaonesha riwaya ya Kiswahili

inavyovuka mipaka kwa kusawiri mavazi, lugha, maadili, kifo, milo na vinywaji kipindi cha utandawazi.

4.3 Vipengele vya Utamaduni wa Waswahili katika Riwaya Teule

Fasihi ikiwamo riwaya ya Kiswahili ni dafina ya kuhifadhi matukio mbalimbali ya kihistoria yaliyopo katika jamii ambayo hurithishwa kizazi kwa kizazi kupitia nyaraka za kifasihi zinazosawiri uhalisi wa maisha uliopo katika jamii (Mulokozi, 1985 na Madumulla, 2009). Riwaya ya *Mirathi ya Hatari* na *Kurwa na Doto* zimehifadhi tamaduni za watu wa Njombe na Unguja mtawalia kwa kuonesha uhalisia wa maisha katika jamii hizo. Sehemu hii inajibu swali mahususi la lengo la kwanza lililolouliza “Ni vipengele gani vya utamaduni wa Waswahili vilivyosawiriwa katika riwaya ya Kiswahili kabla ya zama za utandawazi? Matokeo ya utafiti uliofanyika yanaonesha kuwa kuna vipengele vya utamaduni wa Waswahili vilivyobainika katika riwaya teule ambavyo vinaonesha uamilifu uliobebwa na vipengele hivyo katika jamii. Vipengele vilivyobainika ni lugha, imani za kidini, ndoa, milo na vinywaji, sanaa, kifo na mavazi. Katika kufanikisha ubainishaji wake, mtafiti ameongozwa na misingi ya nadharia ya Sosholojia katika mjadala wake.

4.3.1 Lugha

Kwa mujibu wa TUKI (1990), lugha ni mfumo wa sauti za nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii moja wenye utamaduni mmoja unaofanana ili kuwasiliana. Lugha ni kiungo muhimu katika utamaduni wa jamii fulani kupitia mitindo mbalimbali ya lugha kama kejeli, utani, misimu, mafumbo na lugha za makabila katika kusawiri masuala yanayofungamana na utamaduni wa jamii. Majukumu mbalimbali yanayotekelezwa na lugha yameonesha umuhimu mkubwa katika maisha ya wanajamii. Lugha hutumika kama chombo cha kudumisha umoja na mshikamano katika jamii, kutambulisha mila na desturi, kuhifadhi utamaduni, kuonesha uthamani wa utamaduni, kutambulisha shughuli za jamii na kurithisha amali za jamii kwa kizazi na kizazi (Hymes, 2007 na King’ei, 2010). Waandishi wa riwaya teule wamesawiri utamaduni wa Waswahili kupitia mitindo mbalimbali ya matumizi ya lugha inayosawiri maisha halisi ya wanajamii kupitia mila na desturi zao, lugha ya tasifida na matumizi ya misemo.

Utafiti umebaini kuwapo kwa matumizi ya lugha ambayo yamefungamana na mila na desturi zilizopo katika jamii ya Waswahili. Waandishi wa riwaya teule wamesawiri taratibu na mienendo mbalimbali inayopatikana katika jamii kwa kuonesha namna watu wa jamii wanavyoishi kupitia lugha zao. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kurwa na Doto* jambo hili linathibitishwa na mwandishi kwa kuwatumia Kurwa na Doto waliozaliwa katika jamii ya watu wa Unguja waliofungamana na mila na desturi. Walifanyiwa ada zote zilizopatikana katika jamii yao. Mwandishi katika kuelezea mambo hayo ametumia lugha inayofungamana na maisha ya jamii ya watu wa Unguja kwa kuonesha mila na desturi zilizopo katika jamii. Anatueleza kuwa:

> ….aliwapakata watoto na kuwaadhinia, kesha akawapa majina ya Kurwa na Doto. Yule aliyezaliwa mbele aliitwa Kurwa. Watoto hawa walifanyiwa ada zote, walifungwa vigwe, mvuje na nyimbili wakafunguliwa koo kwa asali na shubiri, na wakarebwa muru na wanja, mikononi, miguuni na usoni wakalazwa ndani ya nyungo za mchele, zenye chuma na kaa, kago la mashetani waovu. Mashimo yalichimbwa nyuma ya nyumba na vitovu vya watoto hao vikazikwa pamoja na makaa, chuma na chumvi. Kabla havijafukiwa vilifudikizwa vijungu vipya tena vikafukiwa na kabla mashimo hayajajaa vizuri palitiwa minazi michanga, yaani kila kitovu kipandwe mnazi (uk. 8-9).

Dondoo hili linaonesha namna mwandishi anavyojinasibisha na jamii ya watu wa Unguja kwa kutumia lugha inayofungamana na maisha yao. Mwandishi ametumia maneno kama vingwe, mvuje na nyimbili akimaanisha dawa za miti shamba zilizowasaidia kufukuza mashetani wabaya ambao wangewadhuru watoto wadogo. Dawa hizi walivalishwa watoto kuwakinga na kila jambo baya ambalo linaweza kutokea. Minazi iliyopandwa juu ya vitovu ina maana maisha ya watoto hao yawe marefu kama minazi, kwa kuwa miti ya minazi huwa mirefu na ina sifa ya kuishi miaka mingi. Imebainika kwamba, matumizi ya lugha kwa kujifungamanisha na mila na desturi za jamii husika, zimesaidia jamii kuelewa matukio ambao yanafanyika ambapo mtu wa nje ilikuwa vigumu kuelewa. Kwa mfano, jamii ya watu wa Unguja walielewa miiko ya kutomruka mama mjamzito wakiwa na moto mkononi. Pia, kupitia lugha zilizosawiri mila na desturi zilijenga ujumi katika mazungumzo ya watu wa jamii husika. Pamoja na hayo, lugha hizi zinaibua hisia kwa wasomaji kurejelea mazingira na matukio halisi kama kupanda vitovu kwenye minazi. Maelezo

yaliyotolewa hapo juu, yanazidi kuthibitishwa kwa mahojiano ya uwandani na Bakari[1] anayeeleza kuwa:

> Katika jamii yetu mtoto anapozaliwa anavalishwa mvuje. Dawa hii hufungwa mkononi au kiunoni kwa mtoto kumkinga na mashetani wabaya. Vitovu vya watoto vinafukiwa chini na kupandiwa miti inayokaa muda mrefu. Miti kama minazi inapandwa juu ya mashimo yanayofukiwa vitovu vya watoto. Wakiwa na imani kuwa mtoto ataishi miaka mingi kama ya mti wa mnazi (Utafiti, 2022).

Vilevile, katika riwaya ya *Mirathi ya Hatari* mwandishi ametumia lugha ya kikabila ambayo imesawiri mila na desturi za Wabena. Lugha hiyo imesaidia kurejelea shughuli zilizofanyika katika jamii hiyo. Mwandishi anathibitisha kwa kusema;

> *"Nye Misoha gya Vakuhu, Nye Vasehe yemwalonguwe*
> *Nye vayangu yetulilumwi, Mpulihe! Mpulihe nene*
> *Yendihwilapangila pahuta? Sindilalonga!Sindilalonga;*
> *Nambi huhodza hela; Idza apa dza baha!*
> *Wonendilemweulu-hadatu,Ihipembihi hinyanyade…!"*
> (uk. 16-17).
> **Tafsiri yake:**
> Enyi mahoka wa mababu,
> Enyi wazee mliotutangulia;
> Enyi wenzangu sikilizeni kiapo changu!
> Sitasema wala kuwaza lolote, la ndani ni la ndani!
> Nishindwe mara tatu, pembe hili linichome moto.

Katika nukuu hiyo, mwandishi anadhihirisha jinsi lugha ya kikabila ilivyobeba kwa ukamilifu imani za kichawi zilizopo katika jamii ya Wabena. Mwandishi amemtumia Gusto kuapa kwa mahoka ili aweze kupokelewa na kuingia rasmi katika shughuli za kichawi. Lugha hii ilisaidia kueleweka kwa mambo yaliyokuwa yanafanyika kipindi cha kumuapisha Gusto. Kwa upande wa data za uwandani, Wikunge[2] alisema:

> Mwandishi amesawiri lugha za kienyeji ambazo zilitumika kwa ajili ya kutambulisha utamaduni uliopo katika jamii. Lugha hizi za kikabila zilibeba thamani na amali zilizopatikana katika jamii. Matumizi ya lugha za kikabila yanasaidia kutangaza mila na desturi

[1] Bi. Asha Bakari ni mwanafunzi wa Shahada ya awali ya fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 14/6/2022 katika madarasa ya CHSS.

[2] Bi. Velmunda Wikunge ni mwanafunzi wa Shahada ya awali katika fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 15/5/2022 katika madarasa ya CHSS.

> kwa wageni na kuonyesha ustaarabu uliopatikana katika jamii za Waswahili (Utafiti, 2022).

Kama ambavyo imekwisha elezwa katika mjadala uliotangulia dondoo hili linaonesha, jinsi ambavyo riwaya teule imetumia lugha kulingana na mfungamano wa masuala yanayopatikana katika jamii. Lugha hizi zimebeba thamani na amali za kitamaduni zilizopo katika jamii husika. Kama ilivyoelezwa katika nadharia ya Sosholojia msingi wa fasihi ni ubunifu kutoka katika jamii, inaakisi lugha zilizopo katika jamii zinazosawiri mila na desturi kulingana na maisha yaliyopo katika jamii. Kwa ujumla, utafiti umebaini kuwa mila na desturi zilizopo katika jamii zinaweza kubebwa katika lugha na kuwasilisha uamilifu wake kupitia matukio mbalimbali yanayopatikana katika jamii. Wa Thiongo (1986) anashadidia kuwa lugha ya jamii ni amali ya utamaduni uliopo katika jamii husika. Wanajamii wanatakiwa kuitumia ili kuendelea kutangaza utamaduni wa jamii yao kupitia lugha inayotambulika katika jamii.

Fauka ya hayo, matokeo yanaonesha riwaya hizi zimetumia misemo inayofungamana na muktadha wa maisha ya Waswahili. Misemo hiyo imebeba taswira ya maisha yaliyopo katika jamii husika na jinsi wanajamii wanavyoendesha shughuli zao za kila siku. Mwandishi wa riwaya ya *Kurwa na Doto* anadhihirisha hilo kwa kutumia misemo mbalimbali inayofungamana na mazingira ya jamii. Anasema:

> Mwishoni waliwekwa kizingitini wakashindiliwa roho zao kwa kuwekewa dole gumba la mguu na mchi wa kutwangia na huku wanaomboleza na kuambiwa, “Watoto mnashindiliwa shingo zenu ili mkinai roho zenu na mtakavyoviona, msije mkaruka roho mkiona vitu vya watu, wala msiombe vitu vya watu roho zenu zikinai na ziwe ngumu kama mawe” (uk.9).

Dondoo hili linaonesha kuwa misemo katika jamii ya Waswahili hubeba maana ambayo husisitiza utunzaji wa maadili na makatazo mbalimbali katika jamii. Baada ya Kurwa na Doto kuzaliwa, kama ilivyo ada siku ya saba walitolewa nje kwa ajili ya kuona jua. Sherehe hiyo iliambatana na mambo mbalimbali kama kuombewa dua ya kuwa watoto wasikivu kwa wazazi wao. Mwandishi anatumia msemo wa “roho zenu zikinai na ziwe ngumu kama mawe’’ akiwa na maana Kurwa na Doto watakapokua waachane na tamaa na kuridhika na vitu walivyonavyo. Utafiti umebaini kuwa, misemo hii imetumika kuonya, kukosoa na

kufunza watoto maadili yanayofungamana na miiko iliyopo katika jamii. Hivyo, mwandishi anajifungamanisha na utamaduni wa Waswahili kwa kujenga maadili yanayotakiwa katika jamii kupitia misemo. Pia, mwandishi anadhihirisha imani zilizopo katika jamii kupitia misemo kwa kusema:

> Mamaye na nduguye asione neno, kwani haya ni makadara na mwanadamu hawezi kuyaepuka. Landikwalo ndilo liwalo mja hana hiari (uk. 25).

Kupitia nukuu hii, imebainika kuwa misemo hufungamana na kuonesha imani za dini zilizopo kwa watu wa Unguja. Mwandishi anatumia msemo wa "Landikwalo ndilo liwalo mja hana hiari" akiwa na maana kuwa Mungu ndiye mpangaji wa kila jambo kwa kila binadamu. Kurwa pamoja na mama yake wanaamini kitendo cha Doto kuolewa na Faki ambaye alikuwa mchumba wa Kurwa ni majaliwa na mipango ya Mungu. Vilevile, katika riwaya ya *Mirathi ya Hatari* misemo imetumika kuelezea mambo yaliyopo katika jamii ya Wabena. Mwandishi anasema:

> …Lakini sasa ghafla nilikuwa nimeachiwa madaraka haya mazito. Laiti baba angekuwa hai bado ningekubali aninyime radhi kuliko kuipokea kazi hii. Na falaula ningefahamu tangu skuli juu ya jambo hili kamwe nisingethubutu kurudi! Lakini majuto ni mjukuu. Nilikuwa nimeangamia!. Neno la akataye roho si la kukataa! (uk.13).

Katika dondoo hili, tunaoneshwa Gusto alivyorithishwa uchawi na baba yake kwa ajili ya kuendeleza kazi hiyo. Mwandishi ametumia msemo wa "Neno la akataye roho si la kukataa" akiwa na maana haitakiwi kukataa wosia ulioachwa na marehemu. Gusto analazimika kufanya kazi ya uchawi, kutii wosia ambao umeachwa na Mzee Kazembe. Katika jamii ya Waswahili, wanaamini wosia wa marehemu haukataliwi kwa mtu aliyeachiwa. Hoja hii inashadidiwa na nadharia ya Sosholojia msingi wa fasihi huonesha ubunifu kutoka katika mazingira ya jamii, ambapo mwandishi ametumia misemo kwa kufungamana na mazingira yanayopatikana katika jamii. Katika mahojiano ya uwandani, Lukas[3] anathibitisha kwa kusema:

> Mazingira yalibeba misemo mbalimbali iliyokuwa na maana kulingana na maisha ya jamii hiyo. Watu waliopatikana katika maeneo ya pwani walijishughulisha na uvuvi na waliongozwa na

[3] Bw. Maxwell Lukas ni mwanafunzi wa Shahada ya awali ya fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 17/5/2022 katika eneo la studio ya CBSL.

> misemo kama “usisahau ubaharia kwa sababu ya unahodha”. Pia, waandishi wamesawiri misemo kulingana na jamii wanazotoka, waliburudika na kueneza utamaduni wao kupitia misemo hiyo (Utafiti, 2022).

Nukuu hii inaonesha kwamba misemo hutumika katika mazingira ya jamii kwa kutambulisha shughuli zinazofanyika katika jamii. Lukas (ktj) katika kushadidia maelezo yake ametumia msemo wa “Usisahau ubaharia kwa sababu ya unahodha” ukiwa na maana ya kutambulisha shughuli za uvuvi zilizokuwa zikiendelea katika maeneo ya pwani. Imebainika kuwa, matumizi ya misemo katika jamii ya Waswahili imesaidia kueneza utamaduni wa Waswahili na kuifanya kujulikana kwa watu wengine kutokana na misemo kupendwa na watu wengi. Pia, katika jamii hizo misemo inatumika kama sehemu ya burudani kwa jamii.

Aidha, riwaya hizi zimetumia lugha ya tasifida katika kutunza maadili yaliyopo katika jamii. Waandishi wa riwaya teule wametumia lugha inayoendana na miiko inayopatikana katika jamii katika kudumisha na kuendeleza maadili yaliyopo katika jamii. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kurwa na Doto* mwandishi anadhihirisha matumizi ya lugha ya tasifida ambayo imebeba taswira ya Waswahili wa Unguja. Mwandishi anathibitisha hili kwa kusema:

> Baada ya miezi, Faki alirudi safarini. Kabla ya siku nyingi hazijapita, vibilifitina na kina pangu pakavu tia mchuzi walimwelezea Faki kadhia yote iliyokuwa ikipita yeye hayupo. Kwanza Faki asisadiki akaona ni uwongo Doto hawezi kufanya hivyo kwa mapenzi wanavyopendana. Faki aliziba macho na kutia komango masikioni asisikie yanayosemwa. Mapenzi yalimtia upofu na uziwi (uk. 37).

Nukuu hii, inaonesha mwandishi alivyotumia lugha ya staha katika kuwaelezea wambea ambao walikuwa wanampa maneno Faki kuhusu mkewe Doto. Mwandishi ametumia maneno kama “Vibilifitina” akiwa na maana ya wanafiki na “Pangu pakavu tia mchuzi” akiwa na maana ya watu ambao ni masikini. Utafiti umebaini kuwa, matumizi ya lugha ya tasifida yana umuhimu kwa jamii katika kuleta heshima ya mazungumzo baina ya wazungumzaji kwa kuzingatia mipaka yao. Pia, lugha ya tasifida imesaidia kuendeleza utamaduni wa jamii kupitia maneno mbalimbali

ambayo yanatunza maadili kwa jamii. Katika mahojiano ya uwandani, Khamis[4] anathibitisha hilo kwa kusema:

> Waswahili katika jamii yetu tuna lugha ambazo ndizo msingi katika maisha yetu. Lugha zetu zimejaa tasifida na staha. Haikuwa rahisi mtu kupata picha ya moja kwa moja kwa yale yaliyozungumzwa, huo ndio utamaduni wetu kwani umejikita katika usiri (Utafiti, 2022).

Mawazo ya Khamis (ktj) yanathibitisha kuwa katika jamii ya Waswahili lugha za tasifida zinatunza heshima na kuhifadhi taswira ya maisha ya wanajamii. Mazungumzo yaliyofanyika yalitumia lugha ya siri ambayo ilikuwa ngumu kwa mtu asiyehusika kuelewa ujumbe uliokusudiwa. Lugha hizo zilifungamana na misingi ya kimaadili iliyokuwapo katika jamii. Vilevile, mwandishi wa *Mirathi ya Hatari* anathibitisha matumizi ya lugha ya tasifida kwa kumtumia Mzee Malipula alipokuwa anamwambia Gusto ana mahusiano na Dina bintiye. Alitumia msemo kupunguza ukali wa maneno. Mwandishi anadokeza kuwa:

> …. Usiniletee ujanja wa kitoto, ewe punguani" Alifoka Malipula sauti yake ingemfanya panya ajikunyate shimoni mwake. Tangu lini kinda la mwewe likaacha kukamata vifaranga? Ee nafahamu pia wewe si mgeni kwa binti yangu. Lakini hilo si juu yangu kulishtaki (uk. 44-45).

Nukuu hii inaonesha namna Mzee Malipula alivyokuwa anafoka kwa hasira kutokana na kifo cha Kapedzile. Aliamini Gusto alishirikiana na wachawi wenzake kuondoa uhai wa Kapedzile. Malipula alimwambia Gusto kuwa "Nafahamu wewe si mgeni kwa binti yangu" akimaanisha anafahamu Gusto ana mahusiano ya kimapenzi na binti yake Dina. Jambo hilo Malipula hakuwa radhi nalo kwani aliamini Gusto hamfai binti yake kwa sababu familia yake inajihusisha na uchawi. Mwandishi amesawiri jamii kupitia lugha ya tasifida iliyohifadhi maadili yaliyopo katika jamii, jambo hili linathibitishwa na nadharia ya Sosholojia kupitia msingi unaosema kuwa mambo yaliyopo katika fasihi ni ujumi na ubunifu uliopo katika jamii. Waandishi wa riwaya teule wametumia lugha za tasifida ambazo zinakubalika katika jamii kusawiri

[4] Dkt. Tatu Khamis ni mhadhiri katika idara ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Pia, ni mzawa wa Unguja, mahojiano yalifanyika tarehe 17/6/2022 ofisini kwake.

uhalisia uliopo katika jamii ya Waswahili. Katika mahojiano ya uwandani, Kihongosi[5] alisema:

> Riwaya za waandishi nguli wa mwanzo katika masuala ya lugha walitumia sana lugha ya mficho kupunguza ukali wa maneno. Walipamba lugha zao kwa kutumia maneno ya staha katika lugha husika. Msomaji alipata burudani kutokana na ubunifu wa lugha uliopatikana katika kazi za kifasihi. Waandishi walijifungamanisha na utamaduni wa Waswahili wa kutumia lugha yenye maadili ili kufikisha ujumbe. Mambo haya yalipatikana katika maisha halisi ya jamii (Utafiti, 2022).

Kinachobainika katika nukuu hii ni kwamba, riwaya zilizoandikwa na waandishi wa awali zilitumia lugha ya mficho ili kupunguza ukali wa maneno. Riwaya hizi zilitunza na kuhifadhi maadili kwa kutumia lugha kubalifu katika jamii. Waandishi wametumia maneno ambayo yalitambulisha jamii kupitia lugha za staha. Senkoro, (1984) anashadidia matumizi ya lugha ya staha pamoja na tamathali za semi kuwa hutumiwa na waandishi kupamba lugha na kuhakikisha lugha inakuwa na mvuto katika kazi za kifasihi. Pia, lugha ya staha ilisaidia kutambulisha taswira ya maisha ya jamii ambayo mwandishi ametoka.

4.3.2 Imani za Dini

Wataalamu mbalimbali waliochambua masuala ya dini wanakubaliana kuwa kuna mfungamano mkubwa kati ya dini za kijadi na utamaduni kupitia miungu iliyopo katika jamii. Waafrika wakiwamo Waswahili katika mfumo wao wa maisha, wamekita imani zao katika miungu iliyopatikana katika jamii zao. Waafrika walikuwa na miungu ya aina mbalimbali kama ya mvua, neema, kisasi na uzao. Miungu hii iliwasaidia katika kutatua matatizo yaliyokuwa yanapatikana katika jamii. Kwa mfano, mvua ikiwa haijanyesha kwa muda mrefu katika jamii, waliomba kwa miungu ya mvua kuruhusu mvua kunyesha. Pia, iliongoza jamii katika ufunuo wa masuala ambayo yatatokea katika jamii. Ujio wa dini za kigeni katika maisha ya Waswahili ulileta dini za Ukristo na Uislamu ambazo Waswahili walimwabudu Mungu kupitia dini hizo (Sanga, 2018).

[5] Bw. Eloi Kihongosi ni mwanafunzi wa Shahada ya awali ya fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 17/5/2022 katika eneo la studio ya CBSL.

Utafiti umebaini kuwa, imani za kijadi hubeba matukio ya kitamaduni katika jamii. Mwandishi wa riwaya ya *Kurwa na Doto* anadhihirisha imani za kijadi zilizopo katika jamii ya Unguja zilivyosawiri matukio ya kitamaduni. Mwandishi anathibitisha kwa kusema:

> Siku moja kabla ya kukoga mwaka, mizimu, mapango na makaburi yalisemezwa na kupewa ada zao. Kadhalika siku hii makohani baada ya kutazamia waliona ya kuwa mji utataka kuzinguliwa kwa dhikiri na kurani pamoja na kuzungushiwa ngombe wenye rangi tatu, weupe, weusi na wekundu (uk. 31).

Ni wazi kwamba, watu wa Unguja kila mwaka walikuwa na sherehe ya kukoga mwaka ambayo lengo lake lilikuwa kujisafisha na kuanza maisha mapya kwa wanajamii. Sherehe hizi zilikuwa za kitamaduni, zilihusisha imani za kijadi kama kusemesha makaburi, mapango na kuhudumia mizimu kwa kutoa kafara ili kuanza mwaka vizuri. Utamaduni huu ulidumishwa na kuenziwa na wanajamii wa Unguja kila mwaka. Katika mahojiano ya uwandani, Abasi[6] anathibitisha kwa kusema:

> Katika sherehe za kukoga mwaka ambazo mara nyingi zilifanyika mwezi Juni na Julai, watu walikusanyika kwa pamoja wakiwa na mavuno ya mazao. Zoezi hili liliambatana na kusameheana kwa wanajamii huku kibanda kikiunguzwa moto ikiwa ni ishara ya kuachana na mambo yaliyopita na kuanza mambo mapya. Watu walikwenda kutembelea makaburi na kuwaombea dua marehemu ya kuwaondoa katika adhabu kali. Mambo haya yaliheshimika katika jamii kwa kuwa yalibeba utamaduni wa jamii (Utafiti, 2022).

Katika dondoo hili imebainika kwamba, katika jamii ya watu wa Unguja sherehe ya kukoga mwaka ziliwaweka watu pamoja na kuendesha matukio mbalimbali ambayo yalikuwa ya msingi katika jamii zao. Tukio la kuchoma moto kibanda liliwasaidia watu waliokosana kusameheana, kuachana na ugomvi, migogoro na visasi. Hivyo, sherehe hizo zilirudisha umoja na mshikamano katika jamii na kusisitiza upendo miongoni mwa wanajamii. Imani hizi zilifungamana na utamaduni wa Waswahili ambao unasisitiza umoja na mshikamamo katika jamii. Matokeo yanaonesha, sherehe za kukoga mwaka hazikuleta msamaha tu katika jamii bali ilikuwa sehemu ya burudani kwa wanajamii kupitia michezo kama nyimbo, ngoma, mashairi na

[6] Bw. Twalha Abasi ni mwanafunzi wa Shahada ya awali katika fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 19/5/2022 katika madarasa ya CHSS.

kuogelea yaliyokuwa yanafanyika wakati wa sherehe za kukoga mwaka. Vilevile, mwandishi wa *Mirathi ya Hatari* anathibitisha imani za kijadi zilizopo katika jamii ya Wabena ambapo ziliwasaidia katika kutekeleza majukumu. Mwandishi anaeleza kuwa:

> Enyi mahoka wa mababu;
> Enyi wazee mliotutangulia
> Enyi wenzangu
> Sikilizeni kiapo changu!
> Sitasema wala kuwaza lolote
> La ndani ni la ndani
> Nishindwe mara tatu,
> Pembe hili linichome moto…! (uk. 17).

Nukuu hii inaonesha namna Mzee Mavengi na wachawi wengine walivyokuwa wanaamini katika mizimu ya mababu waliotangulia. Gusto aliapa kwa mizimu na kujifunga katika kiapo chake. Endapo Gusto atakwenda kinyume na kiapo alitakiwa kuchomwa moto na pembe. Dini za kijadi zilifungamanishwa na maisha halisi ya jamii ya Waswahili kwa kuongea moja kwa moja na mahoka katika mazingira yao. Waswahili waliamini mahoka wana nguvu ya kusikia maombi na kutatua matatizo yao. Jambo hili linathibitishwa kupitia nadharia ya Sosholojia msingi wa umahususi ambao huiona kila jamii ina upekee na kutofautiana katika masuala mbalimbali yaliyopo katika jamii. Imani jadi zilizopatikana katika jamii ya Unguja na Njombe zimeonesha umahususi uliopo katika jamii hizo na hubeba dhima kwa watu wa jamii zao. Katika mahojiano ya uwandani, Ngao[7] anasema:

> Waswahili walikuwa wanaamini wahenga, endapo jamii itakuwa na tatizo walitamani kuwaambia mababu zao waliamini wanawasikia. Tamaduni za kijadi ziliendelea kuwa na umuhimu mkubwa katika jamii. Watu walikuwa na umoja. Waliamini endapo shida itatokea katika jamii, wahenga watasaidia katika kutatua. Maeneo ya mapangoni na makaburini zilikuwa sehemu muhimu kwa ajili ya kutoa kafara ili mambo yaweze kwenda vizuri (Utafiti, 2022).

Waswahili wanaamini katika dini jadi ambazo zilikuwa zinafanyika katika jamii. Walishiriki kutoa kafara ya viumbe. Walipokuwa wanaomba dua zao kwa wahenga, waliamini dua zao zinasikiwa. Maeneo ya mapangoni na makaburini yalikuwa ni

[7] Bw. Daniel Ngao ni mwanafunzi wa Shahada ya awali katika fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 30/5/2022 katika vimbweta vya CHSS.

sehemu maalumu kwa ajili ya kwenda kuongea na mababu kutokana na mahitaji ya jamii. Imani hizi za kijadi zilifanya jamii kuwa na umoja katika kutatua shida zilizokuwa zinatokea katika jamii zao. Matokeo yanaonesha kuwa, maeneo yenye mawe makubwa na miti mikubwa zilikuwa sehemu maalumu ambazo ziliheshimiwa. Kutokana na kuamini katika maeneo hayo, walikwenda kuongea na miungu kwa ajili ya kutatua shida zilizopo katika jamii. Hivyo, imani za kijadi zimefungamana na masuala ya kitamaduni yaliyopo katika jamii za Waswahili. Awolalu, (1976) anashadidia kuwa Waafrika wana dini zao za kijadi ambazo ndizo zilikuwa zikitumiwa na watu hao katika kuhakikisha wanaabudu na kuwa na imani katika yale ambayo yalikuwa yanahitajika kupatikana katika maisha yao ya kila siku. Mbiti (2011) anamuunga mkono Awolalu kwa kusema, Waafrika wakiwamo Waswahili bado wanaheshimu dini za jadi walizozikuta katika jamii. Wanaamini katika kupata mahitaji yao, kupitia dini za jadi ambazo ndiyo asili yao kabla ya ujio wa wageni na kuleta dini mpya ambazo ziliwafanya waonekana kama wanaamini mambo ya kigeni.

Aidha, Matokeo yanaonesha kuwa Waswahili wanamwamini Mungu kupitia dini za Kimagharibi yaani Ukristo na Uislamu. Dini za kigeni zimesawiriwa katika riwaya teule kuonesha jinsi Waswahili wanavyofungamana na masuala ya kidini katika jamii zao. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kurwa na Doto* mwandishi anaonesha namna watu wa jamii ya Unguja walivyofungamana na dini ya Kiislamu. Mwandishi anathibitisha kwa kusema:

> Watoto hao walitiwa chuoni kusoma Kuraani, dini, kuandika na mambo mengine. Walipelekwa chuoni kwa ada ya kutoa rupia nne, rupia mbili na ufito wa kila mtoto. Walipofika *Lam Yakuni*, walipeleka mizigo ya kuni; walipofika Iqra Biismi walipeleka mizigo ya kuni; (uk. 10).

Nukuu hii inaonesha namna wakazi wa Unguja walivyofungamana na dini ya Kiislamu ambayo inafunza maadili yanayotakiwa katika jamii yao. Kurwa na Doto walipelekwa chuoni kwa ajili ya kujifunza elimu ya kidini na shughuli mbalimbali zilizowaandaa kuwa watoto bora katika jamii hiyo. Walijifunza kuchota maji, kupika,

kufagia na kutafuta kuni. Mambo haya yaliwasaidia kujifunza majukumu yaliyokuwapo katika jamii. Katika mahojiano ya uwandani, Abasi[8] anasema:

> Katika jamii watoto wakikua wanapelekwa madrasa kwa ajili ya kujifunza Kuraani na kuifahamu. Tuliamini kwa kumpeleka mtoto chuo atafunzwa maadili kuhusiana na dini ya Kiislamu ambayo yatakuwa mwongozo kwa watoto katika jamii (Utafiti, 2022).

Abasi (ktj) katika mahojiano anaweka wazi kuwa, wazazi waliwapeleka watoto wao kupata elimu ya kidini wakiwa na matumaini watoto hao, wataijua Kuraani vizuri na watapata mawaidha ambayo yatakuwa mwongozo wa maisha ya watoto katika jamii. Watoto walijifunza maadili kutokana na misingi ya dini ya Kiislamu kama vile, namna ya kuvaa na kufanya kazi vizuri katika jamii zao. Kwa ujumla, katika jamii ya Waswahili dini imekuwa wakala mkubwa wa kufundisha malezi kwa watu wa rika mbalimbali wakubwa kwa wadogo. Dini humtengeneza mtu kuwa na hofu ya kufanya mambo ambayo hayakiuki misingi ya kimaadili iliyopo katika jamii. Hivyo, utamaduni wa Waswahili umefungamana na masuala ya kidini ambayo yanasisitiza katika ujenzi wa maadili katika jamii. Vilevile, katika riwaya ya *Mirathi ya Hatari* mwandishi amesawiri dini ya Kikristo katika jamii ya Wabena. Mwandishi anathibitisha kwa kusema:

> "…Niliporudi niliingia chumbani, nikavaa nguo zangu rasmi tayari kwenda kanisani. Si kitambo baadaye dada alileta kifungua kinywa katika sinia kubwa, nikalipokea nikisema, "Hivi mama amekwenda wapi?"
>
> "Amekwenda kanisani", alinijibu akiondoa vitu mezani (uk.22).

Kupitia dondoo hili imebainika kuwa, katika jamii ya akina Gusto, walipokea dini za Kikristo juujuu, lakini uzito waliuweka katika dini za kijadi. Wanakwenda mchana kanisani usiku waendelea kuwanga na kufanya ibada katika mapango. Mwandishi anamtumia mhusika Gusto ambaye usiku alikwenda kuwanga na kumtoa kafara mjomba wake (Kapedzile) na mchana alikwenda kanisani kusali. Dondoo hili linathibisha kuwa dini za kigeni zilizopo katika jamii ya akina Gusto bado hazina nguvu kama dini za kijadi ambazo zilikuwa katika mazingira ya jamii husika, kama

[8] Bw. Omari Abasi ni mwanafunzi wa Shahada ya awali katika fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 28/6/2022 katika madarasa ya CHSS.

ilivyoelezwa katika nadharia ya Sosholojia msingi wa mhakiki wa kazi ya fasihi anapohakiki azingatie muktadha na mazingira ambayo mwandishi ametoka. Jambo hili linajidhihirisha katika riwaya teule kwani waandishi wamesawiri imani za kidini kulingana na mazingira ambayo wanatoka. Katika mahojiano ya uwandani, Kihongosi (ktj) anasema:

> Waswahili licha ya kuamini katika mizimu lakini wanaamini katika nguvu ambayo inatoka kwa Mungu ambayo kila binadamu anaitumaini kwa kuwa ndiyo iliyoumba vitu vyote katika ulimwengu. Jamii ya Wabena imetawaliwa na Wakristo ambao wanaamini Mungu ndiye mpangaji wa kila jambo linalotokea katika maisha (Utafiti, 2022).

Dondoo hili linaonesha Waswahili katika maisha yao wanategemea miungu na Mungu kupata msaada katika maisha na kuhakikisha wanapata ulinzi wa kufanya masuala mbalimbali katika jamii. Mbiti, (1970) anashadidia kuwa Waafrika wakiwamo Waswahili wanatofautiana katika kuamini lakini jamii inamwamini Mungu mkuu anayepatikana katika mbingu anayeruhusu jambo lolote kutokea kwa wakati ambao amepanga.

4.3.3 Milo na Vinywaji

Utamaduni wa Waswahili umefungamana na mfumo milo na vinywaji ambavyo vinapatikana katika jamii zao, na namna inavyowatofautisha na jamii zingine. Waswahili katika suala la milo na vinywaji hutambulika kupitia majina ya vyakula na vinywaji, mikao wakati wa chakula, maandalizi ya chakula, aina za milo, vyombo vinavyotumika katika kuandaa chakula pamoja na adabu wakati wa chakula. Masuala mengine ni kama vile, kusubiriana wakati wa chakula, kutokuwa wachoyo na kutomaliza chakula chote. Mambo haya huifanya jamii ya Waswahili kuwa ya kipekee kutokana na taratibu za milo na vinywaji vilivyopo katika jamii (Sengo, 1992, John, 2018 na Isack, 2020).

Matokeo yanaonesha kwamba, milo imetumika kama sehemu ya kudumisha umoja na mshikamano katika jamii. Waandishi wa riwaya teule wamesawiri jinsi vyakula vilivyowaweka watu pamoja katika kushirikiana kwenye matukio mbalimbali kama sherehe na misiba. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kurwa na Doto* mwandishi

anaonesha watu wa Unguja walivyoshirikiana katika arobaini ya mama yake Kurwa na Doto. Mwandishi anathibitisha hilo kwa kusema:

> Mama alipokoga arobaini, palichinjwa mbuzi yaani akika ya watoto hao. Nyama ilipikiwa mafungu na kugawiwa, nyingine ilichomwa na kuliwa kwenye maulidi ya wanawake; nyingine ilipikwa chakula kilicholiwa kwenye maulidi ya wanaume. (uk.10).

Nukuu hii inaonesha jinsi ambavyo wanawake na wanaume walikusanyika katika maulidi kula chakula kwa pamoja na kufurahia watoto kama ulivyo utamaduni wa Waswahili. Nyama nyingine iligawiwa kwa watu kutokana na utamaduni wa Waswahili kutoruhusu uchoyo, ila umoja ulioleta nguvu katika jamii. Katika mahojiano ya uwandani, Abasi (ktj) anasema:

> Katika jamii ya Waswahili wakati wa chakula ulikuwa muda maalumu kwa ajili ya kurekebishana tabia. Mtoto aliyekula vibaya alionywa na alielekezwa namna ya kula chakula kwa adabu. Pia, watu wazima walitumia muda huo kusema watoto wenye mienendo ambayo haifai waweze kujirekebisha. Hata kama kuna ugomvi ulikuwa umetokea mambo haya yalitatuliwa wakati wa chakula (Utafiti, 2022).

Dondoo hili linathibitisha kuwa katika jamii ya Waswahili, wakati wa chakula ulikuwa muhimu sana kwa watu. Walitumia muda huo kuwarekebisha watoto ili kula kwa adabu kulingana na misingi ya utamaduni wao. Pia watu wenye tabia ambazo hazifungamani na jamii zao walionywa kuziacha ili kuendana na taratibu zilizokubalika katika jamii yao. Waswahili walitumia muda wa chakula kutatua migogoro ya kifamilia ambayo imejitokeza. Nadharia ya Sosholojia inasema, mambo yanayojadiliwa katika fasihi yanaonyesha uhalisia uliopo katika jamii. Umoja na mshikamano uliosawiriwa katika riwaya kutokana na chakula unaonesha uhalisia uliopo katika jamii. Kwa ujumla, data za uwandani na maktabani zinaonesha katika jamii ya Waafrika wakiwamo Waswahili, muda wa chakula ulikuwa muhimu kutokana na masuala yaliyokuwa yakizungumzwa. Kila mwanafamilia alitakiwa kuwepo unapofika muda wa chakula. Mipango ya ustawi wa familia ilipangwa na wakati mwingine walitumia lugha ya utani katika kufikisha ujumbe kwa wahusika.

Vilevile, utafiti umebaini kuwa pombe ya asili inasaidia watu kukaa pamoja na kujadili mambo magumu na mazito. Mwandishi wa riwaya ya *Mirathi ya Hatari*

anathibitisha kuwa pombe ilinywewa kusogeza maongezi yaliyokuwa yanaendelea. Anaelezea kuwa:

> Nilitia ulanzi katika bilauri. Ya kwanza nikampa Dina na ya pili nikaishika mimi mwenyewe; nikakivuta kiti na kukaa karibu naye baada ya kukonga ulanzi mara moja nikaweka bilauri mezani nikisema, "Dina, uliniambia katika barua yako kuwa una jambo muhimu unataka kunieleza. Hebu nieleze sasa (uk. 26).

Nukuu hii inaonesha kuwa, Gusto na Dina walikutana kuzungumza kuhusiana na mipango ya siri iliyopangwa na Malipula na mjomba wake Gusto, kuhusiana na kuiangamiza familia ya akina Gusto endapo wataendelea kufuatilia shamba la pareto la Mkomanzi. Kipindi cha mazungumzo hayo Dina na Gusto walikuwa wakinywa pombe. Katika mahojiano ya uwandani, Ngao (ktj) anathibitisha kuwa:

> Pombe katika jamii ilikuwa ni muhimu sana watu wanapokutana kujadili masuala mbalimbali kuhusu jamii. Pombe ilitumika kuonesha ishara ya umoja wa watu waliokuwapo katika jamii fulani. Matukio muhimu kama sherehe, misiba na ujenzi wa makanisa pombe ilitakiwa kuwepo. Watu walifurahi kutunza umoja na mshikamano kupitia pombe (Utafiti, 2022).

Dondoo hili linaonesha kuwa Waswahili wanatumia pombe katika maeneo mbalimbali kama kwenye sherehe, misiba na kujenga makanisa. Pombe iliwaunganisha watu katika kushirikiana kupanga mipango na kutatua shida zilizopo katika jamii. Imebainika kuwa, katika jamii watu hutumia pombe kama utambulisho wa umoja na mshikamano uliopo katika jamii. Mambo haya yanafungamana na masuala ya kitamaduni yaliyopo katika jamii ya Waswahili.

Aidha, matokeo yanaonesha vyombo vilivyotumika kuwekea chakula vilitambulisha ukarimu uliopo katika jamii ya Waswahili. Mwandishi wa riwaya ya *Kurwa na Doto* amesawiri jinsi masinia na makombe yalivyotumika wakati wa chakula. Mwandishi anasema:

> Nyumbani kulipikwa vyakula na nyuji kuwa ni fuka ya mgeni. Jioni sinia na makombe ya michele yalimiminika kumkaribisha mgeni (uk.49).

Nukuu hii inaonesha masinia yalitumika kuwekea chakula wakati wa kula katika jamii ya Waswahili. Vyombo kama sinia vilikuwa na umuhimu kwa Waswahili

kutokana na tabia ya kuwakarimu wageni wakati wa chakula. Masinia yalitumika kuweka chakula ambacho kililiwa na watu wengi. Jambo hili liliwaweka watu pamoja na ilikuwa ni ishara ya umoja wakati wa kula chakula. Pia, katika riwaya ya *Mirathi ya Hatari* mwandishi ametumia vyombo kama sinia na bilauri vilivyotumika katika chakula. Mwandishi anathibitisha katika ukurasa wa 22 kwa kusema, "Si kitambo baadaye dada alileta kifungua kinywa katika sinia kubwa, nikapokea nikasema mama amekwenda wapi?". Hii inathibitisha kuwa Nandi alitumia sinia kumletea Gusto chakula jambo linaloashiria katika jamii ya Waswahili walisisitiza kutokuwa wachoyo katika chakula. Waswahili waliamini iwapo mgeni atatokea muda wa kula itakuwa rahisi kushiriki chakula. Katika mahojiano ya uwandani, Manase[9] anathibitisha jambo hilo kwa kusema:

> Katika jamii ya Waswahili walitumia masinia kuwekea chakula kwa kuwa umoja wa jamii ulikuwa muhimu wakati wa chakula. Wanawake walitengewa chakula chao, wanaume na watoto, lakini walitumia sinia kuendelezea falsafa ya uduara katika mkao wa chakula. Vyombo hivi vilikuwa vya muhimu kwa Waswahili na ukiangalia familia za kipindi hicho zilikuwa na watu wengi (Utafiti, 2022).

Nukuu hii inaonesha wakati wa chakula kila jinsia ilipakuliwa chakula kwenye sinia lake, lengo lilikuwa kuhakikisha umoja wa maisha unaendelezwa kupitia kula pamoja. Kwa ujumla, data za uwandani na maktabani zimeonesha mfumo milo na vinywaji vilivyotumika katika jamii ya Unguja na Njombe kama viwakilishi vya Waswahili waliotambulisha utamaduni wa Waswahili. Sengo, (1992) anashadidia kwa kuonesha mambo muhimu yanayoutambulisha utamaduni wa Waswahili katika jamii zingine kuwa ni uamilifu wa milo na vinywaji katika maisha yao yaliyowatofautisha na watu wa jamii nyingine.

4.3.4 Ndoa

Katika jamii za Waswahili ndoa ni jambo la heshima kijana anapofikia umri wa kuoa au kuolewa. Taratibu zilizokuwapo katika jamii zilifuatwa ili kuhakikisha vijana wanakuwa na ndoa bora inayozingatia mila na desturi za jamii husika. Kwa msichana

[9] Bi. Mahoza Manase ni mwanafunzi wa Shahada ya awali katika fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 3/6/2022 katika madarasa ya CHSS.

alitakiwa kuwa bikira anapotaka kuolewa na suala la kuchaguliwa mchumba lilipewa kipaumbele katika jamii za Kiafrika wakiwamo Waswahili. Muungano kati ya familia mbili ulidumisha undugu wa kushirikiana katika masuala mbalimbali ya kijamii. Pia, Waswahili walithamini uzazi katika maisha ya ndoa. Waliamini endapo wanandoa watafanikiwa kupata watoto, ni ishara ya utajiri na kuacha kumbukumbu kwa jamii endapo wazazi watafariki (Mbaabu,1985 na Faustine, 2017).

Utafiti umebaini kuwa, wazazi walikuwa msingi katika kuwachagulia vijana wachumba. Uchaguzi huo ulijigeza kwenye uzoefu na utafiti baada ya kujiridhisha kuhusu tabia, afya, bidii katika kazi na kuendana kwa utamaduni na familia ambayo wanataka mtoto wao aoe au kuolewa. Suala la wazazi kuwachagulia watoto wao mtu wa kuoa au kuolewa naye lilionekana jambo zuri katika jamii za Kiafrika. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kurwa na Doto* mwandishi amesawiri jambo hili katika jamii ya watu wa Unguja. Anasema:

> …Kurwa kapata rafiki. Haya yaliwafurahisha kwani hilo ni jambo walilokuwa wakitamani, apate mume wa kusema na kusikilizana. Watu wawili hao waliificha siri hiyo ndani ya vifua vyao. Kurwa kila siku uso ukimng'ara kwa furaha na anapokuwa jikoni au pahala pengine popote nyimbo zikimtoka na kuimba kama ndege (uk.16).

Nukuu hii inaonesha jinsi ambavyo mama yake Kurwa alivyokuwa na furaha alipohisi kuwa Kurwa amepata mwanaume atayesikilizana naye, kwamba, baada ya muda mfupi ataolewa. Hii ni kwa sababu ndoa ni baraka kwa Waswahili. Mama yake na Doto baada ya kugundua, walifurahi kwani waliamini Kurwa amepata mwanaume sahihi ndiyo maana wakati wote alikuwa mwenye furaha na kuimba nyimbo. Pia, mwandishi katika riwaya ya *Mirathi ya Hatari* anaonesha kwamba Mzee Malipula hakupenda mahusiano kati ya Gusto na Dina kwa sababu aliamini Gusto hamfai Dina kutokana na tabia ya uchawi. Mwandishi anadhihirisha kwa kusema:

> Lakini Malipula inaonekana kwamba mwali huyu anampenda sana huyo kijana. Alihoji mmoja kati ya wale aliokuwa nao. "Unaonaje kama ungewaacha tu waoane? Lawama yote ya kumpa mkosi ungeikwepa eeh unasemaje?" Malipula alimaka kama aliyetukanwa ghafla. Wewe ni mzee mwenzangu, Kindimba. Umezaa binti kama mimi. Utakubali kweli binti yako aolewe na mwana wa mchawi aliyegeuka shetani? (uk. 41-42).

Dondoo hili linaonesha wazazi walivyokuwa na nguvu katika kutoa baraka au laana kwa watoto katika suala la ndoa. Utafiti umebainisha kwamba, Waswahili waliamini kuwa wazazi wana nguvu na wanajua familia ambayo itamfaa binti au kijana kuoa au kuolewa. Mzee Malipula hakubariki mahusiano kati ya Dina na Gusto kwani aliamini kwamba Gusto hamfai binti yake kwa kuwa familia yake ilijihusisha na masuala ya uchawi. Jambo hili linathibitishwa na nadharia ya Sosholojia kuwa mambo yanayopatikana katika jamii husawiriwa katika fasihi. Suala la kuchagua mwenzi kwa kuwashirikisha wazazi linaonesha upekee uliopo katika jamii ya Waswahili. Katika mahojiano ya uwandani Kihongosi (ktj) anashadidia kwa kutumia methali ya "Utu uzima dawa" akiwa na maana kwamba wazazi ni watu ambao wameyaona mengi katika dunia, wanajua changamoto ambazo ziko kwenye ndoa na walitumika kama watu wenye uzoefu katika maisha ya ndoa. Anaendelea kusema:

> Enzi za mababu na mabibi zetu ndoa ilichukuliwa kama jambo la thamani ambalo lilitakiwa kuheshimiwa. Binti au kijana anapofikia umri wa kuoa au kuolewa wazazi walitakiwa kutafuta familia ambayo inaonekana kuwa bora kwa kijana au binti yao. Wazazi waliaminika kwa kutafuta wenzi ambao ni bora kutokana na vigezo vilivyowekwa katika ukoo wa watu fulani. Hivyo, mpaka sasa kuna baadhi ya jamii hasa za vijijini bado zinawachagulia vijana wenzi wa maisha japokuwa kwa sasa jambo hili halina nguvu sana kutokana na mabadiliko yaliyopo katika jamii (Utafiti, 2022).

Nukuu hii inaonesha kuwa, katika miaka ya zamani ndoa lilikuwa jambo la thamani kutokana na wanajamii walivyokuwa wakiona wazee wa zamani walivyoishi. Wazazi walikuwa kiungo muhimu kwa kijana au binti anapotaka kuoa au kuolewa walifanya uchunguzi katika familia ambayo kijana au binti anatarajia kuolewa au kuoa ndipo walipokwenda kuchumbia. Utafiti umebaini, ndoa hizi zilizokuwa zinahusisha wazazi katika kuchagua mwezi wa maisha, zilidumu kwa muda mrefu. Kwa sasa jambo hili limebaki katika maeneo machache kutokana na kukua kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia. Maitaria (2012) anaendelea kueleza zaidi kuwa ndoa ni nyanja muhimu katika maisha ya mwanadamu katika jamii anayoishi. Anaongezea kuwa kuna ndoa ambazo wazazi, walezi na watu wa ukoo humchagulia mchumba mtoto wao. Ndoa hizi zimefungamana na masuala ya kitamaduni ambapo kijana au binti anapochagua mchumba mwenyewe anakuwa amevunja miiko ya jamii yake. Matokeo yanaonesha kuwa Waswahili waliheshimu taratibu zilizokuwapo katika jamii hizo kupata familia bora.

Aidha, suala la posa lilikuwa jambo la muhimu katika jamii. Matokeo yanaonesha kuwa katika jamii ya watu wa Unguja posa ilisaidia kutambulisha familia mbili zinazotarajia kuoana. Posa ilidumisha undugu na kuweka ukaribu wa kushirikiana katika masuala ya kijamii baina ya familia ya binti na kijana. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kurwa na Doto* mwandishi amesawiri suala la posa kama lilivyo katika jamii yake. Anasema kuwa:

> Siku ya pili, Faki alikuja mwenyewe kuleta posa naye alipokelewa kwa kichwa na miguu akawekwa ndani ya mboni za macho. Posa zilikubaliwa na harusi kubwa ikafanywa. Mama yao na Kurwa waliisherekea na kuisimamia kila kitu. Doto alitengenezwa kila kitu na dada yake bila kuonyeshwa kinyongo chochote. Kwa ajili hiyo wanadamu; gamba kama walivyoitwa hawakukosa la kwamba Kurwa…(uk. 25).

Dondoo hili linaelezea kuwa, Faki alipokwenda kutoa posa kwa ajili ya kumuoa Doto. Posa ilikubaliwa na harusi kati ya Doto na Faki ilifanywa. Kurwa alisimamia kila jambo kuhakikisha Doto anafurahia siku yake. Imebainika kwamba, katika jamii za Waswahili ujio wa posa nyumbani kwa binti lilikuwa jambo la heshima katika familia ambayo binti anatoka na ulikuwa utambulisho rasmi wa familia mbili ambazo zinaenda kuungana kuwa ndugu. Nadharia ya Sosholojia inaeleza kuwa fasihi ni ujumi na ubunifu kutoka katika jamii. Mwandishi anaonesha namna masuala ya posa yaliyopo katika jamii yanavyosawiriwa katika riwaya. Katika mahojiano, Andrea[10] anathibitisha kwa kusema:

> Binti anapopata mchumba huwa anatolewa posa ili kuonyesha uthamani na shukurani kwa familia ya binti. Posa kwa Waswahili huwa ni utaratibu ambao upo katika familia ya binti ambapo ili awe mke halali lazima umtolee posa kuonyesha umiliki na baadaye kufunga ndoa (Utafiti, 2022).

Nukuu hii inaonesha kuwa katika jamii ya Waswahili posa ilienda kwa wazazi wa binti kwa ajili ya kuwashukuru na kutangaza umiliki. Jambo hili liliwaweka karibu ndugu wa upande wa mwanaume na mwanamke kwa lengo la kudumisha undugu. Katika hili Mbaabu (1965) anasema kuwa mahari ilitegemea utamaduni uliopo katika jamii husika. Kwa mfano, nchini Kenya katika jamii ya Wakikuyu, mahari

[10] Bw. Alexander Andrea ni mwanafunzi wa Shahada ya awali katika fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 1/6/2022 katika eneo la studio ya CBSL.

haikuruhusiwa kutolewa kwa mara moja maana waliamini undugu ulioletwa baina ya ndugu wa pande mbili hauishi na mahari si uhai wa ndoa. Utamaduni wa Waswahili uliambatana na kutoa posa ikiwa kijana wa kiume toka familia fulani alikuwa amempenda mtoto wa kike wa familia nyingine. Hivyo, walitoa mahari nusu, na iliyobaki ilimaliziwa taratibu kadri siku zilivyozidi kwenda.

Utafiti umebaini pia kuwa, katika suala la ndoa, wanawake walitakiwa kuwatii na kuwaheshimu wanaume zao. Jambo la muhimu ambalo wanawake walitakiwa kulifanya ni kuhakikisha kuwa ndoa zinadumu na kuepusha migogoro. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kurwa na Doto* mwandishi anaonesha Doto ambavyo hakumtii mumewe na kuharibu ndoa yake. Mwandishi anasema:

> Faki alihama na kumwachia nyumba Doto. Baada ya kupita haya makazi yao na mapenzi yao yalikuwa segemnege na huenda zikapita siku kadhaa ya nyuso zao hazikuonana. Ingawa Doto akipeleka barua kwao na yeye kuletewa kuelezwa kila kitu lakini hajawaarifu kuwa ana ugomvi na Mumewe (uk. 38).

Nukuu hii inaonesha kuwa, Doto aliolewa na Faki na walitegemea kuishi maisha ya furaha na amani lakini baada ya kumwoa, Doto alikuwa mtu ambaye alijichanganya na marafiki kufikia hatua ya kutomtii mume wake. Jambo hili lilisababisha kutokuwa na maelewano kati ya Faki na Doto. Matokeo yake, Faki anachukua maamuzi ya kuondoka nyumbani na kumwachia nyumba Doto, jambo ambalo lilitia dosari katika ndoa yao. Hivyo, Doto anashindwa kueleza ukweli kwa ndugu zake, anafunga safari na kurudi kusalimia nyumbani. Hatimaye, Doto anakutwa na matatizo akiwa kwao na kufikwa na umauti. Mwandishi anasema:

> Baada ya siku nyingi za kupatikana ugomvi na suitafahum, Doto alisita kupeleka barua. Haya yaliwatia wahka watu wake kwani hiyo haikuwa ni desturi yake. Kadhalika kwa mambo yote yaliyompitia Kurwa, Doto hakuja ila alileta barua za huzuni na misaada iliyohitajika (uk.38).

Dondoo hili linaonesha athari za mwanamke kutokuwa mtii kwa mume wake katika ndoa. Doto anasababisha mgogoro katika ndoa yake na kupelekea Faki kuondoka nyumbani. Masuala kama haya hayafungamani na utamaduni wa Waswahili. Mabinti

walipotaka kuolewa walifundishwa kuwa na adabu njema kwa lengo la kukuza ustawi wa familia yao. Katika mahojiano ya uwandani, Lusian[11] anasema:

> Katika jamii ya Waswahili msichana anapoolewa huwa anafundishwa mambo ya kuzingatia katika maisha ya ndoa. Binti anapokiuka miiko ya kitamaduni na ndoa inapovunjika familia hubeba fedheha. Familia ambayo binti ametoka ilitakiwa imchukue binti na kumfundisha upya namna ya kuishi katika ndoa. Jambo hili huleta aibu katika jamii hivyo walitakiwa kuishi kulingana na mafunzo waliyopata ili kutunza heshima ya familia zao kwa watu wanaowazunguka (Utafiti, 2022).

Kama ilivyoelezwa hapo juu katika mjadala, Lusian (ktj) anathibitisha kwa kuonesha kuwa, katika jamii mwanamke anapoolewa anatakiwa kwenda kudumu katika ndoa kutokana na mafunzo ambayo ameyapata. Binti anapokosea inabidi arudishwe nyumbani kwao kwa ajili ya kupewa mafunzo mapya yatakayomsaidia katika ndoa yake. Kuachika katika ndoa lilikuwa ni jambo la aibu kwa familia ya binti kwani jamii iliamini binti amekiuka taratibu za wazazi wake. Masuala haya yalifungamana na maadili ya ndoa yaliyokuwa yanasisitizwa katika jamii ya Waswahili. Vilevile, katika riwaya ya *Mirathi ya Hatari* mwandishi anaonesha namna mama yake Gusto alivyomtii mumewe katika kila jambo ambapo hata alipoumwa alimhudumia. Jambo hili limefungamana na utamaduni wa Waswahili katika jamii yao. Mwandishi anathibisha kwa kusema:

> Kisha akaomba maji ya kunywa na mama akalichukua birika mezani akajaza maji ndani ya bilauri ndogo; akampa. Mzee aliyanywa maji hayo kwa gugumizo moja; akahema kwa uchovu. Kisha aliwapungia mkono waliokuwepo akiwaashiria waondoke (uk. 13).

Nukuu hii inaonesha jinsi utii ulivyokuwa kitu cha muhimu kwa mwanamke katika kutekeleza jambo analoambiwa na mumewe. Familia zilidumu kutokana na utii na walisaidiana katika shida na raha. Jambo hili linaipa upekee jamii ya Waswahili. Katika mahojiano ya uwandani, Manase (ktj) anathibitisha kwa kusema:

> Katika jamii nyingi za Kiafrika mwanamke alitakiwa kuwa chini ya mume wake. Mwanaume anapozungumza jambo anatakiwa kutekeleza na kutii. Kwa mfano, katika jamii ya Wapangwa mwanaume anapokuwa anatoa maagizo, mwanamke anatakiwa

[11] Bw. Haule Lusian ni mwanafunzi wa Shahada ya awali katika fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 30/5/2022 katika eneo la studio ya CBSL.

> kunyamaza kimya na kupiga magoti kuashiria amepokea maagizo. Mambo haya yaliutambulisha utamaduni wa jamii hiyo (Utafiti, 2022).

Dondoo hili linaonesha kwamba, ndoa za Waswahili zilikuwa zinasisitiza wanawake kuwa na adabu na utii katika nyumba zao. Wanaume walitakiwa kuwa kichwa cha familia na mwanamke kuwa pambo kwa mumewe. Aidha, ndoa ilikuwa jambo la thamani sana katika maisha ya Waswahili. Katika hili Sawe (2018) anashadidia kwa kusema mwanamke anatakiwa kuwa na utii na adabu ili kuepusha migogoro ambayo inaweza kutokea. Katika *utenzi wa Mwana kupona*, Binti Mshamu anamwasa binti yake kuishi kwa adabu, heshima na utii kwa mume wake. Data za uwandani na maktabani zinaonesha kuwa utii katika ndoa ni jambo ambalo linasaidia katika kuleta ustawi wa maisha ya ndoa baina ya mwanamke na mwanaume. Mwanamke anatakiwa kuwa mtii katika masuala yenye tija katika kuendeleza ubora wa familia. Wanawake wengi wameishia kunyanyaswa kutokana na kutofahamu haki zao za msingi na kuwa watii hata katika maeneo yasiyostahiki.

Sanjari na hayo, matokeo yanaonesha kuwa uzazi ni jambo la msingi katika maisha ya ndoa. Familia ambayo ilibahatika kupata watoto iliheshimika katika jamii. Watoto wengi ilikuwa ishara ya utajiri katika jamii ya Waswahili na waliamini kuwa watoto wanaendeleza ukoo. Mambo haya yalifungamana na tamaduni zilizopo katika jamii. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kurwa na Doto* mwandishi anaonesha wanajamii walivyofurahi baada ya wazazi wa Kurwa na Doto kupata watoto. Anasema kwamba:

> Vijana hawa waliishi kwa raha na amani kwa muda wa siku nyingi. Baada ya miaka kupita, yule bibi akashika mimba. Haya yaliwafurahisha sana kwani hawajapata kuroja kuzaa. Mimba ikalelewa kwa kila tunu na tamasha. Bwana akimletea mkewe kila kitu, kilichotamaniwa na kisichotamaniwa. Mimba ilikuwa na kuengwaengwa mpaka siku zikatimia. Siku hizo bibi alikuwa hapitiwi na mtu aliyechukua moto, asije akakatwa uzazi (uk. 7-8).

Nukuu hii inaonesha namna wanajamii walivyopokea kwa shangwe mimba ya mama yake Kurwa na Doto kwa kuwa ilikuwa imepita miaka mingi tangu kufunga ndoa bila kushika mimba. Uzazi kwa wanandoa lilikuwa jambo la ufahari na kielelezo cha

uhai wa ndoa kupitia uzao unaopatikana. Katika mahojiano ya uwandani, Shaaban[12] anathibitisha kuwa:

> Katika jamii ya Waswahili watoto ni zawadi na baraka kutoka kwa Mungu. Familia ambayo ilibahatika kupata watoto iliheshimika na kupendwa. Pia, mwanamke ambaye ana uwezo wa kuzaa hupendwa na kuhudumiwa vizuri, ila mwanamke ambaye hakuwa na uzao hudharaulika, na watu huamini ana mikosi. Wanajamii watakwenda kumjulia hali na kumsisitiza kufanya masuala ya kitamaduni ili kuweza kujifungua na kupata watoto watakao endeleza familia yake (Utafiti, 2022).

Nukuu hii inaweka wazi kuwa katika jamii ya Waswahili watoto walihesabika kama baraka kwa wazazi wao. Mwanamke ambaye hakuwa na uwezo wa kupata mtoto alionekana hana thamani katika jamii kwa kuwa Waswahili waliamini mwanamke kamili lazima awe na uwezo wa kupata mtoto. Pia, mwandishi wa *Mirathi ya Hatari* anaonesha familia ya Gusto walibahatika kupata watoto ambao walikuwa furaha kwa familia hiyo. Gusto alikuwa miongoni mwa watoto ambao walichaguliwa kurithi uchawi ambao baba yake aliumiliki katika kipindi cha uhai wake. Hivyo, watoto walitumika kuendeleza mirathi ya wazazi wao wanapoacha urithi. Mwandishi anasema:

> Baba yake Gusto alizungumza "taratibu siku zangu zimekwisha. sidhani kuwa nitaishi zaidi". Sauti yake ilikuwa ya kukwaruza kidogo. Sikuwa na la kumjibu akaendelea kusema, nilikuwa nikishikilia uhai kama mpanda farasi ashikiliavyo hatamu za farasi mtoro ili nikuone kwa mara ya mwisho mwanangu. Na sasa naweza kufa kwa amani. Alipumzika kidogo akanikagua sikuweza kumwangalia usoni mwanangu, nakuachia kazi kubwa. Ni urithi mkubwa ukiutumia vema; bali ni mirathi ya hatari usipojihadhari nayo. Nakuachia dawa zote za milki yangu katika mizungu ya sihiri! (uk. 12).

Nukuu hii inaonesha jinsi ambavyo katika jamii ya Waswahili watoto wanathaminiwa kwa ajili ya kuendeleza shughuli zinazofanywa na wazazi. Gusto ambaye ni mtoto wa familia ya Mzee Kazembe anapewa kurithi mirathi ya hatari ambayo itamsaidia katika maisha yake. Hivyo, Gusto anakubali kuendeleza mirathi ya baba yake kwa kufanya kazi ya uchawi. Katika mahojiano, Lusian (ktj) anasema:

[12] Bi. Safina Shabaan ni mwanafunzi wa Shahada ya awali katika fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 25/5/2022 katika madarasa ya CHSS.

> Kwa jamii za Waswahili, ili ndoa ionekane imetoa matunda ni lazima mwanamke apate uzao. Waswahili wanaamini kuwa amepata chapa na warithi ikitokea wazazi hao wamefariki. Jamii iliona uthamani wa watoto kwani waliwasaidia wazazi wao katika shughuli mbalimbali za kijamii (Utafiti, 2022).

Dondoo hili linaonesha jinsi ambavyo Waswahili wanathamini uzao kwa mwanamke. Imebainika kwamba, mwanamke ambaye hazai alionekana kama hana maana katika jamii ambayo anatoka. Familia hiyo ilionekana ina mikosi kwa kukosa mtoto laana na lawama zilienda katika ukoo ambao mwanamke ametoka. Familia ambayo walipata watoto ilionekana kuwa na baraka kutokana na uzao wa watoto wale waliokuja na furaha katika familia hiyo. Hoja hii inashadidiwa na nadharia ya Sosholojia ambayo inaonesha kuwa masuala yaliyopo katika jamii yanasawiriwa katika kazi za fasihi. Hivyo, waandishi wa riwaya teule wameonesha namna watoto wanavyothaminiwa katika jamii ya Waswahili tofauti na jamii nyingine. Dai hili vilevile, linashadidiwa na Simchimba (2012) anayeeleza kuwa ndoa ni jambo la msingi sana katika maisha ya Waafrika wakiwamo Waswahili na ni kitu muhimu katika kuanzisha familia ambayo huonekana kutokana na uzao wa mke na mume.

4.3.5 Sanaa

Waswahili katika jamii yao wamezungukwa na sanaa mbalimbali kama ngoma, michezo ya watoto, nyimbo, maghani na michezo ya kuigiza. Sanaa hizi zimefungamana na shughuli za maisha ya kila siku pamoja na mila na desturi za jamii husika. Jamii iliweza kurithisha sanaa kizazi hadi kizazi kwa ajili ya kukuza na kutambulisha utamaduni wa jamii husika (Finnegan, 1970 na Mlama, 1981). Ngoma zilizokuwa zinachezwa katika jamii zilibeba utambulisho wa wanajamii kupitia namna walivyokuwa wanavaa. Pia, nyimbo mbalimbali zilizokuwa zikitungwa zililenga kuwaelimisha wanajamii katika masuala yaliyohusu jamii.

Utafiti umebaini kuwa hadithi na vitendawili vilitoa mafunzo na kujenga umoja miongoni mwa wanajamii. Imebainika kuwa, watoto walipenda hadithi na vitendawili ambavyo vilikuwa vinawapa mafunzo ya namna ya kuwa watoto bora wenye maadili kwa jamii. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kurwa na Doto* mwandishi anadhihirisha jambo hili kwa kumtumia Kurwa aliyehadithiwa hadithi na mama yake ili kumpoza na kumpa mafunzo. Mwandishi anasema:

> Saa za jioni Doto anapokuwa hayupo, hajarudi kwenye matembezi na Faki, Kurwa hupumbazwa na mama yake kwa kumfanyia hadithi, vitendawili au michezo kama drama, karata au michezo mingine ya kitoto kama vile mdako, keti, mchezo wa kadinge ngodani na mingi mingineyo. Haya yakimliwaza na kumsahaulisha kidogo (uk. 23).

Nukuu hii inaonesha hadithi na vitendawili alivyokuwa anasimuliwa Kurwa na mama yake vilimsaidia kumliwaza na kumpunguzia msongo wa mawazo. Doto akiwa ametoka na Faki, mama yake alitumia muda huo kumpoza kwa michezo mbalimbali ikiwamo hadithi na vitendawili vilivyomsaidia kumrudisha katika hali ya kawaida na kumfunza namna ya kukubaliana na hali yoyote pindi mambo yanapoenda kinyume na matarajio. Pia, katika riwaya ya *Mirathi ya Hatari* mwandishi anaonesha hadithi zilizosimuliwa wakati wa jioni kuwa zilikuwa na lengo la kupitisha wakati na kutoa elimu katika masuala yanayohusu jamii. Mwandishi anathibitisha kwa kusema:

> Bisi ambazo zingetanzuka waridi nyeupe za wanga zingeshabihi cheko zetu zilizosababishwa na vitendawili na michezo maridhawa iliyotawala nyumba muhula huu; tukapata amani ya kweli. Lakini ngoja aingie baba Lahaula! Uhuru huo uliyeyuka ghafla. Hadithi zilikatishwa katikati na vitendawili vilivyotengwa havikuteguliwa (uk. 4-5) .

Dondoo hili linaonesha namna Gusto na watoto wengine walivyotumia muda wa usiku kusimuliana hadithi na kutega vitendawili jambo ambalo liliwaburudisha na kuwaweka pamoja kushirikiana katika michezo iliyokuwa ikiendelea. Hoja hii inathibitishwa na mawazo yaliyoelezwa katika nadharia ya Sosholojia kuwa mambo yaliyopo katika jamii yanasawiriwa katika fasihi. Waandishi wa riwaya teule wamesawiri hadithi na vitendawili vilivyopo katika jamii kuonesha hali halisi ya maisha. Katika mahojiano ya uwandani, Nchimbi[13] anasema:

> Jamii ya Waswahili hutumia hadithi na vitendawili kama sehemu ya maisha yao. Hadithi na vitendawili mara nyingi vilisimuliwa na kutegwa usiku wakati ambao kazi zote zilikuwa zimekwisha. Hadithi na vitendawili vilieleza ukweli wa maisha yaliyopo katika jamii, watoto walijifunza maadili kupitia hadithi na vitendawili hivyo (Utafiti, 2022).

[13] Bi. Gabriella Nchimbi ni mwanafunzi wa Shahada ya Umahiri kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 17/6/2022 katika madarasa ya CHSS.

Katika dondoo hilo, Nchimbi (ktj) anaweka wazi kuwa, hadithi zilizokuwa zinasimuliwa katika jamii zilikuwa zimebeba picha halisi ya maisha ya wanajamii. Hadithi hizo ziliwafunza watoto shughuli mbalimbali za kijamii na kuishi maisha ya kimaadili kulingana na jamii yao. Imebainika kuwa, kulikuwa na maeneo maalumu kwa ajili ya kusimulia hadithi hizo. Maeneo ya miti mikubwa yalitumika huku wakiwa wanaota moto. Ussi (2015) anaelezea zaidi kwa kusema michezo jadi iliyokuwa inapatikana katika jamii za Kiafrika ilikuwa muhimu katika kutangaza amali za kijamii zilizopatikana katika mazingira husika. Pia, michezo jadi iliyokuwapo katika jamii husika iliwasaidia watoto kuweza kukua katika maadili mema, kujenga afya na kuelimisha jamii juu ya masuala yanayopatikana katika jamii

Aidha, ngoma zilibeba amali za kitamaduni katika jamii husika. Utafiti umebaini kuwa ngoma zilizokuwa zinachezwa katika jamii zilibeba mavazi ya kitamaduni ambayo watu walikuwa wanavaa, zilibeba jumbe kulingana na tukio lililokuwa linaendeshwa katika muktadha fulani wa jamii, kama vile sherehe. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kurwa na Doto* mwandishi anatoa maelezo yafuatayo:

> Sherehe za kuamkia asubuhi ya mwaka zilianza mapema, hata ilipofika kiasi cha saa nne magoma yalikuwa yameshtadi na kila mmoja anahemkwa. Usiku ulikuwa mzuri na mwezi uling'ara sana na kupendeza (uk. 32).

Nukuu hii inaonesha jinsi Waswahili walivyothamini utamaduni wao kupitia ngoma, katika kuendesha sherehe za kukoga mwaka zilizobeba lengo la kusameheana kwa wanajamii. Ngoma zilitumika kuwaweka watu pamoja na kuwaburudisha. Katika mahojiano ya uwandani, Kasoga[14] anasema:

> Katika jamii ngoma ambazo hutumika zilibeba moja kwa moja utamaduni wa maisha ya wanajamii. Jamii huonesha umoja kupita ngoma za asili zilizokuwa katika jamii. Watu walicheza ngoma na kuvaa mavazi asili yaliyotambulisha jamii husika (Utafiti, 2022).

Dondoo hii linashadidia jinsi ngoma ilivyokuwa kitu cha muhimu katika maisha ya Waswahili kwa kudumisha mila na desturi zao. Waswahili walitambulika kupitia mavazi ya asili waliyokuwa wanavaa katika ngoma. Hivyo, utamaduni wa Waswahili

[14] Bi. Nice Kasoga ni mwanafunzi wa Shahada ya Umahiri katika fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 7/6/2022 katika madarasa ya CHSS.

ulidumishwa. Akitoa mawazo yenye kufanana na hoja hii, Brunotti (2005) anaelezea kuwa katika jamii ya Waswahili, ngoma ni kitu muhimu katika maisha yao ya kila siku. Ngoma hutumika kama chombo cha kuisoma jamii, historia na kuelewa maisha ya watu. Mbali na kutumia ngoma kama sehemu ya kufurahia na kupata burudani, Waswahili huitumia kama sehemu ya kuendeleza utamaduni wao.

Vilevile, nyimbo zilitumika kubeba matukio yaliyotokea katika jamii. Matokeo yanaonesha kuwa Waswahili katika jamii yao wana matukio mengi kama sherehe na misiba. Mambo haya yaliambatana na nyimbo kulingana na aina ya tukio linalofanyika. Nyimbo hizo zilibeba dhima mbalimbali kama kufunza jamii, kusifia, kukosoa na kuburudisha. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kurwa na Doto* nyimbo za taarabu zimesawiriwa kutokana na nyimbo hizo kupendwa katika maeneo ya Unguja. Nyimbo hizo zilibeba mafumbo na vijembe vilivyokuwa vinatoa mafunzo na kuburudisha watu katika jamii hiyo. Mwandishi anasema:

> Katika kumfurahisha Kurwa na mama yake, siku moja Faki alipigisha taarabu nyumbani kwao. Waghani wazuri walikuja na taarabu ilisitawi sana. Watu wote walikuja walipumbazika kwa mkabala, nyimbo na vyakula. Taarabu ilikesha mpaka majogoo yaliposikikana (uk. 51).

Dondoo hili linaonesha kuwa nyimbo za taarabu zilikuwa maarufu katika jamii ya Unguja. Nyimbo hizi zilifungamana na utamaduni wa maisha ya pwani kutokana na kukosoa watu kuachana na mambo yasiyofaa. Taarabu hizi ziliwaburudisha watu na kuwapooza na majukumu waliyokuwa nayo kwa muda wa siku nzima. Mwandishi amesawiri taarabu zinazopatikana katika maeneo ya pwani, na nyimbo hizi zilipendwa na watu wa mwambao wa pwani. Vilevile, katika riwaya ya *Mirathi ya Hatari* mwandishi anaonesha wimbo ulioimbwa na mama Tumwene kwa Gusto uliokuwa umebeba manuizo ya kumlinda Gusto dhidi ya maadui wanaomzunguka. Mwandishi anasema:

> Waaidha mama Tumwene alinivisha kitu kama hirizi hivi akawa anaimbilia taratibu:
> ukipatwa na adha
> sihiri hii ikutulize
> ukionwa na hasidi
> fingo hii impumbaze
> utende mambo kwa idhaa
> kago hii ikuongoze…. (uk. 18).

Nukuu hii inaonesha mama Tumwene aliimba wimbo wa kunuiza maneno kwa Gusto. Anaposema hirizi iwe kinga katika maisha yake mapya ya uchawi ina maana kwamba wimbo huu umefungamana na utamaduni wa Waswahili kupitia mila na desturi ambazo zipo katika jamii. Katika mahojiano ya uwandani, Zabron[15] anasema:

> Nyimbo katika jamii ya Waswahili zimebeba utamaduni wa jamii husika. Kila jamii huwa na nyimbo ambazo zikiimbwa zinatambulisha utamaduni wa mahali fulani. Kwa mfano, katika jamii ya Wasukuma kuna nyimbo ambazo ni maalumu kwa harusi, kazi nk. Nyimbo hizo zinakuwa zimebeba ujumbe kwa watu wa jamii yao. Kila atakayesikiliza anatambua utamaduni uliopo katika jamii ya Wasukuma (Utafiti, 2022).

Dondoo hili linaonesha umuhimu wa nyimbo katika jamii ya Waswahili. Nyimbo hizo zilikuwa ni amali ya kutambulisha maisha ya jamii yao. Waswahili walitumia nyimbo kuhakikisha wanaweka jamii kuwa katika maadili yanayotakiwa. Nyimbo huwafundisha watu masuala yanayohusu jamii kwa undani. Kwa mfano, kuna nyimbo mahususi kwa ajili ya ndoa ambapo watu walijifunza maisha ya ndoa kupitia nyimbo ambazo ni utambulisho wa tamaduni za jamii, hivyo, ziliwaonya, ziliwaburudisha na kuwaadilisha. Pia, katika jamii kuna nyimbo zilizokuwa zinahamasisha kufanya kazi kwa bidii. Zilitumiwa na wanajamii wakati wa shughuli zilizoendelea katika jamii husika.

4.3.6 Kifo

Kifo ni jambo ambalo linahuzunisha na kuleta upweke katika jamii. Utamaduni wa Waswahili umefungamana na utaratibu wa uandaaji wa maiti, wosia, urithi na maisha baada ya kifo ambao hutofautiana baina ya jamii moja na nyingine. Jamii za Waswahili wanatazama kifo kama sehemu ya kuwatenga na wapendwa wao kimwili lakini wanaamini wanaweza kuwasiliana kupitia mizimu na ndoto (Sengo, 1992 na Nyonje, 2016).

Aidha, Waswahili wanaamini kwamba kuna maisha baada ya kifo. Utafiti umebaini kuwa Waafrika wakiwapo Waswahili wanaamini maisha ya binadamu yapo katika uduara, yaani, mtu anazaliwa, anakufa na kuwa hai tena katika dunia nyingine. Jamii

[15] Bi. Eva Zabron ni mwanafunzi wa Shahada ya Umahiri katika fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 18/5/2022 katika madarasa ya CHSS.

hizo huwaona marehemu wanaweza kuwasaidia katika kutatua masuala yaliyopo katika jamii yanayowatatiza. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kurwa na Doto* mwandishi anathibitisha kwa kuonesha watu wa Unguja katika sherehe ya kukoga mwaka walikuwa wanaongea na watu ambao wamekufa na kutoa kafara ili maombi yao yapokelewe. Mwandishi anathibisha kwa kusema:

> Siku moja kabla ya kukoga mwaka, mizimu, mapango na makaburi yalisemezwa na kupewa ada zao. Kadhalika siku hii makohani baada ya kutazamia waliona mji utataka kuzinguliwa na dhikiri na kuraani pamoja na kuzungushiwa ng'ombe mwenye rangi tatu, weupe, weusi na wekundu. Asubuhi, watoto walikusanyika nyumbani kwa mkuu wa kiambo ambaye alikuwa mmoja katika watu wanne tangu zama za asili na jadi (uk.31).

Nukuu hii inaonesha sherehe za kukoga mwaka zilizofanywa na watu wa Unguja zilihusisha kusemeza makaburi, mapango na mizimu. Waliamini kwa kusemeza makaburi ya ndugu zao na kutoa kafara, marehemu hao wanauwezo wa kutatua shida za ndugu zao. Katika mahojiano ya uwandani, Abasi (ktj) anathibitisha kwa kusema:

> Katika jamii jambo hili limegawanyika katika mitazamo miwili, wa kiimani na kitamaduni. Kiimani tunaamini watu waliokufa tunapoenda katika makaburi yao kusafisha na kuwaombea dua tunaamini kuwa kama wako katika adhabu mwenyezi Mungu awapunguzie na kama wako pazuri waendelee. Pia, kitamaduni tunaamini kwenda katika makaburi ya watu wenye elimu kubwa wanaweza kutupa baraka na kufanikiwa katika maisha (Utafiti, 2022).

Dondoo hili linaonesha katika jamii kuna watu wanaamini kuna maisha mtu anapokufa. Ndugu wanapoenda kusafisha kaburi na kumuombea wanaamini Mungu anasikia na kumpunguzia adhabu. Pia, katika kutembelea makaburi ya watu wenye elimu ya kidini wanaamini baraka na mafanikio makubwa kama waliyokuwa nayo marehemu yatamfikia muomba dua. Vilevile, mwandishi wa *Mirathi ya Hatari* anaonesha namna Gusto alivyoamini anaongea na Dina baada ya kufa. Mwandishi anashadidia kwa kusema:

> …Pokea zawadi hizi za maua mfuto. Sina zaidi cha kutoa isipokuwa moyo wangu ambao ni mali yako tayari. Nilitulia kidogo nikaendelea nachukua nafasi hii pia kuomba jambo muhimu. Nakusihi unipe heshima ya kujilipiza kisasi kwa Malipula, baba yako ameniumiza vya kutosha na juhudi yangu ya kubaki mpole haina budi kukomea hapo. Moma ni nyoka mpole lakini akichomoza huuma, na akiuma

> sumu yake haina dawa. Dina, nipe fursa hii kwa mara ya mwisho, tafadhari…’’. Kwa mbali nilisikia msalagambo wa chamchela nikashangaa kilitokea wapi (uk.71).

Kama inavyoelezwa katika nukuu hii, Waswahili kama zilivyo jamii nyingine huamini mtu anaweza kuongea na marehemu na akapata majibu ya maombi yake. Gusto anakwenda kaburi la Dina kumpelekea zawadi ya maua, na kuomba ridhaa ya kulipa kisasi kwa Malipula. Baada ya muda kidogo upepo unachukua maua aliyoyaleta Gusto na kuyatawanya. Gusto anaamini Dina amesikia na kupokea zawadi alizompelekea kaburini. Jambo hili linadhihirisha Waswahili wanaamini kuna maisha mengine baada ya kifo. Mtu anapokufa, huendelea kuwasiliana na ndugu waliopo katika ulimwengu. Hivyo, katika suala la kifo jamii ya Waswahili inaonyesha upekee katika suala la kuamini maisha baada ya kifo. Katika mahojiano ya uwandani, Wikunge (ktj) anasema:

> Hata katika jamii yetu tuna utamaduni wa kwenda kusafisha makaburi ya ndugu zetu. Tunapofika tunalimia majani na kuweka maua lakini kabla hatujaondoka kila mtu mwenye shida huenda kulia katika kaburi la ndugu yake akiamini marehemu anaweza kumsaidia katika kupata yaliyo mahitaji yake. Utamaduni huu ulisaidia kuamini kuwa ndugu yetu hatupo naye kimwili lakini kiroho tupo wote na tuliamini anaishi (Utafiti, 2022).

Dondoo hili linaonesha kuwa, katika jamii za Kiafrika wakiwamo Waswahili, suala la kusafisha makaburi ya marehemu na kuomba dua katika makaburi kulionesha ishara ya uhai wa kiroho kwa ndugu zao huku kimwili wakiwa hawako pamoja. Waswahili katika jamii zao bado wana imani kubwa kuwa mtu anapokufa, hubadilika kwenda kuishi katika dunia ya mizimu ambapo huweza kuongea na ndugu zake kupitia njia mbalimbali kama vile, ndotoni au kumtokea katika matukio mbalimbali. Jambo hili linaendeleza utamaduni wa Waswahili kupitia maisha yao baada ya kifo. Temple (1959) anashadidia kuwa Waswahili wanaamini kuwa kuna uhai na kifo ambapo mtu anazaliwa, anaishi na kufa. Hii ina maana kwamba baada ya kufa anaenda kuishi katika dunia ya mizimu na anakuwa na uwezo wa kuongea na ndugu zake.

Matokeo yanaonesha kwamba, Waswahili hutoa wosia kabla ya kufa ili kuendeleza masuala mbalimbali katika jamii. Imebainika kuwa Waswahili wanaamini mtu kabla ya kufa mara nyingi huacha mawaidha ya kuendeleza mambo mazuri au kuachana na

mambo mabaya ambayo hayana tija katika jamii. Mtu kabla ya kufa hutumia muda huo kuwaasa ndugu wanaobaki kuishi maisha mema kwa kuendeleza maadili yanayotakiwa katika jamii. Wosia uliwasaidia wanajamii kuepukana na balaa kwa kuendeleza mambo waliyoshauriwa na ndugu yao kabla ya kufa. Pia, mtu kabla ya kufa alitoa mgawanyo wa mali zake kwa mtu anayetamani kumrithisha kwa ajili ya kuziendeleza. Vilevile, wosia ulisaidia jamii kuepukana na migogoro ambayo inaweza kutokea. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kurwa na Doto* mwandishi anashadidia kwa kumwonesha Doto anatoa wosia kwa Kurwa na kuomba radhi kwa kumkosea na kwa kumchukulia mchumba wake aliyeitwa Faki. Pia anamwomba Kurwa na mama yake kumwombea msamaha kwa Faki kwa mambo mabaya aliyomtendea. Anasema:

> Kurwa na mama yake walimsogelea na kumpa moyo. Doto alilia sana na kutoa buriani na huku anamwomba msamaha ndugu yake kwa uovu alioufanya kwa kumchukulia mchumba wake. Kurwa alikinga chozi na huku anamwambia kuwa amemsamehe duniani na akhera kwa mambo yote aliyoyafanya kisha akamtaka Kurwa na mama yake wamtakie msamaha kwa Faki kwa jeuri na maudhi aliyomfanyia ya kumtilia marafiki ndani. Aliposema hivyo walitanabahi kwa nini kaja peke yake na Faki kaondoka bila kusema alipokwenda au lini anarudi (uk. 41).

Maelezo haya yanazidi kudhihirisha kuwa, mtu kabla ya kufa kama aliwafanyia makosa ndugu, jamaa na marafiki aliomba msamaha ili akifa asiache kinyongo kwa ndugu zake. Waswahili wanaamini kwa kufanya hivyo, duniani na akhera anakuwa amesamehewa katika matendo mabaya. Doto kabla ya kufa anamwomba Kurwa msamaha kwa kumchukulia mchumba. Jambo hili lilimkosesha raha Doto na kuamini endapo hatamuomba Kurwa radhi hatasamehewa. Katika mahojiano ya uwandani, Kihongosi (ktj) anasema:

> Katika jamii za Kiafrika wosia ulikuwa jambo la muhimu kabla mtu hajafa. Aliacha kumbukumbu katika jamii hiyo. Kama alikuwa na mali iligawanywa kutokana na wosia uliotolewa na kama mali yake anataka kutoa sadaka alisema ili wanaobaki waweze kufuata maagizo hayo (Utafiti, 2022)

Maelezo yaliyotolewa na Kihongosi (ktj) yanathibitisha wosia katika jamii ya Waswahili ni jambo ambalo lina maana katika jamii. Mtu kabla hajafa aligawa mali kwa ndugu na nyingine zilikwenda kutolewa sadaka msikini au kwa watu

wasiojiweza. Waliamini wanapata thawabu kwa Mungu kupitia misaada iliyotolewa. Pia, wosia uliacha kumbukumbu kwa ndugu wa marehemu kuenzi mambo mazuri yaliyofanywa na ndugu yao aliyetangulia mbele za haki. Pia, katika riwaya ya *Mirathi ya Hatari* baba yake Gusto alitoa wosia kwa Gusto wa kumwachia mirathi ya hatari. Katika wosia wake alimweleza kwamba akiitumia vizuri mirathi hiyo itamsaidia katika maisha yake. Mwandishi anathibitisha hili kwa kusema:

> Mwanangu, nakuachia kazi kubwa. Ni urithi mkubwa ukiutumia vema; bali pia ni mirathi ya hatari usipojihadhari nayo. Nakuachia dawa zote na milki yangu katika mizungu ya sihiri! (uk. 12).

Nukuu hii inaonesha jinsi Gusto alivyoachiwa wosia wa kurithi dawa zote za milki ya Mzee Kazembe kuweza kuziendeleza na kuzitumia vizuri ili ziweze kumsaidia. Gusto hakatai urithi huo kwani aliamini neno la mkata roho si la kukataa. Jambo hili linathibitishwa na mahojiano ya uwandani pale Nchimbi anaposema:

> Katika jamii mtu akiwa mgonjwa au anayetaka kufa huacha wosia kwa watu wanaoendelea kuishi. Pia, kama kuna mali ambayo angependa amwachie ndugu au mtoto alimrithisha kabla ya kufikwa na mauti. Wosia na urithi wa marehemu lengo lake ni kuenzi mambo mazuri yaliyofanywa na marehemu na kuendeleza jina lake ili asisahaulike kwa ndugu zake (Utafiti, 2022).

Maelezo haya yanaweka wazi jinsi wosia ulivyo muhimu kwa ndugu wa marehemu katika kuendeleza mambo ambayo aliyapenda marehemu. Jambo hili linathibitishwa na mawazo ya nadharia ya Sosholojia ambayo huona mambo yaliyopo katika kazi ya fasihi ni taswira ya jamii. Waandishi wa riwaya teule wamesawiri wosia uliopo katika jamii ya Kiafrika. Wosia mara nyingi ulitolewa kuachana na mambo ambayo si mazuri na kufuata mambo ambayo yanafuata misingi ya kimaadili iliyopo katika jamii. Matokeo yamebaini kuwa katika jamii ya Waswahili mtu anapokufa bila kuacha wosia au mgawanyo wa mali huleta migogoro katika jamii. Ndugu wa marehemu huingia katika chuki na mafarakano kwa kugombania mali zilizoachwa na marehemu jambo ambalo halina tija katika maisha.

4.3.7 Mavazi

Mavazi ni sehemu ya utamaduni ambayo huitambulisha jamii husika. Waswahili huvaa mavazi kwa malengo mbalimbali kama vile, kutambulisha jamii yao na kuonyesha stara na heshima. Utamaduni wa Waswahili umefungamana na mavazi.

Hii ina maana kwamba jinsi watu wa jamii fulani wanavyovaa huwakilisha utambulisho wa maisha ya jamii yao. Imebainika kuwa, Waswahili walitumia vazi la khanga lililobeba jumbe mbalimbali zilizokuwa zinatoa elimu kwa jamii na kutambulisha maisha ya Waswahili (Mbaabu, 1965 na Khamis, 2007).

Matokeo yanaonesha kuwa, Waswahili hutambulika kwa mavazi ya heshima ijapokuwa hawana vazi maalumu linalojulikana kuwa la Waswahili. Imebainika kwamba mavazi yanayoustiri mwili ndio yanayoutambulisha utamaduni wa Waswahili na kuonesha heshima kwa jamii. Waafrika wakiwamo Waswahili wanasisitiza kuvaa mavazi yenye stara kwa ajili ya kuepukana na vishawishi, kujenga maadili ya jamii na kutambulisha vyema utamaduni wa jamii. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kurwa na Doto* mwandishi anamwonesha Vumbwe kuwa alikuwa maridadi katika kuvaa mavazi ya stara kwa kijana wa kiume. Mwandishi anadhihirisha kwa kusema:

> Vumbwe alikuwa maridadi, kanyoka, mrembo, na mwenye tambo la kupendeza. Vumbwe na wenziwe saa za jioni wakisha kuvaa kanzu zao za tarabizuna zenye pande la zari badani, hutengeneza bulbul zao kichwani makubadhi miguuni na bakora mkononi (uk. 27).

Nukuu hii inaonesha utamaduni wa watu wa Unguja ambao waliathiriwa na mavazi ya Kiarabu pamoja na dini ya Kiislamu, ambapo vazi la kanzu katika jamii hiyo ni vazi linaloheshimika. Vazi hili lilitunza utamaduni wa Waswahili uliopatikana kwa watu wa Pwani ya Afrika ya Mashariki na lilionesha heshima na maadili kwa mtu aliyekuwa amelivaa. Pia, katika riwaya ya *Mirathi ya Hatari* mwandishi anasawiri mavazi ya kanzu na buibui yaliyopatikana Tanga. Mwandishi anasema:

> Kutazama kwake upande huu wangu kukanifanya nami nigeuke na kuangalia nyuma. Hatukuwa peke yetu. Nyuma yangu kulikuwa na halaiki ya waungwana waliovalia kanzu nyeupe na kofia za kitunga. Wote walikuwa katika hali ya uchungu na simanzi tele. Upande wa kushoto kulikuwa na kina mama waliojitanda buibui (uk. 62).

Dondoo hili linaonesha kuwa, wanawake na wanaume waliokuwa wamevaa kanzu na buibui, mavazi hayo yalikuwa maalumu kwa watu wanaopatikana katika mji wa Tanga kutokana na kuwepo kwa dini ya Kiislamu iliyokuwa inasisitiza mavazi ya stara na heshima katika jamii. Waswahili hawa walitunza utamaduni wao kupitia mavazi yao yaliyokuwa yamebeba hadhi na taswira ya jamii yao. Hoja hii

inashadidiwa na mawazo ya nadharia ya Sosholojia yanayoelezea upekee uliopo katika jamii. Hivyo, upekee uliopo katika mavazi ya Waswahili yanatambulisha utamaduni wa jamii yao. Katika mahojiano ya uwandani, Andrea (ktj) anasema:

> Mavazi yaliyokuwa yanasisitizwa katika jamii ya Waswahili yaliustiri mwili na kuonyesha stara ambazo zilimwepusha binti kuweka viungo vyake wazi. Wanawake mara nyingi walipenda kuvaa buibui na khanga, hizi ndizo nguo zilizobeba heshima katika jamii (Utafiti, 2022).

Kama ilivyokwisha elezwa katika mjadala hapo juu, Waswahili walifungamana na mavazi yanayostiri mwili kutokana na maadili yaliyokuwapo katika dini ya Kiislamu yaliyosisitiza zaidi stara katika mavazi. Mwanamke hakutakiwa kuonesha mwili wake ovyo kwani ilisadikika mwili wa mwanamke ni pambo la mumewe. Mwanaume pia alitakiwa kuvaa mavazi ambayo yatampa hadhi katika jamii anayotoka. Imebainika kuwa, Waswahili huvaa madera, buibui na khanga. Mavazi haya yanatumika katika shughuli mbalimbali za kijamii kama msibani, kwenye sherehe na msikitini.

4.4 Mkengeuko wa Utamaduni wa Waswahili katika Riwaya Teule

Mwingiliano ulioletwa na utandawazi katika nchi za Kiafrika umesababisha mabadiliko makubwa katika nyanja mbalimbali za kimaisha kama kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Athari za utandawazi zimevuka mipaka na kuonekana moja kwa moja katika utamaduni kutokana na mwingiliano baina ya nchi za Kimagharibi na Kiafrika. Utamaduni wa Waswahili umebadilika na kupoteza uthamani kutokana na mwigo wa tamaduni za kigeni zilizoletwa na utandawazi katika nchi za Kiafrika (Mbele, 2020). Sehemu hii imejadili swali la lengo la pili linalouliza mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unajitokezaje katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* na *Almasi za Bandia* zama za utandawazi?. Vipengele vilivyobainishwa ni lugha, ndoa, kifo, maadili, imani za kidini na mavazi. Ufuatao ni ufafanuzi wa vipengele hivyo:

4.4.1 Lugha

Lugha ni miongoni mwa vipengele vya utamaduni ambacho kimepokea mabadiliko katika kazi za fasihi. Mwandishi huathiriwa na kile kinachotokea katika jamii kwa kuchota fikra, maudhui, falsafa, mtindo, maumbo kutoka katika jamii hasa

inapokuwa kwenye kasi ya mabadiliko. Mabadiliko yanayotokea katika lugha huathiri utamaduni wa jamii kwa namna mbalimbali kama vile, kumtenga mwanajamii na utamaduni wake, kuleta mwingiliano wa kiutamaduni na kupoteza utambulisho wa jamii kupitia lugha. Mabadiliko hayo yamesambaa mpaka katika baadhi ya kazi za kifasihi ambazo hutumia lugha za kigeni zinazosawiri mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili (Shartry, 1996 na Kevogo, 2018).

Utafiti umebaini kuwapo kwa matumizi ya lugha ya Kiingereza katika riwaya teule. Imebainika kuwa, waandishi wa riwaya teule wametumia lugha ya Kiingereza katika riwaya zao ambazo msingi wa uandishi wake ni lugha ya Kiswahili. Kwa kufanya hivyo waandishi wanaitenga hadhira lengwa na utamaduni wa jamii yao jambo ambalo linasawiri mkengeuko wa utamaduni wa jamii husika. Hali hii inaathiri lugha zilizopo katika jamii kwa kutawaliwa na lugha za kigeni ambazo zililetwa na wakoloni. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wan*gu mwandishi anathibitisha matumizi ya lugha ya Kiingereza kupitia mazungumzo kati ya Kabula na Derrick. Anaelezea kuwa:

> *Hey Don't you have another topic to discuss ? The only thing you can talk is about my breast? Leave my breasts alone, I have told you that my body has grown fat, that's all, there is no any other answer (uk. 32).*

Dondoo hili ni ushahidi tosha kuwa lugha ya Kiingereza imetumika katika riwaya teule za Kiswahili ambazo msingi wa uandishi ni lugha ya Kiswahili. Mwandishi amemtumia Kabula aliyekuwa anazungumza na Derrick kuhusiana na mabadiliko ya mwili wake kwa kutumia lugha ya Kiingereza, kuonesha ufahari wa kuzungumza lugha ya kigeni. Jambo hili linasababisha lugha ya Kiswahili kushuka thamani kutokana na wazungumzaji kuona ufahari wa kutumia lugha ya Kiingereza ambayo hutambulisha utamaduni wa kigeni. Pia, mwandishi wa riwaya anaendelea kuonesha mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza unavyotumiwa katika riwaya teule ya Kiswahili jambo linaloendelea kuthibitisha mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule. Mwandishi anasema:

> Mwezi mmoja tu baada ya wakuu wapya wa majeshi kuteuliwa upelelezi wao uliibuka na taarifa mpya kutoka katika visiwa vya *Peace of Mind* vilivyokaliwa na magaidi wa *Sokomoni Peoples Movements for Democracy* (uk. 122).

Dondoo hili linaonesha jinsi lugha ya Kiswahili na Kiingereza ilivyochanganywa katika riwaya teule. Kikundi cha waasi wa serikali ya Rais Gabriel walikuwa wakifanya upelelezi katika kisiwa cha *Peace of Mind* ambapo mwandishi ametumia lugha ya Kiingereza katika kutaja kisiwa hicho. Pia, ametumia maneno ya Kiingereza kama *Sokomoni Peoples Movements for Democracy* kutaja kikundi cha magaidi waliokuwa wanaishi Sokomoni. Imebainika kuwa, waandishi wanapotumia lugha za kigeni katika uandishi wao, utamaduni wa Waswahili unakengeuka kwa kufungamana na lugha za kigeni ambazo ni wakala wa kueneza tamaduni za kigeni. Jambo hili linaleta athari kwa jamii kwa kuona ufahari wa kuendelea kutumia lugha za kigeni na kuacha lugha ya Kiswahili ambayo inawaunganisha katika utamaduni wa jamii yao. Pia, katika riwaya ya *Almasi za Bandia* mwandishi anathibitisha kwa kumtumia Yakini ambaye alikwenda kumtembelea Zambe kuwa alitumia mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Mwandishi anathibitisha kwa kusema:

> "Vipi leo mmekuja kunipeleka *out* na mama watoto wangu?" Zambe aliendelea na mizaha yake. "Wacha bwana! Kuna *out* gani miaka ya leo? Labda kama umekusudia watoto walale na njaa," Yakini alijibu huku akicheka (uk. 57).

Dondoo hili linaonesha kuwa waandishi wa riwaya teule wanaonesha athari ya utandawazi katika jamii ya Waswahili kupitia kusawiri lugha za kigeni kama vile, lugha ya Kiingereza ambayo inatambulisha watu kutoka nje ya nchi. Waandishi hao wanaacha kuthamini lugha ya Kiswahili ambayo inaunganisha watu katika utamaduni wa Waswahili. Jambo hili linapelekea lugha ya Kiswahili kushuka thamani kwa kuonekana haina misamiati ya kutosha kutokana na watu wengi kuona ufahari wa kutumia lugha ya kigeni kuliko Kiswahili. Nadharia ya Ubaada Ukoloni kupitia msingi unaosema matumizi ya lugha ya Kiingereza katika nchi zilizotawaliwa ni kuendeleza ukoloni mamboleo, imedhihirisha hali hiyo katika riwaya teule kwa kuwa zimetumia lugha ya Kiingereza. Katika mahojiano ya uwandani, Abasi (ktj) anathibitisha jambo hili kwa kusema:

> Waandishi wa riwaya katika kipindi cha utandawazi kiukweli hali inasikitisha. Ukiingia katika duka la vitabu unakuta kitabu cha riwaya ya Kiswahili lakini unakuta jina limeandikwa kwa Kiingereza na ukiangalia ndani ya riwaya unakuta waandishi hao wametumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Ukiangalia kazi za waandishi walio

> wengi hawatoi na hawaoni umuhimu wa kuendeleza utamaduni wa Waswahili kupitia lugha zao zinazowatambulisha kipindi cha utandawazi kitu ambacho ni amali ya thamani katika kutambulisha utamaduni wa Waswahili kwa watu wa jamii nyingine (Utafiti, 2022).

Maelezo ya Abasi (ktj) yanaonesha jinsi waandishi wa kipindi cha utandawazi wanavyotumia lugha ya Kiingereza katika kazi zao. Jambo hili linapelekea utamaduni wa asilia kupitia lugha kuendelea kupoteza thamani na kuendelea kutukuza lugha za kigeni kupitia riwaya ya Kiswahili ambayo msingi wa uandishi ni Kiswahili. Kwa mfano, riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* katika jalada la kitabu mwandishi ameandika kwa maandishi makubwa *The President Loves My Wife*. Jambo hili ni uthibitisho kuwa lugha ya Kiingereza imetumika katika baadhi ya riwaya za Kiswahili zilizoandikwa kipindi cha utandawazi. Mahojiano ya Abasi (ktj) yanashadidiwa na Khamis (ktj) kwa kusema:

> Lugha ni kipengele ambacho kimepokea mabadiliko kwa kiasi kikubwa katika uandishi wa riwaya katika kipindi cha utandawazi. Waandishi wanaona ufahari kuingiza baadhi ya lugha za kigeni katika kazi zao jambo linalofifisha lugha ya Kiswahili na kudunisha lugha hiyo. Unakuta mwandishi anatumia lugha ya Kiingereza katika riwaya ya Kiswahili ambayo msingi wake mkubwa ni lugha ya Kiswahili (Utafiti, 2022).

Katika jamii waandishi wanaendelea kutumia lugha za Kiingereza katika uandishi wa riwaya jambo linaloathiri lugha inayotambulisha utamaduni wa jamii husika. Lugha ya Kiswahili inadunishwa na kufifishwa kutokana na kuchanganywa na lugha kutoka katika nchi za Kimagharibi, jambo linalopelekea lugha ya Kiingereza kuonekana bora kuliko lugha ya Kiswahili inayowaunganisha Waswahili. Naye, Faustine[16] anathibitisha dai hili kwa kusema:

> Utandawazi umeifanya dunia kuwa kijiji. Kwa asilimia kubwa lugha ya Kiingereza imekuwa lugha ya sokoni ambayo inatawala mawasiliano. Waandishi wengi wanadhani kuandika riwaya zao kwa kuchanganya lugha au kutumia lugha ya Kiingereza ndio usomi lakini waandishi wanasahau wanamwandikia nani? Pia utamaduni wa Waswahili umeunganishwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Kuiga matumizi ya lugha za kigeni katika riwaya ya Kiswahili kunasawiri mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili. Utandawazi umepelekea

[16] Dkt. Stella Faustine ni mhadhiri katika idara ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 29/6/2022 ofisini kwake.

> watu waone ili msomi atambulike lazima atumie lugha ya Kiingereza jambo linalopelekea kuacha lugha ya Kiswahili inayotambulisha jamii yao (Utafiti, 2022).

Dondoo hili linaonesha kuwa, baadhi ya waandishi wa riwaya ya Kiswahili katika kipindi cha utandawazi wanasahau wanaandika riwaya ya Kiswahili kwa ajili ya nani. Matumizi ya lugha ya Kiingereza katika riwaya ya Kiswahili kwa ajili ya kuonesha ufahari, kunasawiri mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili. Waandishi wanaacha lugha zinazounganisha utamaduni wa jamii husika wanaiga lugha ya Kiingereza ambayo haina mfungamano na utamaduni wa Waswahili. Imebainika kuwa, katika jamii ya Waswahili wanajamii wengi hupenda kutumia lugha ya Kiingereza kuonesha ustaarabu na kuelimika kwao, jambo linalopelekea kuacha lugha zao ambazo ni msingi wa utamaduni wao na kufungamana na lugha za kigeni ambazo zimebeba tamaduni wa kigeni. Hivyo, wanajamii wanapoteza lugha ya Kiswahili ambayo inafungamana na utamaduni wao kwa kuiga lugha ya Kiingereza ambayo inatambulisha itikadi za kigeni kwa Waswahili. Galtung (1980) anasema kutokana na lugha ya Kiingereza kupenya katika nyanja mbalimbali za maisha kumefanya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili kuamini kuwa kutumia lugha ya Kiingereza ni ishara ya maendeleo. Jambo hili linaathiri jamii kwani kupoteza lugha ni kupoteza utamaduni na kupoteza utamaduni ni kupoteza maarifa muhimu katika jamii.

Sambamba na hilo, utafiti umebaini kuwapo kwa matumizi ya lugha isiyo na kificho katika riwaya teule. Imebainika kuwa, waandishi wa riwaya teule wametumia lugha isiyo na kificho katika uandishi wa masuala mbalimbali yanayotokea katika jamii. Lugha hizi zina athari katika jamii kwani zinapelekea mmomonyoko wa maadili yaliyopo katika jamii. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* mwandishi anadhihirisha hilo kwa kumtumia Rais Gabriel aliyembaka Kabula. Anathibitisha kwa kusema:

> Kabula alipotokeza tu bafuni, Rais alinyanyua mkono wake na kumpulizia dawa hiyo usoni. Aliporomoka hadi chini kama mzigo bila hata kupiga kelele! Bila kuchelewa Rais Gabriel alianza kufungua suruali yake na kuishusha hadi miguuni, kisha akapiga magoti chini akikamata gauni la Kabula na kulipandisha juu kuelekea kiunoni! (uk. 22).

Nukuu hii inaonesha namna lugha isiyo kuwa na kificho ilivyotumika katika kuelezea tukio la ubakaji lililofanywa na Rais Gabriel kwa Kabula. Katika utamaduni wa Waswahili, kuelezea masuala ya mapenzi pasipo kutumia lugha ya kificho kunakiuka misingi ya utamaduni wao. Mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unajidhihirisha kwa kwenda kinyume na misingi ya kimaadili ambayo inaongoza jamii. Vilevile, katika riwaya ya *Almasi za Bandia* mwandishi ametumia lugha isiyo na kificho katika baadhi ya sehemu katika uandishi wake. Hii inadhihirisha pale mwandishi anaposema:

> … Patricia alipigapiga miguu yake alipoona Merton anakusudia kuishika na kuitanua, naye Merton sasa alikuwa akisikia damu kuchemka kwa ashiki. Iliyozidi kumpanda kadri huyu msichana alivyozidi kujihami na kukataa kujisalimisha. Sasa Merton alikuwa amefaulu; alipopata nafasi ya kusogeza mkono wake kiunoni kwa Patricia, aliivuta chupi ya yule msichana na kuichania mbali bila ya huruma wala kujali. Alikuwa anahema kama faru na kutoka udende kwa uchu. Na sasa mwili wake wote ulikuwa juu ya mwili wa Patricia (uk. 95).

Dondoo hili linathibitisha kuwa lugha isiyo na kificho imetumika kuelezea kitendo cha ubakaji kilichofanywa na Merton kwa Patricia. Mwandishi anapoweka wazi kuwa mwili wa Merton ulikuwa juu ya mwili wa Patricia, jambo hili linajenga taswira na tukio la moja kwa moja lililofanywa na Merton. Pia, mwandishi anaeleza kwa uwazi kuwa "Merton aliivuta chupi ya yule msichana na kuichana" hivyo, lugha isiyo na kificho imetumika na kwenda kinyume na misingi inayojenga maadili katika jamii ya Waswahili. Mwandishi anaendelea kuthibitisha matumizi ya lugha isiyo na kificho katika riwaya ya *Almasi za Bandia* kwa kusema:

> …Mmeona pale wanavyosema, ati wanaweza kufanya hata vitu vingine vya ajabu kama vile kuutia mdomoni uume wako! (uk. 53).

Katika dondoo hili mwandishi ametumia lugha isiyo na kificho ambapo ametumia neno "kuutia uume mdomoni" bila kutumia tasifida, jambo ambalo linadhihirisha mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili. Waandishi wa riwaya teule wametumia lugha isiyo na kificho kwa kuiga misingi ya uwazi iliyopo katika tamaduni za kigeni. Mambo haya yanapelekea maadili katika jamii kuendelea kumomonyoka siku hadi siku katika zama za utandawazi. Jambo hili linathibitishwa na nadharia ya Ubaada Ukoloni msingi wa mwingiliano wa kitamaduni unaoelezea kuwa utamaduni wa

Waswahili umepokea athari kutoka katika tamaduni za kigeni. Hivyo, kupitia lugha isiyo na kificho iliyotumiwa na waandishi katika baadhi ya sehemu za riwaya teule, kunaonesha mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule. Hii inatokana na kutumia lugha ambazo hazisisitizi maadili kwa jamii husika. Vilevile, mwandishi wa riwaya ya *Almasi za Bandia* anaelezea kuwa:

> Akikimbia shoti, akisukumwa kwa nguvu za ajabu huku akimvuta yule msichana nyuma yake. Walipotelea katika vichochoro vya majumba na kushituka wamesimama nyuma ya choo cha "kuta" za magunia kinachonuka harufu mbaya, huku wakihema pua zao zikipanuka na kujifinya kufuatilia pumzi zao. Nguo zao zilikuwa zimelowa jasho kama vile walikuwa wametoka majini na sketi ya yule msichana ilikuwa imejipachika katikati ya matako yake makubwa kama vile imegundishwa (uk.20).

Nukuu hii inaonesha mwandishi alivyotumia lugha ya wazi anaposema "sketi ya yule msichana ilikuwa imejipachika katikati ya matako". Katika utamaduni wa Waswahili maneno kama hayo yanapaswa kutumia lugha ya mficho ili kulinda heshima ya jamii husika. Mwandishi anapotumia maneno kwa uwazi misingi iliyopo katika maadili ya jamii inakiukwa. Katika mahojiano ya uwandani, Khamis (ktj) anasema:

> Lugha ya Kiswahili imejaa tasifida. Ukiangalia riwaya za watangulizi wa kazi za fasihi walitumia lugha ya mficho katika masuala ya mapenzi. Lugha ambayo ilikuwa vigumu kupata jambo lililokuwa linafanyika, lakini riwaya za sasa zimetumia lugha ya wazi. Kama tusi linaonekana, na masuala ya kimapenzi yanadhihirishwa wazi na kwa kutumia lugha ambayo inajenga taswira ya jambo linalotaka kufanyika. Jambo hili linakwenda kinyume na utamaduni wa Waswahili. Utandawazi umeleta uwazi katika kila sehemu na kupelekea vijana kuendelea kujifunza vitu ambavyo kimsingi sio umri wao. Hali hii inaendelea kusawiri mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili uliopo katika maisha (Utafiti, 2022).

Maelezo hayo ya Khamis (ktj) yanashadidia hoja zilizokwisha jadiliwa hapo juu. Anaonesha kuwa uandishi wa riwaya za kipindi cha utandawazi na riwaya za awali zinatofautiana katika matumizi ya lugha. Waandishi wa riwaya teule wametumia lugha isiyo ya kificho katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Wanajamii wanajifunza na kuiga matendo yasiyofaa kupitia kazi za riwaya, jambo linaloendelea kudhihirisha

mkengeuko wa utamaduni kwa kutothamini lugha inayotunza staha ya maisha katika jamii ya Waswahili. Naye, Jumanne[17] anaunga mkono dai hili kwa kusema:

> Kuna utofauti mkubwa wa matumizi ya lugha kati ya waandishi wakongwe na wasasa. Waandishi wakongwe waliandika kazi zao kwa kutumia ufundi wa lugha uliokuwa na mafumbo ndani yake yaliyopunguza ukali wa maneno katika masuala ya chumbani lakini riwaya za sasa zimeweka masuala yote wazi bila kutumia lugha ya faragha kusawiri jamii, kitu kinachokwenda kinyume na utamaduni wa jamii (Utafiti, 2022).

Maelezo ya Jumanne (ktj) yanaonesha kuwa riwaya za zamani zilitumia lugha za mficho na kupunguza ukali wa maneno kupitia tasifida. Baadhi ya riwaya zinazoandikwa katika kipindi cha sasa zinatumia maneno kwa upwekepweke. Masuala ya chumbani yamewekwa wazi. Mambo haya yanakengeusha utamaduni wa Waswahili kutokana na jumbe za wazi tunazozipata katika riwaya hizi. Achebe (1964) anashadidia kuwa utamaduni wa Waswahili unapotea kwa jina la utandawazi ambapo waandishi wanakengeuka kwa kufuata misingi ambayo haipo katika utamaduni asilia na kuendeshwa na masuala ya Kimagharibi yaliyozagaa katika jamii. Kwa ujumla, kutokana na mjadala uliokwisha jadiliwa hapo juu lugha katika jamii ya Waswahili imebadilika kutokana na ujio wa utandawazi. Jambo hili linapelekea kuwapo kwa tofauti kati ya lugha iliyotumika kuandika riwaya ya Kiswahili kipindi cha awali na cha sasa. Riwaya za awali zilitumia lugha iliyotunza staha na heshima katika jamii lakini baadhi ya riwaya za sasa zinatumia lugha ambayo inapoteza utambulisho wa maadili yaliyokuwapo kwa jamii, jambo linalodhihirisha mkengeuko uliopo katika utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule.

4.4.2 Ndoa

Utandawazi umekuja na mambo mapya katika asasi ya ndoa ambayo yana athari katika utamaduni wa jamii. Mambo hayo ni kama vile, ndoa za mikataba, ndoa za jinsia moja na ukosefu wa uaminifu katika ndoa. Wanajamii wanaacha misingi ya kitamaduni inayowaongoza katika masuala ya ndoa na kuthamini mwigo kutoka nchi za Kimagharibi. Jambo hili linaathiri maadili yanayofungamana na masuala ya utamaduni katika jamii. Masuala ya ndoa yamechukuliwa kama jambo la kawaida

[17] Bi. Arafa Jumanne ni mhadhiri msaidizi katika idara ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 31/6/2022 ofisini kwake.

kutokana na tamaduni za Kimagharibi zilizoenea katika jamii za Kiafrika. Mabadiliko haya yameleta athari katika jamii ya Waswahili kama kuibuka kwa migogoro katika ndoa, usaliti na kuvunjika kwa ndoa (Munyoki, 2015). Utamaduni wa Waswahili unakengeuka kutokana na kuachana na masuala ya ndoa yaliyobeba tija katika jamii.

Matokeo yanaonesha kuwa, riwaya hizi hazionyeshi uthamani wa maisha ya ndoa. Waandishi wa riwaya teule wanaonesha jinsi wanaume wanavyoweza kuishi na wanawake bila kuoa na kupata huduma zote kama mke na mume. Pia, waandishi hawa wamesawiri ndoa za jinsia moja kama jambo la kawaida. Mambo haya hayafungamani na misingi iliyopo katika utamaduni wa Waswahili. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* mwandishi anamtumia Kabula na Rais Gabriel kuonesha walivyokuwa wanaishi kama wanandoa wakati bado hawajaoana. Mwandishi anaeleza kuwa:

> Maisha ya Kabula na Rais Gabriel yalikuwa ni picha halisi ya mke na mume. Hakuwa na tofauti na watu waliokwisha kufunga ndoa katika maisha yao. Walilala pamoja, walikula pamoja na waliogelea pamoja katika bwawa lililokuwa ikulu (uk. 120-121).

Nukuu hii inaonesha jinsi Kabula na Rais Gabriel walivyokuwa hawajafunga ndoa ijapokuwa waliishi kama wanandoa. Jambo hili linaonesha misingi iliyokuwapo katika utamaduni imeachwa, kama msingi wa nadharia ya Ubaada Ukoloni unavyoeleza kuwa mwingiliano wa utamaduni umeleta mseto katika masuala mbalimbali likiwemo suala la ndoa tofauti na yaliyokuwapo katika jamii za Afrika. Ndoa lilikuwa ni jambo linaloruhusu mwanamke na mwanaume kuishi pamoja baada ya kufuata taratibu zilizopo katika jamii kama mume na mke. Jamii inazidi kufuata utamaduni wa kigeni na kuharibu tamaduni zilizosisitizwa katika maisha ya jamii yao. Vilevile, katika riwaya ya *Almasi za Bandia* mwandishi anamtumia Merton kuonesha alivyokosa uaminifu katika ndoa hali iliyosababisha Gloria kugundua usaliti aliokuwa nao mume wake wa kushiriki tendo la ndoa na wanawake wengine. Jambo hili lilimuudhi Gloria na hasa pale alipowafumania hotelini. Mwandishi anasema:

> “Ah kila wakati kuongea mambo yenu tu!” Msichana alilalamika, “Kwanza wewe Athumani nenda chumbani kwako ukamsubiri huyo msichana wako huko huko. Kama hutaki, basi sisi tutaanza mambo yetu mbele yako!”. Gloria alihisi kutokwa na nguvu miguuni. Moyoni akajisikia wepesi wa tiara na ubaridi mgeni ulichanganyika na hasira. Wazo la kwanza lililomjia akilini, ni ukosefu wa uaminifu kwa Merton (uk.129).

Nukuu hii inaonesha jinsi ambavyo ndoa katika kipindi cha utandawazi zilivyopoteza thamani kwa kuendekeza masuala ya ngono nje ya ndoa na usaliti kuonekana kama jambo la kawaida. Wasichana wanatumika kwa ajili ya starehe, mambo ambayo hayakufungamana na misingi ya maadili katika jamii ya Waswahili. Mwandishi anamtumia Merton ambaye alikuwa ameoa huku akiwalaghai wasichana kwa lengo la kutimiza tamaa zake za kimwili. Katika mahojiano ya uwandani, Kihongosi (ktj) anasema:

> Baadhi ya riwaya za sasa hazifunzi maadili ya ndoa ambayo yalitakikana kwa wanandoa badala yake riwaya hizi hutumika kama chombo cha kufundisha haki sawa kwa wanandoa. Jambo hili linapelekea ndoa kuingia katika migogoro na kupotea kwa thamani ya maisha ya ndoa yaliyosawiriwa na wazee wa zamani. Mambo haya yamechagizwa na mwingiliano wa utamaduni kati ya Afrika na Ulaya na kupelekea kuacha misingi ya kitamaduni iliyokuwa inatuongoza katika ndoa (Utafiti, 2022).

Nukuu hii inaonesha kuwa baadhi ya riwaya za sasa zinasisitiza zaidi masuala ya haki sawa kwa wanaume na wanawake jambo linalopelekea ndoa nyingi kuingia katika migogoro. Thamani ya maisha ya ndoa haionekani, bali wanachukua mambo kutoka katika jamii za Kimagharibi na kuacha misingi ya jamii yao. Mambo haya yanakengeusha utamaduni wa jamii ya Waswahili kutokana na kuingia kwa mabadiliko katika jamii. Kwa ujumla, Umagharibi umeingia katika ndoa za Waswahili jambo linalopelekea jamii kutaka kuishi maisha kama ya wazungu na kusahau misingi ambayo jamii ilikuwa imejiwekea katika masuala ya ndoa. Ndoa ziko katika hatari ya kuvunjika kutokana na kukengeuka miongozo ya jamii. Munyoki (2015) anashadidia mjadala wa hapo juu kwa kuonesha jinsi familia za Kiafrika zilivyo katika njia panda ya migongano ambayo inasababishwa na mabadiliko yaliyopo katika jamii. Familia hizi zinaiga utamaduni wa Kimagharibi kwa kuona ndio ustaarabu na kuachana na utamaduni wa Waswahili ambao huonekana kuutumia ni kutostaarabika.

Aidha, utafiti umebaini kuwa wazazi siyo watu wa msingi katika kuchagua wachumba. Matokeo yanaonesha kuwa utamaduni wa Waswahili unakengeuka kwa kutoonesha umuhimu wa wazazi katika kutoa miongozo kwa watoto wao kuhusu mtu wa kuoa au kuolewa naye katika kipindi cha utandawazi. Jambo hili linaathiri jamii kwani ndoa na familia nyingi ziko katika migogoro, usaliti na vijana kujilea pasipo kujua maadili ya jamii zao. Kwa mfano, katika riwaya *ya Rais Anampenda Mke Wangu* mwandishi anamtumia Kabula kwa kuonesha pale alipopendana na Rais Gabriel, alikwenda kutoa taarifa kwa wazazi ya kutaka kuolewa. Wazazi hawakuridhia, lakini Kabula alisema hakuna anayeweza kumchagulia mume wa kuishi naye. Mwandishi anathibisha hili kwa kusema:

> Wiki moja kabla ya harusi, Kabula alisafiri hadi kijijini kwao kuwataarifu wazazi wake juu ya harusi yake. Alishangazwa na mapokezi duni aliyoyapokea kutoka kwa wazazi wake! Mama na baba yake hawakuitikia salamu yake na alipoeleza juu ya harusi ya jioni ya siku hiyo jibu alilopewa lilimsikitisha. "Huwezi kuolewa mara mbili mwanangu kama mmefanya njama kumuua mtoto wa watu Derrick ili muoane na Rais wako, basi mmekwama. Hakuna mtu atakayehudhuria harusi yako haramu hakuna baraka zetu!" baba yake Kabula alisema kwa ukali. Nitaolewa tu mtake msitake. Si mimi wa kuchagua Kabula alisema. Kabula alitoka nje ambako aliingia ndani ya gari na kumwamuru dereva wake aendeshe gari kurudi tena jijini Shuntown (uk. 91-92).

Nukuu hii inaonesha jinsi ambavyo Kabula hakutaka kuwapa wazazi kipaumbele katika ndoa yake na alifanya maamuzi ya kuolewa na Rais Gabriel bila kuangalia wazazi wake wanasema nini kuhusiana na ndoa hiyo. Hili linathibitishwa na Kabula anaposema "Nitaolewa mtake msitake. Si mimi wa kuchagua". Jambo hili linathibitisha jinsi usasa ulivyoenea katika masuala ya ndoa kwa kuonesha wazazi hawapewi kipaumbele cha kutoa miongozo, ila watoto ndio wenye wajibu mkubwa wa kuchagua wenzi wa maisha yao. Pia, katika riwaya ya *Almasi za Bandia* mwandishi anathibitisha hilo kwa kuonesha jinsi Merton alivyompenda Gloria na kuahidi kumuoa. Hata hivyo, baada ya muda mfupi Merton alikwenda nyumbani kwao Gloria na kutoa posa kwa ajili ya kumwoa. Mwandishi anasema:

> Hizo wiki mbili ndizo ziliamua maisha yao ya baadaye. Merton alimweleza wazi Gloria kwamba yuko tayari kumwoa, hakujali kama ana mtoto kwani la muhimu ni kuficha tu hiyo siri kwa wazazi wake na kumwacha mtoto kwa mama yake Gloria (uk. 125).

Katika nukuu hii inaoneshwa kuwa katika ndoa za sasa kijana anapomridhia binti, utaratibu hufanyika bila kutaka ushauri au ridhaa ya wazazi au jamaa wa karibu. Jambo hili linakengeuka kutoka kwenye utamaduni wa Waswahili, ambapo mzazi alitakiwa kuwa msaada wakati kijana anapotaka kuoa. Mwandishi anamtumia Merton aliyempenda Gloria na akahidi kumuoa kwa masharti kuwa Gloria amuache mtoto kwa mama yake. Katika mahojiano ya uwandani, Nchimbi (ktj) anasema:

> Ndoa za zamani zilikuwa zinadumu kwani wazazi waliangalia familia ambazo hazina tatizo ndio waliwaozesha mabinti zao. Wazazi walikuwa msingi wa kuwaongoza watoto katika ndoa bora. Utandawazi umeathiri tamaduni zilizokuwapo katika jamii kwani kutumia misingi ya ndoa za kitamaduni kunaonekana ni kupitwa na wakati. Wazazi walikuwa na uwezo wa kubariki ndoa na kuwatakia maisha mazuri huko waendako. Jambo hili kwa sasa halipewi kipaumbele kutokana na mwingiliano wa kitamaduni ulioletwa na utandawazi. Utamaduni wa Waswahili unakengeuka kwa kuacha miongozo mizuri kutoka kwa wazazi katika masuala ya ndoa (Utafiti, 2022).

Maelezo haya yanazidi kuthibitisha kuwa ndoa za sasa zina utofauti na ndoa za zamani. Ndoa za sasa haziwapi nafasi wazazi ya kufanya uchunguzi kwenye familia ambayo kijana au binti anakwenda kuolewa. Usasa umeingia katika ndoa na kuona wazazi hawana umuhimu sana katika ndoa na kuendelea kufanya hivyo ni kuendeleza ushamba. Jambo hili linashadidiwa na nadharia ya Ubaada Ukoloni msingi wa utabaka unaosisitiza kuacha kutumia miongozo ya wazazi katika masuala ya ndoa na kuiga masuala ya Kimagharibi yanayoonekana kuwa bora katika jamii. Katika ulimwengu wa sasa watoto wamechukua majukumu na kuwajibika katika kutafuta mtu wa kumwoa. Suala hili si baya hata hivyo, wazazi wanatakiwa kupewa nafasi ya kuwashauri watoto pale wanapoona kijana au binti anakwenda kuolewa na mtu ambaye wazazi hawajaridhia. Alloys (2003) anathibitisha mjadala wa hapo juu kwa kusema:

> *Due to culture change, men find their wives on their own without the consent of their parents. They are not willing to know or investigate things about who to marry; they can make decisions on where and when the marriage will hold. Which has often times resulted to regrets, abandonment and even Quarrel between the two parties* (pg. 46).
>
> Kutokana na mabadiliko ya utamaduni, vijana wa kiume wanatafuta mabinti wa kuwaoa wao wenyewe bila kuzingatia ushauri kutoka kwa

> wazazi. Hawako tayari kujifunza mambo gani ya kuzingatia mtu anapotaka kuoa, wao hufanya maamuzi ya lini na wapi ndoa ifanyike. Jambo linalopelekea majuto, utengano na migogoro baina ya pande mbili (Tafsiri ya Mtafiti).

Katika nukuu hii, Alloys anaonesha kuwa, katika jamii za Waswahili masuala ya ndoa yamebadilika tofauti na ndoa za awali. Kijana anapotaka kuoa hayuko tayari kufanya uchunguzi kwa mtu anayetarajia kufunga naye ndoa. Kitu kikubwa wanachojali ni lini na wapi ndoa itafanyika. Mambo haya yanasababisha majuto, utengano na migogoro katika ndoa. Murithi, Wafula na King'ei (2018) wanaendelea kushadidia kuwa katika zama hizi za utandawazi wazazi hawahusishwi sana katika masuala ya ndoa. Vijana wakipendana wanaanza maisha ya ndoa na wakihitaji ushauri wanapata uamuzi kutoka kortini tofauti na ndoa za jadi zilizokuwa zinawategemea wazazi kuwa washauri wakuu katika ndoa za watoto wao.

4.4.3 Kifo

Katika kipindi hiki cha utandawazi kutokana na kuingia kwa ustaarabu wa kigeni suala la kifo limebeba taswira tofauti na ile ya mwanzo katika jamii za Kiafrika. Utafiti umebaini kuwa mauaji ni jambo la kawaida katika riwaya teule za zama za utandawazi. Waandishi wa riwaya teule wamesawiri mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili ambapo wanaonesha mauaji kama sehemu ya sherehe na shangwe kinyume na utamaduni wa Waswahili uliochukulia mauaji kama sehemu ya simanzi inayowahusu watu wote katika jamii. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* mwandishi anamtumia Kabula, Roggers, Regan na Ghadaffi kuonesha namna walivyopanga mipango ya kumuua Derrick hadi kufanikiwa. Mwandishi anathibitisha kwa kusema:

> Njiani Kabula, Roggers, Regan, Ghadaffi walishangilia ushindi walioupata kwa kumuua Derrick Kisayansi. Hakuna aliyetegemea kazi ile ingekuwa rahisi kiasi kile. Kwa Kabula alishangilia kwa sababu sasa harusi kati yake na Rais Gabriel ingefungwa na yeye angehamia ikulu na kuwa mke wa Rais. Wakati Kabula alishangilia kuingia ikulu, Ghadaffi na wenzake walishangilia kupata mamilioni ya pesa zao zilizobaki. Kila mmoja wao alijiona tayari tajiri (uk. 84).

Katika nukuu hii mwandishi anamuonesha Kabula aliyepanga njama ya kumuua Derrick ambaye alikuwa mume wake, anavyofurahia kutekeleza kitendo hicho jambo ambalo linakwenda kinyume na utamaduni wa Waswahili kwa kuwa utamaduni huo

unasisitiza utu wa mtu ni bora kuliko kitu. Kabula anapanga njama na Rogger, Ghadaffi na Regani ya kutoa uhai wa maisha ya Derrick jambo ambalo si la kiutu katika jamii. Rogger, Gadaffi na Regani wanathamini pesa kuliko uhai wa Derrick. Mambo haya yanakiuka msingi wa utu wa mtu katika jamii ya Waswahili. Pia, mwandishi anaendelea kuthibitisha jambo hili pale ambapo Kabula, Rogger, Ghadaffi na Regani wanafanya sherehe kubwa kwa ajili ya kifo cha Derrick. Mwandishi anaelezea kuwa:

> Walipofika nyumbani sherehe kubwa ndani iliendelea kufurahia kifo cha Derrick! Hakuna aliyeumia kuwa binadamu mwenzao alikuwa amekufa. Kifo cha Derrick kilikuwa ushindi mkubwa kwao (uk.84).

Nukuu hii inaendelea kuonesha kitendo cha Derrick kufa kilikuwa ni shangwe na furaha kwa Kabula na wenzake kwa kuwa waliamini kila jambo walilolitaka lingetimia. Kifo cha Derrick kilisindikizwa na sherehe kubwa iliyofanywa na Kabula, Rogger, Ghadaffi na Regani bila kuwa na huruma ya kutoa uhai wa binadamu mwenzao. Nadharia ya Ubaada Ukoloni inaeleza kuwa nchi za Kiafrika zimeiga mambo kutoka katika nchi za Kimagharibi, jambo linalopelekea kusawiri masuala ya kifo kama sehemu ya sherehe na kujipongeza, wakati katika jamii ya Waswahili kifo lilikuwa tukio la kuhuzunisha. Katika mahojiano ya uwandani, Zabron (ktj) anasema:

> Katika jamii ya Waswahili suala la mauaji kwa kutumia silaha au kawaida ni jambo la kushangaza. Kitendo cha binadamu kutoa uhai wa binadamu mwingine ni kukosa utu na misingi ya jamii inakuwa imevunjwa. Katika riwaya za kitandawazi waandishi wanaweka mauaji kama jambo la kawaida katika jamii. Waandishi hawa wamepata mwigo na athari kutoka katika maisha ya Kimagharibi ambapo mauaji kwao ni jambo la kawaida ambalo halishangazi. Waandishi wameacha misingi ya kuonesha umuhimu wa utu. Wanakengeuka utamaduni wa jamii yao (Utafiti, 2022).

Maelezo haya yanathibitisha kuwa waandishi wa riwaya za sasa wanaandika riwaya zao kwa kupata mwigo wa Kimagharibi. Riwaya hizo hazisisitizi mauaji kama jambo la kushangaza bali huonesha kama jambo la kawaida lisiloleta simanzi kwa jamii. Suala hili linadhihirisha mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili. Imebainika kuwa, waandishi wa riwaya katika zama hizi wanaandika kazi zao kwa kuiga mambo yanayofanyika katika jamii za Kimagharibi, yanayokwenda kinyume na utamaduni wa Waswahili hasa katika suala la mauaji.

Aidha, matokeo yanaonesha kuwa, katika kipindi cha utandawazi wanajamii wanaamini hakuna maisha mtu anapokufa. Imebainika kuwa, waandishi katika kipindi cha utandawazi wamesawiri suala la kifo kuwa mtu akifa harudi tena, anakuwa amekufa jumla. Suala hili ni kinyume na utamaduni wa Waswahili ambao wanaamini juu ya uduara katika maisha. Kwamba mtu anapokufa huwa anabadilika kutoka ngazi moja kwenda nyingine. Hivyo, huamini kuwa mtu akifa hubadilika kuwa mzimu na huweza kurudi kwa njia mbalimbali kuweza kuwasiliana na watu walioko hai. Hivyo, masuala yaliyokuwapo katika utamaduni wa Waswahili, kuyaendeleza ni ushamba kama vile, kuamini maisha baada ya kifo. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* mwandishi anamtumia mhusika Kabula ambaye aliamini baada ya kumuua Derrick atakuwa amemaliza kila kitu na atakuwa na uwezo wa kuendelea na maisha yake. Mwandishi anathibitisha hilo kwa kusema:

> Simu ya kwanza kuingia ilikuwa ni ya Rais Gabriel alishangazwa na taarifa alizozipata katika televisheni wakati alikwisha taarifiwa na Kabula kuwa Derrick alikufa katika mapango … (uk. 90).

Nukuu hii inaonesha jinsi ambavyo riwaya hii inavyoonesha kuwa mtu akifa anakuwa ametoweka, hana maisha tena. Mwandishi anaonesha kuwa Kabula na Rais Gabriel waliamini kuwa baada ya Derrick kufa kwenye mapango, mipango yao ya kuoana itakuwa imefanikiwa kwa kuwa hakutakuwa na changamoto nyingine. Ndoa baina ya Rais Gabriel na Kabula itafanikiwa kutokana na kifo cha Derrick. Pia, katika riwaya ya *Almasi za Bandia* mwandishi anaonesha kuwa Baba yake Tereza alifariki muda mrefu baada ya uhuru. Mwandishi anathibitisha kwa kusema:

> …Baba yake Tereza alifariki miaka michache tu baada ya uhuru, wakati Tereza akiwa darasa la tano katika shule ya bweni. Mzee Mtweza alikufa kutokana na kuugua kwa kihoro (uk. 85).

Dondoo hili linamwonesha baba yake Tereza kuwa alifariki baada tu ya kupata uhuru. Na ingawa katika kijiji chao Tereza walipata shida ya mvua, pamoja na kwamba walimkumbuka baba Tereza, lakini hawakuonesha kama kuna msaada anaweza kuwapatia akiwa huko peponi. Jambo hili linakengeusha utamaduni wa jamii ya Waswahili kwa kupuuza na kutoamini juu ya nguvu aliyonayo mtu baada ya kifo. Katika mahojiano ya uwandani, Kasoga (ktj) anasema:

> Katika jamii za sasa watu wengi wameathiriwa na utandawazi ambapo wanasahau nguvu waliyonayo mahoka, ambao walisaidia katika kutatua matatizo yanayotokea katika jamii. Riwaya hizi zinaonesha mtu akifa kila kitu kimeishia hapo. Jambo hili linapingana na utamaduni wa Waswahili wanaoamini kuna maisha baada ya kifo (Utafiti, 2022).

Maelezo hayo ya Kasoga (ktj) yanathibitisha mkengeuko uliopo katika suala la kifo ambapo jamii inaamini mtu anapokufa hawezi kurudi katika maisha ya kawaida. Imani hii inakiuka misingi ya utamaduni iliyokuwa inawaunganisha watu waliohai na wale waliokufa. Kwa ujumla, data za uwandani na maktabani zinaonesha jinsi mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika masuala ya kifo ambapo katika maisha ya kabla ya kipindi cha utandawazi waandishi walisawiri masuala ya kifo kuwa yalihusu jamii nzima na walishirikiana katika huzuni na majonzi. Riwaya teule zilizotumika zinathibitisha mkengeuko kwani riwaya hizi zinasawiri suala la kifo kama sherehe na kufurahia jambo linalokwenda kinyume na utu wa mtu katika jamii ya Waswahili.

4.4.4 Maadili

Maendeleo ya sayansi na teknolojia katika jamii yameibua vifaa vya kidigitali kama mitandao ya kijamii, televisheni na simu ambavyo kwa kiasi kikubwa vinasambaza utamaduni wa kigeni ambao umeleta athari kwa jamii. Kitendo cha wanajamii kukumbatia tamaduni za kigeni zilizokuja na utandawazi kumepoteza thamani ya maadili iliyofungamanishwa katika mila na desturi za jamii husika. Utamaduni huo unasababisha ongezeko la mmomonyoko wa maadili katika jamii kutokana na athari zilizoletwa na utandawazi (Kabiru, 2013 na Mbele, 2020).

Utafiti umebaini kuwa, maadili yaliyopo katika riwaya teule yamebeba taswira ya Umagharibi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* mwandishi anaelezea namna Rais Gabriel alivyokuwa anafanana na Rais wa Zimbabwe aliyediriki kufanya mapenzi na wanaume wenzie. Mwandishi anadhihirisha kwa kusema:

> Alikuwa ni Rais mpenda ngono kupita kiasi. Wengi walimlinganisha na Rais Canaan Banana wa Zimbambwe aliyediriki hata kufanya mapenzi na wanaume wenzake. Gabriel alikuwa mtu wa kuoa na kuacha (uk.55).

Nukuu hii inaonesha kuwa misingi ya maadili iliyopo katika utamaduni wa Waswahili haikusisitiza kuoa na kuacha bali kuoa wanawake wengi ulikuwa ufahari kwa mwanaume. Rais Gabriel alikuwa mtu anayependa ngono na mara nyingi alioa na kuacha wanawake. Walimfananisha na Rais Canaan Banana aliyediriki kufanya mapenzi na wanaume wenzake. Jambo hili si la kimaadili na linakwenda kinyume na misingi ya kimaadili iliyopo katika utamaduni wa Waswahili. Imebainika kuwa, jamii ya Waswahili inasisitiza ndoa kati ya mwanamke na mwanaume na kitendo cha kufanya mapenzi kinyume na maumbile ni kitendo ambacho hakiruhusiwi na hakikubaliki katika jamii. Pia, katika riwaya ya *Almasi za Bandia* mwandishi amemtumia Bwana Ashanti aliyekuwa anafungulia sinema ya uasherati kwa ajili ya kuwanasia wasichana kusawiri mkengeuko wa maadili. Mwandishi anasema:

> …Bwana Ashanti alifungulia video yake na kuonyesha sinema ya uasherati iliyojaa uhabiti wa kihayawani. Alionyesha kwa ridhiko la furaha akimsimulia kwamba hizo sinema ndizo ambazo huwa anawanasia wasichana…(uk. 50).

Dondoo hili linaonesha namna Bwana Ashanti alivyokuwa huru kufungulia video za uhayawani na kumwonyesha Yakini akijisifu kuwa video hizo anazitumia kuwanasia wasichana. Katika utamaduni wa Waswahili jambo hili linakwenda kinyume na mfungamano wa maadili ambayo yanasisitizwa katika jamii. Jambo hili linashadidiwa na nadharia ya Ubaada Ukoloni msingi wa mwingiliano wa kitamaduni unaoelezea jinsi nchi za Kiafrika na Magharibi zinavyoingiliana katika masuala ya kimaadili. Katika mahojiano ya uwandani na Jumanne (ktj), suala hili linadhihirika anaposema:

> Utandawazi umekuja na masuala ya kuingia katika mitandao ya kijamii na kuona vitu ambavyo si vya kimaadili. Waandishi wa riwaya za utandawazi wanasawiri masuala haya katika kazi zao jambo linaloendelea kuharibu utamaduni wa Waswahili kwa kuiga tabia ambazo hazikuwepo. Elimu ambayo watu huipata kwa kutumia mitandao na kupakua vitu ambavyo vinavunja maadili ya Waswahili na kupelekea utamaduni kuendelea kuharibika. Hivyo, utamaduni wa Waswahili unakengeuka kwa kufuata utamaduni wa Kimagharibi (Utafiti, 2022).

Maelezo haya yanaonesha kuwa, utandawazi katika jamii ya Waswahili umeingiwa na usasa wa kutumia mitandao ya kijamii. Uhuru wa kuingia katika mitandao ya kijamii umepelekea vijana wengi kujifunza vitu ambavyo havisisitizi maadili

yaliyopo katika jamii ya Waswahili. Jambo hili linapelekea kuendelea kujifunza maadili yaliyopo katika utamaduni wa kigeni ambao unakwenda kinyume na jamii ya Waswahili. Oyinade na Daramola (2015) wanathibisha kuwa utamaduni wa Waswahili umeathirika kutokana na kuingia kwa utandawazi ambapo filamu za kigeni, vipindi mbalimbali vya televisheni na bidhaa za kigeni zimetawala katika nchi ya Afrika. Waafrika wanapoikumbatia, kuitegemea na kuiamini mitandao ya kijamii kwa kila jambo, ambayo kwa sehemu kubwa imesheheni maisha ya jamii za Kimagharibi, huendelea kusambaza utamaduni wao ambapo vijana huendelea kubadilika kitabia, mwono na sifa.

4.4.5 Imani za Kidini

Utandawazi umechangia kuenea kwa dini za Kimagharibi katika jamii za Kiafrika wakiwamo Waswahili wakati dini jadi zikiwa zimedhoofishwa. Imani za dini za kijadi zilichukua nafasi kubwa katika kazi za fasihi zilizokuwa zinatungwa na Waafrika kabla ya utandawazi kukua kwa kasi. Ujio wa wageni katika nchi za Kiafrika umebadilisha mitazamo ya Waswahili kuhusu dini zao za asili ambazo zimeonekana ni ushamba kutokana na usasa ulioingia katika jamii hizo. Kusambaa kwa utandawazi katika jamii hizo kumesababisha dini za kijadi kukosa nguvu kutokana na kuenea kwa ustaarabu mpya wa dini za kigeni ambao umekithiri katika maisha ya jamii (Alloy, 2003 na Sanga, 2018).

Matokeo yanaonesha kuwa, dini za kigeni zinakiuka misingi ya kimaadili katika jamii. Katika kipindi cha utandawazi dini za kijadi zilizokuwapo katika jamii zinaonesha kutostaarabika na kutumia dini zilizoletwa na wageni ni kigezo cha ustaarabu. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* mwandishi anasawiri jinsi imani ya Kikristo inavyokiuka maadili katika jamii. Mwandishi anasema:

> Maelfu ya watu walifurika kanisani, ilikuwa siku ya furaha lakini katika maelfu hayo hapakuwepo ndugu hata mmoja wa Kabula. Ilikuwa ni siku ya harusi yake na Rais Gabriel. Magari yasiyo na idadi yalikuwa nje na palikuwa na ulinzi mkali kupita kiasi. Kifupi serikali ni kama ilihamia kanisani siku hiyo. Derrick alivaa kofia kubwa na ndevu za bandia na kufanikiwa kuingia hadi ndani ya kanisa bila kuruhusiwa, aliketi kiti cha nyuma bila kugundulika, akisubiri muda ambao mchungaji angeuliza. Ni nani anaweka pingamizi ndoa hii

> isifungwe! Moyo wake ulidunda kwa nguvu na jasho jingi lilimtoka na kuzilowanisha nguo zake (uk. 102).

Nukuu hiyo hapo juu inaonesha jinsi imani ya Kikristo iliyoletwa na wageni inavyoenda kinyume na maadili yaliyopo katika utamaduni wa Waswahili. Mchungaji ambaye alifungisha ndoa ya Kabula na Derrick anahalalisha ndoa nyingine baina ya Kabula na Rais Gabriel katika kanisa hilo. Maadili yaliyokuwapo katika jamii ya Waswahili yanakiukwa na kuona Umagharibi ndio ustaarabu unaotakiwa katika jamii. Pia, mwandishi amesawiri mauaji yaliyotokea katika kanisa jambo ambalo linakiuka utu wa mtu katika jamii ya Waswahili. Mwandishi anathibitisha kwa kusema:

> Kwa….kwe...li.. ha..ta..mi…mi..siju..i ame..fikaje ha..! kabla sentensi yake haijamalizika Kabula alilegea mwili na kuanguka chini macho yake yakiwa yamegeukia juu. Heka heka ilianza kanisani watu wakijaribu kumbeba Kabula kumtoa nje ya kanisa ili akimbizwe hospitali. “Meja John!” Rais Gabriel alimwita mpambe wake. “Ndiyo mkuu! Hebu ua huyu mdudu haraka sana sitaki kumwona! (uk. 105).

Dondoo hilo hapo juu linaonesha ambavyo kanisa limegeuka kuwa sehemu ya kutoa uhai wa mtu. Jambo hili linakengeuka misingi katika utamaduni wa jamii ya Waswahili. Kanisa lilifunza upendo kwa binadamu na kuwa na umoja, jambo ambalo katika riwaya teule limekiukwa. Badala yake, wanaonesha kanisani kama sehemu ya kufanya matendo ambayo si ya kimaadili. Pia, katika riwaya ya *Almasi za Bandia* mwandishi anamtumia Yakini kuonesha imani kwa Mungu ambapo aliogopa kubishana na kufanya mahojiano na wanafunzi wenzake kuhusu kati ya Mungu na wanasayansi nani zaidi? Wanasayansi waliamini vitu vya kisayansi ni vitu halisi kwa kuwa vinaonekana lakini Mungu ni dhahania, haonekani. Mwandishi anathibitisha hilo kwa kusema:

> Hapa ndipo Yakini aliposhuhudia vita vikali kati ya sayansi iliyodai kusimamia katika misingi ya uyakinifu na dini inayodaiwa kusimamia misingi ya udhanifu, ikihalalisha unyonge na ugandamizwaji. Mwanzoni, Yakini alihofu kuwa hayo majengo yangeweza kubomoka wakati wowote kutokana na ghadhabu za Mwenyezi Mungu. Aliona ajabu jinsi gani watu hawa walikuwa hawakumbuki kwamba Mungu aliwahi kuingilia baadhi ya mambo kati, kama vile alivyoleta gharika katika enzi za Nuhu, na alivyotia kiberiti Sodoma na Gomora, au hata yaliyompata Yona alipojitia kumkimbia Mungu, kisha akaishia kumezwa na hatimaye kutapikwa na nyangumi (uk. 18).

Nukuu hii inazidi kuthibitisha kuwa dini za kigeni zilizopo katika jamii bado zinasisitiza na kuhalalisha unyonge na ugandamizaji. Utamaduni wa jamii unakengeuka kwa kutofuata misingi ya kiutu inayosisitizwa katika jamii. Imebainika kuwa, licha ya dini za kigeni kusisitiza ustaarabu wa kuabudu kutoka katika jamii za Kimagharibi, dini hizi zinawakandamiza watu katika jamii. Katika mahojiano ya uwandani, Kasoga (ktj) anasema:

> Baada ya ujio wa utandawazi kumekuwa na mapokeo ya dini kutoka katika nchi za Kimagharibi zinazoonesha ustaarabu. Nchi za Kiafrika zinasadikika kuwa hazijastaarabika kutokana na kuabudu miungu iliyokuwapo katika jamii. Utandawazi umeleta dini ya Ukristo na Uislamu ambazo zinakiuka maadili yaliyokuwa yanasisitizwa katika jamii. Waandishi wa riwaya za sasa wanasawiri mabadiliko haya katika riwaya zao na kuacha dini za mababu na mabibi zilizokuwa zinatambulisha utamaduni wa Waswahili (Utafiti, 2022).

Dondoo hili linaonesha jinsi maisha ya jamii yalivyobadilika kutokana na uwepo wa imani za dini tofauti katika jamii zilizoletwa na utandawazi. Waandishi wanasawiri imani za kigeni zilizokuja katika jamii yao na kutozipa nafasi dini jadi katika riwaya zao ambazo zina umuhimu wa kutambulisha maisha ya Waswahili. Oni (2005) anashadidia kwa kusema Utamaduni wa Kiafrika umebadilika kutoka katika asili na kuiga utamaduni wa kigeni. Jinsi ya kuabudu miungu imeondoshwa, sasa wanamtegemea Mungu katika jamii za Kiafrika ikiwamo Waswahili. Jambo hili linakengeusha asili ya utamaduni wa Mswahili.

4.4.6 Mavazi

Mavazi ni miongoni mwa kipengele cha utamaduni kilichopokea mabadiliko kutokana na mwingiliano kati ya jamii za Kimagharibi na Kiafrika. Mwingiliano huu umesababisha kuenea kwa mavazi ya kigeni ambayo yana athari katika utamaduni wa jamii. Athari hizo zimejipambanua na kusababisha kupotea kwa uthamani wa maadili yaliyopo katika jamii ya Waswahili kupitia mavazi. Hivyo, mavazi yanayoonesha taswira ya mavazi ya kustiri katika utamaduni asilia wa Waswahili yamepotea na kubaki mavazi ambayo yanaeneza Umagharibi katika jamii za Kiafrika (Omer, 2017).

Matokeo yanaonesha kuwa, mavazi yanayosawiriwa hayaoneshi thamani ya maadili yanayosisitizwa katika utamaduni wa Waswahili. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais*

Anampenda Mke Wangu mwandishi anathibitisha kwa kumtumia Kabula aliyekuwa anavaa nguo fupi zilizoacha maungo ya mwili wake wazi na kusababisha ajali mbaya barabarani. Mwandishi anaeleza kuwa:

> Nguo fupi alizovaa zilimfanya awape wanaume wengi matamanio na kila mtu alikiri kuwa mke wa Derrick alikuwa mwanamke mzuri kuliko mwanamke yoyote yule katika jiji hilo. Kila mwanaume aliyeuona uzuri wa Kabula alitamani kuwa naye kitandani kuna wakati alisababisha ajali mbaya ya basi la abiria iliyoua watu saba pale pale na kujeruhi wengine ishirini, baada ya dereva wa basi kumkodolea macho Kabula na kujisahau kuwa alikuwa barabarani (uk. 25).

Nukuu hii inaonesha jinsi nguo fupi zinavyosawiriwa na waandishi kama sehemu ya uzuri wa mwanamke kinyume na utamaduni wa jamii. Imebainika kuwa katika jamii za Kiafrika wakiwamo Waswahili uzuri wa mwanamke hauonekani kwa kuvaa mavazi yanayoacha viungo vya mwili wazi bali kuvaa nguo zinazoonesha heshima na staha kwa jamii. Matokeo yanaonesha kuwa, nguo fupi alizovaa Kabula zilikuwa na athari kwa watu wanaomzunguka kwani zilisababisha ajali na kuua watu katika basi. Pia, nguo hizo zilipelekea wanaume kumtamani, mambo ambayo hayasisitizwi katika jamii ya Waswahili. Pia, katika riwaya ya *Almasi za Bandia* mwandishi amesawiri mavazi yanayotumiwa na Wazungu namna yalivyovaliwa na wahudumu wa baa. Wahudumu hao walivaa chupi na sidiria tu jambo ambalo linadhihirisha mkengeuko wa mavazi yaliyopo katika utamaduni wa Waswahili. Anaeleza kuwa:

> …Kama vile hakuwa anasikia alichokuwa anakisema Merton na huku kageukia kwenye kaunta, Zambe alianza kusema kwa utani wa kificho “Hii baa ni nzuri sana. Na sasa nimetambua kwa nini watu wengi tumekutana hapa kwa mara moja. Huku akionyesha picha zilizobandikwa ukutani akaendelea, Hebu tazama hayo mapicha ya wanawake wanaokaa uchi, na halafu kule kaunta wauzaji waliovaa sidiria na chupi tu! Mwanaume uombe nini tena? (uk. 99).

Dondoo hili linaonesha kuwa, mwandishi amesawiri mavazi ya chupi na sidiria yaliyokuwa yanavaliwa na wahudumu katika baa. Watu wengi walikwenda katika baa ya Wenches kutokana na mavazi yaliyokuwa yakivaliwa na wahudumu hao. Jambo hili linathibitisha mkengeuko katika mavazi kwani Waswahili kwao chupi na sidiria ni mavazi ya ndani ambayo mtu hatakiwi kuonekana akiwa amevaa bila nguo nyingine kwa juu. Nadharia ya Ubaada Ukoloni inashadidia kuwa mwingiliano wa

utamaduni katika jamii umepelekea jamii ya Waafrika kuiga mavazi ambayo hayautambulishi utamaduni wao na kuiga mavazi ya Kimagharibi kutokana na utandawazi uliopo katika jamii. Katika mahojiano ya uwandani, Faustine (ktj) anathibitisha kwa kusema:

> Waandishi wa riwaya ya Kiswahili wanaandika kazi zao kwa kuzingatia soko la kazi zao. Mwandishi anaonesha mwanamke mzuri ni yule ambaye amevaa mavazi ya kuachia wazi viungo vya mwili, kitu ambacho hakipo kwenye utamaduni wa Waswahili. Utamaduni wa Waswahili humwonesha mwanamke mzuri ni yule anayevaa mavazi ya stara na heshima kwa jamii. Hivyo, usawiri wa mavazi yasiyo na stara katika riwaya ya Kiswahili ni kuendelea kukengeusha utamaduni wa Waswahili jambo linaloendelea kupoteza asili ya Waswahili katika maisha ya jamii (Utafiti, 2022).

Maelezo ya Faustine (ktj) yanaonesha kuwa mavazi yamebeba taswira ya maisha ya jamii fulani kupitia kufungamana na utamaduni wa jamii husika. Mavazi ya kuacha viungo wazi katika jamii ya Kiafrika hayasisitizwi. Jamii iliamini mavazi hayo hayaoneshi maadili kwa jamii. Pia, mavazi hayo yanapotumiwa na watu wa Kimagharibi katika utamaduni wao hayaoneshi uvunjifu wa misingi ya kitamaduni iliyopo katika jamii kwa kuwa ujumi wa mavazi yao ndivyo ulivyo. Hivyo, waandishi wanapoandika kwa kusawiri mavazi ya Kimagharibi utamaduni wa Waswahili unakengeuka na kuingiwa na Umagharibi.

4.5 Athari za Mkengeuko wa Utamaduni wa Waswahili katika Riwaya Teule

Sehemu hii imejibu swali la lengo la tatu lililouliza, “mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili una athari gani katika riwaya teule za Kiswahili?” Matokeo ya utafiti huu yamebainisha athari chanya na hasi za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi kama ifuatavyo:

4.5.1 Athari Chanya

Utafiti huu umebaini athari chanya za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule za Kiswahili ambazo ni: Kuleta upya katika riwaya ya Kiswahili, kusambaa kwa ujumi wa utamaduni wa kigeni, upanuzi wa soko na hadhira, kuongezeka kwa watunzi na kuongezeka kwa maarifa mapya. Ufuatao ni ufafanuzi wa athari hizo:

4.5.1.1 Kuleta Upya katika Riwaya ya Kiswahili

Mabadiliko ya kiutamaduni yanayotokea katika jamii zama za utandawazi yanasawiriwa katika kazi za kifasihi ikiwamo riwaya ya Kiswahili kwa namna ambayo inaleta ubunifu mpya katika uandishi wa riwaya hizo. Imebainika kuwa, waandishi wa riwaya teule wametumia mbinu mbalimbali katika kuleta upya wa riwaya zao. Mbinu hizo ni kama kuchanganya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Aidha, waandishi hao wametumia lafudhi za kigeni kama kihindi katika uandishi wa riwaya hizo. Mambo haya yamezifanya riwaya zilizoandikwa kuwa na mvuto kwa wasomaji wake kutokana na kutumia mbinu mpya katika uandishi wake. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* mwandishi amemtumia Dick ambaye alitaka kulipa kisasi kwa Derrick ambaye ilimlazimu kutafuta koti la kidaktari ili aweze kuingia katika chumba alicholazwa Derrick hospitalini. Mwandishi anatueleza kuwa:

> "*Can I have one white doctor's coat* ?" (Ninaweza kupata koti moja jeupe la daktari?)
> "*Yes, sir* !"(Ndiyo mzee)
> "*How much*?"(Kiasi gani)
> "*Fity thousand Rand Only*!" (Rand elfu hamsini tu) (uk.189)

Dondoo hili linaonesha jinsi mwandishi alivyotumia mtindo wa lugha ya Kiingereza na kutafsiri mazungumzo hayo kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Jambo hili linaleta muonekano wa tofauti katika kazi yake. Riwaya hii inaonesha ubunifu aliotumia mwandishi katika kuifanya kazi yake kuwa na mvuto wa kipekee kwa wasomaji. Pia, katika riwaya ya *Almasi za Bandia* mwandishi ametumia lafudhi ya lugha ya Kihindi katika kuleta upya katika kazi yake. Anatueleza kuwa.

> "Ndiyo kijana, iko tambua nyinyi ishi hali gumu. Lakini kili mutu nalipwa kwa jusi yake. Fanyakaji mingi *African* hapana soma iko vivu. Hapana kuwa kama *European*" (uk.26)

Nukuu hiyo hapo juu inaonesha jinsi mwandishi wa riwaya ya *Almasi za Bandia* alivyosawiri uhalisia wa maisha ya jamii kwa kutumia lafudhi ya kihindi. Wasimamizi wa chama cha wafanyakazi kutoka Uingereza walitumia lafudhi ya kihindi kwa lengo la kutaka kuunda vyama vya wafanyakazi katika nchi ya Afrika. Kama inavyoelezwa katika msingi wa nadharia ya Ubaada Ukoloni mwingiliano wa kiutamaduni katika nchi za Kiafrika umeleta upya katika mambo mbalimbali

yakiwamo matumizi ya lugha za kigeni katika uandishi wa kifasihi. Katika mahojiano ya uwandani, Jumanne (khj) anasema:

> Mkengeuko wa utamaduni katika riwaya umeibua upya wa kutumia lugha za kigeni kwa lengo la kuweka ubunifu mpya katika riwaya. Mbinu hizi huzitofautisha riwaya zilizotungwa katika mrengo wa kabla ya utandawazi. Mwandishi anapotumia lugha ya Kiingereza katika riwaya ya Kiswahili ni ubunifu unaoleta upya katika uandishi wa riwaya katika zama za sasa. Jambo hili linazifanya riwaya kukua na kuvuka mipaka siku hadi siku (Utafiti, 2022).

Kama ilivyojadiliwa hapo juu, dondoo hili linaonesha jinsi ambavyo riwaya za kabla na baada ya utandawazi zinavyotofautiana katika uandishi wake. Riwaya zinazosawiri mkengeuko wa masuala ya utamaduni zimebeba upya katika uandishi kutokana na utandawazi ulioingia katika jamii zao. Hali hii inazitofautisha na riwaya zilizoandikwa kabla ya ujio wa utandawazi ambazo zimesawiri masuala ya utamaduni wa jamii ya Waswahili.

4.5.1.2 Kusambaa kwa Ujumi wa Tamaduni za Kigeni

Waandishi kujitenga na utamaduni wao na kuiga utamaduni wa nchi za Kimagharibi kunasababisha utamaduni wa nchi hizo kusambaa kupitia kazi mbalimbali za kifasihi kama riwaya. Jambo hili linaendelea kutandawazisha masuala yaliyopo katika utamaduni wa kigeni kama mavazi, vyakula, ndoa, lugha na imani za dini. Utafiti umebaini kwamba, masuala haya yanasaidia kujua mambo kutoka katika jamii zingine za Kimagharibi. Watu kutoka katika jamii ya Kiafrika wanajifunza na kuzijua tamaduni za jamii nyingine nje ya Afrika kupitia riwaya ambazo zinakuwa wakala wa kusawiri utamaduni wa kigeni. Kwa mfano, katika riwaya ya *Almasi za Bandia* mwandishi amesawiri namna wazungu wanavyothamini wanyama kama mbwa na katika nchi zao kuna chama cha kutetea haki za wanyama hao. Kutokana na riwaya kusawiri mtindo huo wa maisha, nchi za Kiafrika zinajua namna wazungu wanavyoishi na wanyama katika jamii zao. Mwandishi anasema:

> …Baada ya ukimya mfupi aliendelea, Halafu basi, kichekesho ni kwamba, kuna wakati fulani kulitokea maandamano ya watu weupe wakidai kwamba tabia ya kuuza mbwa wa Kiingereza katika nchi ya Nigeria, ikomeshwe kwa sababu huko wanawatumia kwa ulinzi badala ya kuwafuga kama wanyama wa nyumbani wanaostahili upendo wa kila hali. Umewahi kusoma habari ya chama kinachoitwa

> *Animal Liberation Front*? Hata kabla hajapata jibu aliendelea, “Hiki ni chama kinachotetea haki za wanyama (uk. 8).

Nukuu hii inaonesha namna riwaya zinavyosawiri namna mbwa wanavyothaminiwa katika nchi ya Uingereza ambapo wanatakiwa kuishi na kuwa na haki kama binadamu. Pia, wanyama wanatakiwa kuishi na kupewa upendo wa aina zote pasipo kutumikishwa na kunyanyaswa majumbani. Riwaya hizi zimekuwa wakala wa kutambulisha na kusambaza tamaduni za kigeni katika jamii za Kiafrika. Jambo hili linashadidiwa na mawazo ya nadharia ya Ubaada Ukoloni ambayo huona mwingiliano wa utamaduni uliopo katika nchi za Afrika umesambaza tamaduni za kigeni katika jamii hizo. Katika mahojiano ya uwandani, Khamis (ktj) anasema:

> Uandishi wa riwaya zinazosawiri mkengeuko wa utamaduni zimekuwa wakala wa kutandawazisha utamaduni wa Kimagharibi. Mwandishi anasawiri namna mavazi yaliyopo vyakula, ndoa na sanaa zao ambapo mambo haya yanafanya wasomaji wa Kiafrika kujifunza tamaduni za kigeni na kuenea katika jamii (Utafiti, 2022).

Kama ilivyojadiliwa hapo juu, dondoo hili linaonesha namna riwaya zilizoandikwa kipindi cha utandawazi zinavyosawiri utamaduni mseto kati ya jamii za Kimagharibi na Kiafrika. Hii ni kupitia vyakula, ndoa na mavazi vinavyokuwa vinasawiriwa na waandishi wa riwaya. Jambo hili linaleta umuhimu kwa hadhira wa kujifunza tamaduni za nje ya Afrika ambazo zinawasaidia kwenda na wakati kutokana na mabadiliko yanayotokea katika jamii yao. Ogbum (1922) anashadidia kwa kusema:

> *Invention, discovery and diffusion are some of the way by which culture can change or grow invention for instance the recombination of exsting cultural elements its fashion new thing* (pg. 12).

> Uvumbuzi, ugunduzi na uenezaji ni baadhi ya njia ambazo utamaduni unaweza kubadilika na kukua kwa mfano mchanganyiko wa vipengele vya kiutamaduni vilivyopo ni mtindo wa mambo mapya. (Tafsiri ya Mtafiti).

Nukuu hii inaonesha jinsi utamaduni wa jamii ulivyobadilika kutokana na mabadiliko ya kiteknolojia yaliyopo katika jamii. Waandishi wanapoandika kazi za riwaya wanakuwa wanakwenda na mabadiliko yanayotokea katika jamii na kushindwa kuhifadhi utamaduni wa jamii husika. Hivyo, kuiga utamaduni mpya wa kigeni unaokuja na utandawazi kunafanya utamaduni wa Waswahili uonekane wa kishamba na kuendeleza masuala ya Kimagharibi yanayoonesha ustaarabu.

4.5.1.3 Upanuzi wa Hadhira

Kutokana na riwaya ya Kiswahili kusawiri mkengeuko katika masuala ya utamaduni kunasababisha kuongezeka kwa watumiaji wa utanzu huo. Riwaya hizo zinakuwa na mawanda mapana kwa kuwa zinasawiri masuala mtambuka ya kidunia. Hivyo, zinakuwa na wasomaji dunia nzima. Hali hii imesaidia waandishi kutojifunga na mikatale ya kijiografia na kuandika masuala mbalimbali yanayopatikana katika nchi za Kiafrika na Kimagharibi. Hivyo, riwaya hizi zinaleta umoja na mshikamano baina ya pande mbili ambapo watumiaji kutoka maeneo mbalimbali ya nchi wanaongezeka. Katika riwaya ya *Almasi za Bandia* mwandishi amesawiri tatizo la ubaguzi wa rangi katika nchi za Ulaya. Mwandishi anasema kuwa:

> Lakini hii, ni ushenzi mtupu! Jana kwa mara ya kwanza nimegundua kwamba nchi hii ina ubaguzi. Nilikuwa nadhania kwamba watu weusi wana matatizo yao wenyewe wanapodai kuna ubaguzi, lakini sasa naamini (uk. 99).

Dondoo hili linaonesha namna riwaya hizi zinavyojadili masuala mbalimbali yaliyopo kwenye ulimwengu kama ubaguzi wa rangi ambapo mambo haya yanajadiliwa kwa kina katika riwaya hizi na kusomwa na watu kutoka katika nchi mbalimbali. Mwandishi wa riwaya hii amevuka mipaka kwa kujadili mambo yanayosumbua ulimwengu zaidi na maudhui haya kuwafikia watu mbalimbali katika maeneo yao. Nadharia ya Ubaada Ukoloni katika msingi wa mwingiliano wa utamaduni unaelezea kuwa utandawazi umeleta mwingiliano baina ya nchi za Kimagharibi na Kiafrika kupitia kusawiriwa kwa mambo mbalimbali katika riwaya ya Kiswahili. Katika mahojiano ya uwandani, Kihongosi (ktj) anasema:

> Mabadiliko yaliyoletwa na utandawazi katika kazi za kifasihi yamepelekea kuongezeka kwa watumiaji wa riwaya ya Kiswahili. Kutokana na riwaya hizi kuwa na mvuto kwa hadhira. Hii ni kwa sababu riwaya hizi zinasawiri masuala yanayosumbua ulimwengu kwa sasa. Jambo ambalo linapelekea riwaya kuvuka mipaka na kupata watumiaji kutoka katika nchi mbalimbali. Hivyo, riwaya hizi zinafikisha maudhui kwa hadhira (Utafiti, 2022).

Kama ilivyojadiliwa hapo juu Kihongosi (ktj) anashadidia kuwa mabadiliko yanayoletwa na utandawazi katika jamii yamesababisha riwaya ya Kiswahili kupata watumiaji wengi kutoka katika maeneo mbalimbali kutokana na riwaya hizi kusawiri masuala mbalimbali yanayousumbua ulimwengu katika kipindi cha utandawazi.

Hivyo, riwaya hizi zinasawiri mawanda mapana kwa kuyaelezea maisha kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Hivyo, kupelekea kuongezeka kwa watumiaji wa riwaya hizo katika kipindi cha utandawazi.

4.5.1.4 Kuongezeka kwa Watunzi

Utafiti umebaini kuwa kutokana na mkengeuko wa utamaduni unaojitokeza katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi, umepelekea kuibua vipaji vya waandishi wanaoandika kazi bila kuzingatia utamaduni wa jamii ya Waswahili. Waandishi hawa wanaandika riwaya kwa kusawiri hali halisi iliyopo katika jamii kwa wakati huo kulingana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Kwa mfano, katika riwaya ya *Almasi za Bandia* mwandishi amesawiri vyakula kama chipsi kuku vilivyokuwa vinaliwa na wazungu katika nchi ya Ulaya. Pia, mwandishi amesawiri nyimbo mbalimbali za kigeni zilizokuwa zinapigwa katika kumbi za starehe, nyimbo hizo kama *reggae, calypo, rumba* na hata nyimbo za *kinshansa* ambazo ziliwastarehesha akina Zambe, Yakini na Merton katika kumbi za starehe. Kutokana na waandishi hawa kuangazia masuala ya maisha kwa kina kwa wakati wa sasa inapelekea vitabu wanavyoandika kupendwa kwa wingi kwa sababu ya masuala yanayojadiliwa katika kazi hizo. Hivyo, uandishi wa mkondo wa mkengeuko katika masuala ya utamaduni unapata waandishi chipukizi wengi kutokana na riwaya kuandikwa pasipo kufungwa na mipaka ya kimaeneo. Mwandishi anakuwa huru kuandika mambo ambayo yanaonesha uhalisia uliopo katika jamii kupitia kazi za riwaya. Katika mahojiano ya uwandani, Mabawa[18] anasema:

> Mabadiliko yaliyopo katika jamii yanapelekea kuibuka kwa watunzi wenye vipaji mbalimbali ili kuweza kusawiri hali ya maisha iliyoko katika jamii. Waandishi wanaibuka na kuandika kazi za riwaya kwa kusawiri ulimwengu kwa ujumla. Jambo hili linasababisha kazi ya riwaya kusomwa na watu wa maeneo mbalimbali. Hivyo, kazi hizi kusomwa kwa wingi kiulimwengu (Utafiti, 2022).

Nukuu hii inaonesha namna ambavyo mabadiliko yaliyopo katika jamii yanavyochangia kuibuka kwa vipaji vya waandishi kuweza kuandika masuala yanayopatikana katika jamii kwa wakati huo. Uibukaji wa masuala halisi katika jamii unasababisha kuwepo kwa wimbi la waandishi katika kipindi cha utandawazi.

[18] Bi. Eunice Mabawa ni mwanafunzi wa Shahada ya awali katika fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 16/5/2022 katika eneo la studio ya CBSL.

4.5.1.5 Ongezeko la Maarifa Mapya

Kutokana na kuwepo kwa matini nyingi za kifasihi ambazo hazifungwi na utamaduni wa jamii moja kumesababisha wanajamii kukua kifikra kwa kupata mawazo kutoka katika maeneo mbalimbali na kujua vitu vingi kutoka nje ya jamii yao. Hali hii imepelekea kuwapo kwa mwingiliano wa kitamaduni hata katika uandishi wa kazi mbalimbali za riwaya ya Kiswahili. Waandishi wanajikita katika kuchambua masuala ya kina yaliyopo katika jamii zao kwa kuyaona mambo mapya kutoka katika maeneo mengine yanaongeza ujuzi katika maisha. Kwa mfano, katika riwaya ya *Almasi za Bandia* mwandishi anaonesha mji wa Glasgow ambao ulikuwa maarufu kwa viwanda. Anasema:

> Glasgow, mji wenye majengo meusi kwa sababu ya moshi wa viwanda. Afadhali sasa walikuwa wanayasafisha baadhi yake. Huu ulikuwa kati ya miji ya kwanza ambapo mapinduzi ya viwanda yalitokea, ukawa maarufu kwa ujenzi wa meli. Kadhalika ulikuwa miongoni mwa miji ambamo harakati nyingi za wafanyakazi zilikuwa zimetokea tangu mwanzo wa karne hii hadi miaka ya 1940 (uk.40)

Dondoo hili linaonesha namna mji wa Glasgow uliopo Ulaya ulivyokuwa maarufu kwa ujenzi wa meli. Pia, nchi hii ni miongoni mwa nchi zilizokuwa na harakati nyingi za wafanyakazi ambao walikuwa wanadai haki zao kutokana na hali ngumu ya kiuchumi iliyokuwa imeikumba nchi hii. Waandishi wa riwaya teule wanapokuwa wanasawiri mambo mbalimbali kutoka katika nchi za nje wanakuwa wanaongeza maarifa kwa wasomaji wa kazi za riwaya ambayo yanawasaidia katika maisha ya kila siku. Katika mahojiano ya uwandani, Lukas (ktj) anasema:

> Mabadiliko yanayosawiriwa katika riwaya za Kiswahili yanawasaidia wasomaji kujifunza na kuongeza ujuzi juu ya mambo ambayo walikuwa hawayafahamu au hayakuwepo katika jamii zao. Waandishi wanapoandika kazi zao kwa kusawiri ulimwengu katika mambo mbalimbali inapelekea wasomaji kuelewa masuala yaliyopo nje ya utamaduni wao na kuyachukua endapo yana tija katika jamii yao (Utafiti, 2022).

Kama ilivyokwisha jadiliwa hapo juu Lukas (ktj) anashadidia mabadiliko yanayotokea katika jamii na yanayosawiriwa katika riwaya yana tija kwa jamii. Wasomaji wa riwaya hizo wanapata ujuzi kutokana na yaliyoandikwa katika kazi hizo. Hivyo, wasomaji wanakua kifikra kwa kutafakari mambo muhimu kama

yanavyotokea katika jamii yao na kujijenga katika mtazamo chanya wa mambo yanayotoka nje ya nchi yao.

4.5.2 Athari Hasi

Utafiti huu umebaini athari hasi za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule za Kiswahili ambazo ni kuharibu historia ya utamaduni wa Waswahili, mtazamo hasi juu ya utamaduni wa Waswahili, kupotea kwa thamani ya lugha ya Kiswahili, kuharibu thamani ya utamaduni wa Waswahili, mmomonyoko wa maadili, kupotea kwa utambulisho kupitia riwaya na kupoteza mvuto wa kiujumi wa Kiafrika. Ufuatao ni ufafanuzi wa hoja hizo:

4.5.2.1 Kuharibu Historia ya Utamaduni wa Waswahili

Historia ya utamaduni wa jamii ya Waswahili hutunzwa kwa ajili ya maisha ya vizazi vijavyo. Wanajamii hujifunza historia ya jamii zao kupitia kazi za fasihi ikiwamo riwaya ya Kiswahili ambayo imehifadhi historia ya utamaduni wa jamii. Imebainika kuwa riwaya teule za awali zimefungamana na masuala yaliyopo katika utamaduni wa Waswahili kwa kuonesha namna jamii ilivyoishi kupitia lugha, mavazi, milo na vinywaji, ndoa, sanaa na masuala ya kifo. Utamaduni huo uliobebwa katika riwaya uliwatambulisha na kuhifadhi historia iliyokuwapo katika jamii yao. Hata hivyo matokeo yanaonesha kuwa, baadhi ya riwaya za zama za utandawazi badala ya kuhifadhi utamaduni katika zama za maendeleo ya sayansi na teknolojia, riwaya hizo zinasawiri mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili. Jambo hilo linaharibu historia ya utamaduni wa Waswahili katika vipengele vya mavazi, vinywaji, milo, lugha na dini na kusababisha kupotea na kuacha historia ngeni kwa vizazi vijavyo. Imebainika kuwa, baadhi ya riwaya za sasa zimesawiri utamaduni mseto baina ya wageni na Waafrika wakiwapo Waswahili. Jambo hili linaathiri vizazi vijavyo kwa kutokujua historia ya utamaduni wao ni ipi, kutokana na mchanganyiko wa utamaduni unaosawiriwa katika riwaya hizo.

Utafiti umebaini kuwa, riwaya inatumika kusawiri masuala ya utandawazi zaidi na kuacha thamani ya utamaduni unaowatambulisha Waswahili. Jambo hili linasababisha waandishi kushindwa kutunza kumbukumbu ya utamaduni katika kipindi hiki cha utandawazi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* mwandishi amesawiri mavazi yanayoacha viungo wazi. Mavazi haya

hayafungamani na utamaduni wa jamii ya Waswahili. Kabula anavaa nguo zinazoonesha maungo ya mwili ambayo yanasababisha ajali za barabarani kutokana na madereva kumtamani. Imebainika kuwa, masuala kama haya hayafungamani na maadili yaliyopo katika utamaduni wa jamii ya Waswahili. Pia, katika riwaya ya *Almasi za Bandia,* mwandishi amesawiri mavazi ya wasichana katika baa ya Wenches wanavyouza bia, wakiwa katika mavazi ya chupi na sidiria. Mambo haya hayafungamani na maadili yaliyopo katika utamaduni wa Waswahili. Hivyo, historia ya utamaduni wa Waswahili katika baadhi ya riwaya za sasa umeharibika kutokana na mwingiliano uliopo katika jamii, kama ilivyoelezwa na nadharia ya Ubaada Ukoloni msingi wa mwingiliano wa kiutamaduni kuwa nchi zilizotawaliwa zina utamaduni mseto, jambo hili linajidhihirisha katika riwaya teule. Katika mahojiano ya uwandani na Faustine (ktj), suala hili linadhihirika anaposema:

> Riwaya ya Kiswahili ya zama za sasa ni tofauti na riwaya zilizoandikwa kabla ya utandawazi haujaenea kwa kasi. Waandishi wa sasa wameweka shabaha ya kusawiri masuala ya kigeni ambayo huvutia jamii kwa kiasi kikubwa. Jambo hili linaharibu historia ya utamaduni wa Waswahili iliyokuwapo katika riwaya tangulizi (Utafiti, 2022).

Dondoo hili linaonesha jinsi riwaya za awali na sasa zilivyotofautiana katika kuweka historia ya utamaduni wa Waswahili. Imebainika kuwa, baadhi ya riwaya zilizoandikwa katika kipindi cha utandawazi zimesawiri mwingiliano wa utamaduni baina ya wageni na wenyeji. Jambo hili linaharibu historia ya utamaduni wa Waswahili. Wanajamii wanavutiwa na mambo ya kigeni na kuathiri utamaduni wa jamii. Hivyo, historia ya utamaduni wa Waswahili inaendelea kuharibika na kupotea kutokana na tamaduni za kigeni zilizopo katika jamii.

4.5.2.2 Mtazamo Hasi Juu ya Utamaduni wa Waswahili

Utandawazi umeingia katika jamii za Kiafrika wakiwamo Waswahili na kuleta ustaarabu wa kuona kutumia masuala yaliyoletwa na Umagharibi ni bora kuliko kuendelea kutumia utamaduni wa Waswahili ambao unaonekana kuwa wa kishamba. Mtazamo huu unakwenda moja kwa moja kwa baadhi ya waandishi wa riwaya ambao huona kusawiri utamaduni wa kigeni katika uandishi wa riwaya kunaonesha ubora na kustaarabika. Imebainika kuwa, baadhi ya waandishi wa riwaya ya Kiswahili wanaona bora kufinyanga kazi zao zifanane na mtindo wa Kimagharibi

ndio zionekane kuwa bora katika jamii. Jambo hili linajidhihirisha kwa vijana kuendelea kupenda tamaduni za kigeni kwa kutaka kwenda na wakati na wanaamini utamaduni wa Waswahili hauendi na wakati. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* mwandishi amesawiri masuala ya ndoa yanavyofungamana na usasa. Kabula ana nguvu ya kuamua kuolewa bila kutaka miongozo kutoka kwa wazazi na anaolewa kwa mara ya pili. Jambo hili linashadidiwa na nadharia ya Ubaada Ukoloni msingi wa utabaka ambao unaona mambo ya Kimagharibi ndio kustaarabika na kufuata msingi ya Kiafrika ni kutostaarabika. Katika mahojiano ya uwandani, Ngao (ktj) anashadidia kwa kusema:

> Mwisho wa siku unakuta wanajamii wameiga vitu visivyofaa kwa kuacha kuthamini utamaduni wa Waswahili unaoonekana wa kishamba. Jamii inaendelea kubadilika kwa kuona milo, mavazi, lugha, ndoa na sanaa za kigeni ni bora kuliko vitu vilivyopo katika jamii ya Waswahili. Jambo hili linaathiri utamaduni wa Waswahili katika maisha ya jamii (Utafiti, 2022).

Dondoo hili linaonesha kuwa kutokana na utamaduni wa Kimagharibi kusambaa katika jamii za Kiafrika, hali hii inasababisha wanajamii kuiga na kuthamini vitu mbalimbali vilivyoletwa na wageni kama vile, milo, mavazi, lugha, ndoa na sanaa. Vitu hivi huonekana bora kuliko vitu kutoka katika jamii zao. Ngao (ktj) anasema jambo hili linazifanya tamaduni zilizopo katika jamii kuendelea kudumaa kadri wakati unavyozidi kwenda.

4.5.2.3 Kupotea kwa Thamani ya Lugha ya Kiswahili

Kutokana na baadhi ya riwaya za Kiswahili kuchanganya lugha mbalimbali kama Kiingereza na lafudhi za kigeni, kumebainika kushusha thamani katika lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo msingi wa kuwaunganisha watu katika utamaduni wa Waswahili. Matumizi ya lugha za kigeni katika riwaya ya Kiswahili ni kuendelea kusambaza itikadi za mataifa ya Kimagharibi na utamaduni wao kupitia lugha zao zinazowatambulisha, kama inavyoelezwa na nadharia ya Ubaada Ukoloni msingi wa matumizi ya lugha za kigeni ni kuendeleza ukoloni mamboleo. Lugha ya Kiswahili inaathiriwa na lugha za kigeni ambazo zinaonekana kuwa zina hadhi ya juu kuliko lugha inayowaunganisha watu katika utamaduni wa Waswahili. Imebainika kuwa, matumizi ya lugha za kigeni katika riwaya ya Kiswahili ni kutandawaza tamaduni za Kimagharibi kupitia lugha zao ambazo zinashusha hadhi na kupoteza thamani ya

lugha ya Kiswahili inayotambulisha utamaduni wa Waswahili. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu,* jambo hili linajidhihirisha ambapo mwandishi ametumia mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili katika baadhi ya maeneo. Mwandishi anathibitisha matumizi ya lugha ya Kiingereza katika riwaya teule ya Kiswahili kwa kusema:

> " *He will probably have Paraplegia or even qudraplegia! What is his state of blood pressure at the moments ?"Let me check! Where is the Sphygimomanometer?.* Aliuliza nesi na alipoonyeshwa mashine hiyo alichukua na kuanza kumpima Derrick kwa haraka. "*It is 90/70mmhg!* (uk. 184).

Nukuu hii inaonesha nesi alivyokuwa anahojiwa na daktari kipindi cha kumtibu Derrick aliyekuwa ameumia kipindi cha mapambano kati yake na Rais Gabriel. Anatumia lugha ya Kiingereza katika kujibu. Pia, katika riwaya ya *Almasi za Bandia* mwandishi ametumia lafudhi za lugha za kigeni katika riwaya yake. Mwingiliano kati ya lugha ya Kiswahili na lugha za kigeni ni mkubwa. Katika mahojiano ya uwandani, Feruzi[19] anasema:

> Unakuta mwandishi katika jina la kitabu ameweka jina kubwa la kitabu kwa kutumia lugha ya Kiingereza lakini ukiingia ndani unakuta ametumia lugha ambayo ni mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na kigeni. Jambo hili linashusha thamani ya lugha ya Kiswahili ambayo ndio msingi wa utamaduni wa Waswahili (Utafiti, 2022).

Dondoo hili linaonesha baadhi ya waandishi wa riwaya ya Kiswahili wanatumia lugha za kigeni katika uandishi wa riwaya zao jambo ambalo linaathiri utambulisho wa utamaduni wa Waswahili kupitia lugha za kigeni ambazo zinaathiri lugha ya Kiswahili. Ajayi (2003) anashadidia jinsi ambavyo utandawazi umebadilisha maisha katika jamii na kutumia lugha za kigeni katika masuala ya kijamii ikiwamo katika uandishi wa kazi za kifasihi. Anasema:

> *Globalization is a continuation and expansion of western imperialism this is because to him it is a fresh phase in recolonization of Africa socities which attempts to continue the promotion of western linguistic heritage and literacy esthetic canons at the expeme of African indigenous language and literature* (pg. 32)

[19] Dkt. Abdulmalick Feruzi ni mhadhiri katika idara ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, mahojiano yalifanyika tarehe 8/6/2022 ofisini kwake.

> Utandawazi ni mwendelezo wa kukua kwa utawala wa kimagharibi hii ni kwa sababu kwao ni hatua ya kuonyesha ukoloni mamboleo katika jamii za Kiafrika ambazo zinaendeleza urithi wa lugha za kigeni inapelekea kudumaza lugha na fasihi ambazo zipo kwenye jamii ya Afrika (Tafsiri ya Mtafiti).

Nukuu hii inaonesha kuendelea kutumia lugha za kigeni katika nchi ambazo zimepata uhuru kunaendeleza ukoloni mamboleo katika jamii, jambo ambalo linasababisha jamii kusahau lugha zilizopo katika jamii na kuendeleza lugha za kigeni ambazo zimeletwa na wageni. Kwa ujumla, lugha ya Kiswahili ambayo inawaunganisha watu katika utamaduni wa Waswahili inashuka thamani kwa kutumia lugha za kigeni katika jamii hizo.

4.5.2.4 Kuharibu Thamani ya Utamaduni wa Waswahili

Umagharibi ulioingia katika jamii za Kiafrika umekengeusha utamaduni wa jamii ya Waswahili na kuondoa thamani ya amali za kitamaduni zilizopatikana katika maisha ya jamii. Waswahili katika jamii zao walithamini masuala ya kitamaduni yaliyokuwapo katika jamii zao. Utafiti umebaini kuwa, Umagharibi umesambaza itikadi za kigeni katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Fasihi ya Kiswahili imegubikwa na wimbi la utandawazi kiasi ambacho mwandishi kuandika kwa kuonesha thamani ya maisha ya utamaduni, anaona anapitwa na wakati. Imebainika kuwa, maadili yanayofunzwa katika baadhi ya riwaya zilizoandikwa kipindi cha utandawazi zimebeba misingi ya tamaduni za kigeni ambazo hutofautiana na zile zilizokuwepo katika utamaduni wa Waswahili zilizokuwa zinatoa maadili kwa kufungamana na utamaduni wa jamii ya Waswahili. Matokeo yanaonesha kwamba, mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya umeondoa thamani ya utamaduni asilia kwa kuona tamaduni za kigeni ndizo bora kuliko tamaduni zinazowatambulisha Waswahili katika jamii. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* mwandishi anaonesha jinsi Rais Gabriel alivyofananishwa na Rais Canaan Banana wa Zimbabwe aliyediriki kufanya mapenzi na wanaume wenzake. Katika utamaduni wa Waswahili jambo hili haliendani na maadili ya jamii husika. Thamani ya utamaduni imeharibika kwa kuingiza vitu vipya vya kigeni ambavyo vinaharibu mfumo wa utamaduni. Hivyo, watu wanapuuza mambo ya kitamaduni na kuvutiwa na Umagharibi ambao unaonekana kuwa bora

kuliko mambo yaliyopo katika utamaduni ya Waswahili. Akpa (2002) anashadidia kwa kusema:

> "Maendeleo ya kasi ya sayansi na teknolojia, mila, desturi na tamaduni zimeporomoka kwa kiasi kikubwa katika jamii za Kiafrika kiasi kwamba watu wametupilia mbali mila na desturi zao. Fikra na mawazo ya baadhi ya watu hawaamini kuwa kuzibeba mila na desturi za asili ni kutostaarabika. Kulingana na hayo ndiyo maana watu wengine hutumia ngoma na nyimbo kwa minajili ya starehe tu" (uk. 11).

Nukuu hii inaonesha kuwa katika kipindi hiki cha sayansi na teknolojia watu wameacha kuthamini utamaduni wa jamii zao. Jambo hili linasababisha watu wanaodumisha mila na desturi za Waswahili kuonekana washamba kutokana na kuenea kwa tamaduni za kigeni katika jamii za Kiafrika. Hivyo, utamaduni wa Waswahili unapoteza thamani kwa kutumia zaidi tamaduni za Kimagharibi.

4.5.2.5 Kuimarisha Utamaduni wa Kimagharibi

Kutokana na baadhi ya kazi za riwaya kusawiri utamaduni wa Kimagharibi, utamaduni huo umeimarika zaidi siku hadi siku. Matokeo yanaonesha kuwa, riwaya zinazoandikwa katika kipindi cha utandawazi zimekuwa wakala wa kuonesha mavazi, milo, lugha, vinywaji na maadili ambayo kwa kiasi kikubwa yamefungamana na utamaduni wa Kimagharibi. Utamaduni wa kigeni unaendelea kuenea mpaka katika jamii na Waswahili wanaendelea kujivunia kuwa Waswahili kwa jina ila maisha na mienendo yao haitofautiani na wazungu. Imebainika kuwa mkengeuko huo umesababisha kuendelea kuzisawiri tamaduni za kigeni ambazo zimekuja na utandawazi katika riwaya ya Kiswahili ambazo hazioneshi utamaduni wa Waswahili. Utamaduni wa Kimagharibi unaonekana kuwa bora kuliko utamaduni asilia uliopo katika jamii ya Waswahili. Nadharia ya Ubaada Ukoloni msingi wa utabaka unashadidia jambo hili kwa kuonesha waandishi wanavyothamini usasa katika kazi zao. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* mwandishi anaonesha jinsi Kabula alivyopambwa kwa kuwekwa dawa kwenye nywele, nyusi kutindwa, kope kunyoshwa na midomo yake kupakwa rangi. Haya ni baadhi ya mambo ambayo yameletwa katika kipindi cha utandawazi ambayo yanaendelea kuimarishwa na kukita mizizi kwenye utamaduni wa Waswahili na katika riwaya ya Kiswahili. Katika mahojiano ya uwandani, Kihongosi (ktj) anasema:

> Wazungu wanahitaji kusoma utamaduni wa Waswahili katika kazi zao ili kujua utamaduni wao. Baadhi ya riwaya za Kiswahili zimeweka Umagharibi katika masuala ya mavazi, milo na vinywaji, dini, ndoa na lugha. Utamaduni wa Kimagharibi unaendelea kuimarika katika jamii kupitia riwaya zinazoandikwa katika kipindi cha utandawazi. Jambo hili ni la ajabu kwani riwaya ya Kiswahili inasawiri Umagharibi zaidi kuliko utamaduni wa Waswahili (Utafiti, 2022).

Dondoo hili linaonesha jinsi baadhi ya waandishi wa riwaya ya Kiswahili wanavyoweka Umagharibi katika riwaya zao, na kutokuwako utofauti kati ya riwaya ya Kiswahili na riwaya kutoka nchi nyingine. Utamaduni wa Kimagharibi unaendelea kuimarika siku hadi siku katika riwaya zinazoandikwa kutoka Afrika. Jambo hili linasababisha kumwona mzungu katika riwaya ya Kiswahili kuliko Waswahili.

4.5.2.6 Mmomonyoko wa Maadili katika Jamii

Maadili katika kipindi hiki cha utandawazi yameharibika katika jamii kutokana na kuiga kila jambo kutoka katika utamaduni wa kigeni na kuona ndio usasa. Baadhi ya waandishi wa riwaya ya Kiswahili wanaandika kwa kuiga mambo mapya ambayo hayana tija katika jamii zao. Imebainika kuwa vijana wanaiga mambo ambayo hayafai yanayopatikana katika kazi za kifasihi na kuyashikilia. Jambo hili linasababisha mmomonyoko wa maadili katika jamii. Kwa mfano, katika suala la mavazi, maadili na lugha mambo haya yamebeba sura ya Kimagharibi katika riwaya teule. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* mwandishi amemtumia Kabula aliyekuwa akivaa nguo fupi zilizokuwa zinaacha wazi maungo ya mwili na kusababisha ajali za barabarani. Imeelezwa na nadharia ya Ubaada Ukoloni kuwa nchi zilizotawaliwa zina mwingiliano wa kiutamaduni katika masuala mbalimbali yakiwamo mavazi. Hivyo, vijana wanapoiga mavazi haya wanakiuka maadili yaliyopo katika jamii yao kwa kuiga mitindo mipya iliyoletwa na utandawazi. Katika mahojiano ya uwandani na Feruzi (ktj), suala hili linadhihirika anaposema:

> Kiukweli baadhi ya riwaya za kipindi cha utandawazi zinakiuka suala la maadili katika jamii. Riwaya ambazo zinatumika kufundishia wanafunzi katika shule za sekondari kuna maneno ambayo wanafunzi wakiyafikia kusoma yanakuwa yanamvua nguo mwalimu. Darasa linakuwa halina usikivu, kiukweli waandishi wanatumia maneno ambayo yanakwenda kinyume na utamaduni wa Waswahili (Utafiti, 2022).

Dondoo hili linaonesha jinsi baadhi ya waandishi wa riwaya ya Kiswahili wanavyokengeuka katika utamaduni wa Waswahili kwa kutumia maneno ambayo kwa wanafunzi wa umri mdogo inakuwa tatizo kuyatumia. Maadili yanaendelea kumomonyoka kutokana na riwaya kuendeleza mkengeuko. Katika riwaya ya Kiswahili, wanafunzi wanajifunza masuala ambayo hawakutakiwa kujifunza kwa umri wao. Kiplang'at (2009) anafafanua zaidi kwa kusema:

> "Utandawazi ni kikwazo kikubwa cha nyimbo jadi au asili kubadilika. Jamii za Afrika zimejikita kufuata mila na desturi za Kimagharibi wakiamini ndio ustaarabu lakini hali hii imepelekea kuwa na utamaduni mseto na kupelekea utamaduni ubadilike jambo hili linapelekea kumomonyoka kwa maadili'' (uk. 8).

Nukuu hii inaonesha namna utandawazi unavyopoteza maadili ya jamii ya Waswahili kwa kuonesha kuwa kushabihiana na Umagharibi ndio usasa. Nyimbo za asili zilizokuwa na mafunzo mbalimbali zinapotea na kuingiza nyimbo za kigeni ambazo zinaonyesha zaidi masuala ya Kimagharibi. Utamaduni mseto unabadilisha mambo mengi katika jamii ambapo utamaduni wa jamii unabadilika na kuingia katika mmomonyoko.

4.5.2.7 Kupotea kwa Utambulisho Kupitia Utamaduni wa Waswahili

Kutokana na mwingiliano wa utamaduni uliopo kati ya nchi za Kiafrika na Kimagharibi kumesababisha Waswahili kutojulikana kupitia utamaduni wao kutokana na mseto wa utamaduni unaopatikana katika maisha ya jamii ya Waswahili. Waandishi wa riwaya wanapoandika kazi za riwaya kwa kuchanganya tamaduni mbalimbali zinazopatikana katika jamii, inafanya utamaduni wa Waswahili kutojulikana. Utafiti umebaini kuwa, Waswahili wanashindwa kutambulika kupitia mavazi, dini, sanaa, maadili na lugha zao jambo ambalo linaathiri maisha ya Waswahili. Imebainika kuwa, riwaya teule za awali zimetambulisha utamaduni huo kwa namna watu wanavyokuwa wanaishi katika jamii zao. Baadhi ya riwaya za sasa zinapoteza asili ya utamaduni wa Waswahili uliokuwapo katika jamii. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* mwandishi amesawiri dini za Kimagharibi ambavyo zinakiuka misingi ya kimaadili iliyokuwapo katika jamii. Mwandishi anaonesha mauaji yanavyofanyika katika kanisa kupitia mhusika Rais Gabriel aliyekuwa anahamasisha jambo hilo. Pia, makanisa yanafungisha ndoa mara mbili, mambo ambayo hayafungamani na utamaduni wa Waswahili. Hivyo, watu

wanapotaka kuwatambua Waswahili kupitia utamaduni wao wanashindwa kutokana na Umagharibi ulioingia katika maisha yao. Hoja hii inashadidiwa na nadharia ya Ubaada Ukoloni katika msingi wa utamaduni mseto ambapo utamaduni asilia wa Waswahili hauonekani. Hali hii imesababisha kutotambulika kwa utamaduni asili wa Waswahili kuwa ni upi kutokana na jamii kuendelea kupoteza utambulisho wake kupitia kazi za fasihi zikiwamo riwaya. Mwandishi wa riwaya ya Kiswahili anapokuwa anaandika kwa kutumia lugha ambayo si ya jamii yake inasababisha lugha inayotambulisha jamii husika kuendelea kupoteza ubora katika riwaya ambazo zinaongea masuala yanayowahusu Waswahili. Kupoteza utambulisho wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili kuna athari kwa jamii na vizazi vijavyo.

4.5.2.8 Kupoteza Mvuto wa Kiujumi wa Kiafrika

Riwaya ya Kiswahili kabla ya utandawazi ilikuwa na mvuto mkubwa kwa jamii kutokana na kubeba mafunzo mazito yaliyoijenga jamii katika mwelekeo wa maadili yaliyopatikana katika utamaduni wa jamii husika. Baadhi ya riwaya za sasa zimepoteza mvuto kutokana na kukithiri kwa tamaduni za kigeni katika kazi hizo ambazo huhifadhiwa kwa ajili ya vizazi vijavyo. Imebainika kwamba, jamii inaendelea kujifunza mambo ya Kimagharibi kupitia riwaya hizo jambo ambalo linaendelea kuitenga jamii na utamaduni wake. Matokeo yanaonesha kuwa utamaduni wa Waswahili katika riwaya unapotea kwa jina la utandawazi. Riwaya iliyopaswa kutangaza Waswahili ni akina nani, inatangaza utamaduni mseto uliopo katika jamii. Riwaya ya Kiswahili inakosa mvuto katika jamii ya Waswahili kutokana na kutosawiri ujumi wa asili ya Kiafrika. Kwa mujibu wa nadharia ya Ubaada Ukoloni msingi wa mwingiliano wa kiutamaduni, athari zilizoachwa na wageni katika maisha ya Waswahili ni kubwa. Taathira hizi zimeenea mpaka katika riwaya ya Kiswahili kuwa inasawiri Umagharibi. Katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu*, mwandishi amesawiri masuala ya mauaji ya kutumia silaha kama jambo la kawaida ambapo katika jamii ya Waswahili masuala ya mauaji hayasisitizwi kwa kuwa yanakiuka maadili ya jamii. Masuala kama hayo yanatokea zaidi katika nchi za kizungu. Kusawiriwa kwake katika riwaya ya Kiswahili, kunasababisha yakose uhalisia wa moja kwa moja katika jamii. Riwaya ya Kiswahili inapoteza mvuto kwa kuandika masuala ambayo yanavuka mipaka ya kiulimwengu na kukosa uhalisia katika jamii. Hivyo, mvuto uliokuwapo katika riwaya za awali unapotea kutokana na

kukosa uzalendo wa tamaduni zao. Katika mahojiano ya uwandani, Kasoga (ktj) anaelezea:

> Tunapokuwa tunasoma kazi za kifasihi ambazo zimeandikwa kwa ajili ya jamii ya Waswahili, tunatarajia kupata elimu ambayo iko katika kazi za kifasihi na kutupa mwangaza kuhusiana na jinsi ya kuendeleza utamaduni wa Waswahili. Hali inapokuwa mbaya, riwaya zinachanganya utamaduni, hivyo zinapoteza mvuto. Riwaya ambazo zinafundishia shule za sekondari zimetumia lugha ya wazi ambayo kwa kiasi kikubwa lugha hiyo haifai kwa watoto. Hivyo, kazi za riwaya zinakuwa na mvuto hasi kwa jamii ambayo inafuata utaratibu wa kimaadili uliopo katika maisha ya Waswahili (Utafiti, 2022).

Kutokana na maelezo hayo, inaonesha wazi kuwa riwaya ya Kiswahili katika zama hizi za utandawazi inapoteza mvuto kwa kuandika masuala ya kigeni kuliko kuandika masuala ya utamaduni wa jamii ya Waswahili. Mambo haya yanapelekea jamii kuendelea kubadilika siku hadi siku na kuacha utamaduni ambao ndio msingi wa maisha ya Waswahili.

4.6 Muhtasari wa Sura ya Nne

Katika sura hii tumewasilisha matokeo ya utafiti kwa kuzingatia malengo mahususi ya Utafiti. Sehemu ya kwanza, ilibainisha vipengele vya utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule pamoja na uamilifu ambavyo ni lugha, ndoa, mavazi, kifo, milo na vinywaji, dini na sanaa. Pili, namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili ulivyojitokeza katika riwaya teule kupitia vipengele vya utamaduni vilivyobainishwa katika lengo la kwanza. Tatu, sehemu hii imetathimini athari chanya na hasi za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili. Athari chanya zilizobainishwa ni kama vile, kuleta upya, kuenea kwa utamaduni wa kigeni, kupanua hadhira, kuongezeka kwa waandishi na kuongezeka kwa maarifa mapya. Pia, utafiti huu ulibainisha athari hasi kama vile, kuharibu historia ya utamaduni wa Waswahili, kupoteza mvuto wa riwaya ya Kiswahili, kuimarisha utamaduni wa kigeni katika riwaya, kupoteza thamani ya lugha ya Kiswahili, mmomonyoko wa maadili katika jamii na kupoteza utambulisho wa utamaduni wa Waswahili. Sura inayofuata inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia muhtasari wa tasnifu, hitimisho na mapendekezo. Hivyo, sura hii inaundwa na sehemu tano ambazo ni utoshelevu wa nadharia zilizotumika, mchango mpya wa utafiti huu, mapendekezo ya utafiti huu, mapendekezo kuhusu tafiti zijazo pamoja na muhtasari wa sura ya tano.

5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii imechunguza mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili Zama za utandawazi. Utafiti huu ulikuwa na jumla ya malengo mahususi matatu ambayo ni: kubainisha vipengele vya utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili kabla ya zama za utandawazi, kufafanua namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya teule ya Kiswahili zama za utandawazi na kutathimini athari za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule.

Tasnifu hii imegawanyika katika sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi ambao umefafanua istilahi na dhana muhimu zilizotumika katika utafiti huu: Istilahi na dhana hizo ni riwaya, riwaya ya Kiswahili, Waswahili, mkengeuko, utamaduni na utandawazi. Aidha, sura hii imefafanua kuhusu usuli wa tatizo la utafiti, tamko la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mawanda ya utafiti .

Sura ya pili imefafanua mapitio ya maandiko yanayoendana na mada husika na kubainisha mapengo yaliyozibwa na utafiti huu. Maandiko hayo yalihusu riwaya, utamaduni na utandawazi. Aidha, sehemu hii imebainisha nadharia zilizotumika kuongoza utafiti huu. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya Sosholojia, iliyotumika kufanikisha lengo la kwanza na nadharia ya Ubaada Ukoloni iliyotumika katika lengo la pili na la tatu.

Sura ya tatu ni methodolojia ya utafiti ambayo imefafanua vipengele ambavyo ni usanifu wa utafiti, mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, pamoja na njia na zana za kukusanyia data. Vipengele vingine ni uchanganuzi wa data,

uzingatizi wa maadili ya utafiti, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti na changamoto za utafiti huu na jinsi zilivyotatuliwa.

Sura ya nne imejikita katika kuwasilisha mjadala wa matokeo kuhusu mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili Zama za utandawazi. Sura hii imegawanywa katika sehemu kuu tatu kulingana na malengo ya utafiti: Sehemu ya kwanza imejikita katika kubainisha vipengele vya utamaduni wa Waswahili vilivyokuwapo katika riwaya ya kabla ya utandawazi ya *Mirathi ya Hatari* na *Kurwa na Doto.* Vipengele vilivyobainishwa ni lugha, ndoa, milo na vinywaji, imani za kidini, mavazi na kifo. Sehemu ya pili, imechunguza namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi. Utafiti umebaini kuwa, vipengele vilivyopo katika utamaduni wa Waswahili vimekengeuka. Navyo ni ndoa, lugha, maadili, imani za kidini, kifo na mavazi. Sehemu ya tatu, imejikita katika kutathimini athari chanya na hasi za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule ya Kiswahili. Athari chanya zilizobainishwa ni kama vile, kuleta upya, kuenea kwa utamaduni wa kigeni, kupanua hadhira, kuongezeka kwa waandishi na kuongezeka kwa maarifa mapya. Pia, utafiti huu ulibainisha athari hasi kama vile, kuharibu historia ya utamaduni wa Waswahili, kupoteza mvuto wa riwaya ya Kiswahili, kuimarisha utamaduni wa kigeni katika riwaya, kupoteza thamani ya lugha ya Kiswahili, mmomonyoko wa maadili katika jamii na kupoteza utambulisho wa utamaduni wa Waswahili.

Sura ya tano inahusiana na muhtasari, hitimisho na mapendekezo. Katika sura hii, muhtasari wa tasnifu umefafanuliwa kwa kila sura. Pia, hitimisho la tasnifu limetolewa kwa kuzingatia utoshelevu wa nadharia zilizotumika na mchango mpya wa tasnifu hii. Aidha, sura hii imetoa mapendekezo mbalimbali.

5.3 Hitimisho la Tasnifu

Sehemu hii imegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni utoshelevu wa nadharia zilizoongoza utafiti na mchango mpya wa utafiti.

5.3.1 Utoshelevu wa Nadharia Zilizotumika

Nadharia zilizoongoza utafiti huu ni mbili ambazo ni: Nadharia ya Sosholojia na nadharia ya Ubaada Ukoloni. Nadharia ya Sosholojia kupitia misingi mbalimbali

kama vile, umahususi wa jamii, fasihi haitoki katika ombwe na mhakiki wa kazi za fasihi kuhakiki kwa kuzingatia muktadha anaotoka mwandishi, imeweza kufikia na kufanikisha lengo la kwanza la kubainisha vipengele vya utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule ya Kiswahili ya zama za kabla ya utandawazi. Kutokana na misingi hiyo kuathiriana na lengo hilo na kutoa matokeo yenye tija. Pia, nadharia ya Ubaada Ukoloni ilitumika katika lengo la namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya ya Kiswahili ya zama za utandawazi na kutathimini athari za mkengeuko wa utamaduni katika riwaya teule ya Kiswahili. Nadharia hii kupitia misingi kadha wa kadha kama vile matumizi ya lugha ya Kiingereza ni kuendeleza ukoloni mamboleo, utabaka, na mwingiliano wa utamaduni imesaidia kufikia kile kilichokusudiwa katika malengo hayo na kutoa matokeo thabiti na bora. Hivyo, nadharia zote mbili zimekamilishana na kutosheleza malengo ya utafiti uliofanyika na kutoa matokeo yaliyokusudiwa katika utafiti huu.

5.3.2 Mchango Mpya wa Utafiti Huu

Utafiti umeibua maarifa mapya kuwa riwaya ya Kiswahili ya zama za utandawazi ni wakala mmoja wapo wa kueneza utamaduni wa Kimagharibi. Kutokana na mkengeuko wa utamaduni kubebwa katika riwaya ya Kiswahili ya zama za utandawazi, utafiti huu umesaidia wasomaji kuelewa namna riwaya inavyokuwa wakala wa kusambaza utamaduni wa kigeni kutokana na athari za utandawazi.

Sambamba na hilo, utafiti huu umetumia riwaya za kabla ya utandawazi na zile za baada ya utandawazi hali ambayo inafanya utafiti huu ubebe sura ya ulinganishi hivyo kuwa halisi zaidi na halali kwa sababu msomaji anaweza kuona mabadiliko ya wazi kadri miaka inavyopita na jamii inavyobadilika.

5.4 Mapendekezo

Kutokana na utafiti uliofanyika mapendekezo yamegawanywa katika sehemu mbili. Kwanza, mapendekezo ya utafiti huu kwa wadau mbalimbali na pili, mapendekezo kuhusu tafiti zijazo.

5.4.1 Mapendekezo ya Utafiti Huu kwa Wadau Mbalimbali

Katika kuhakikisha utamaduni wa jamii ya Waswahili unadumishwa na kuthaminiwa, utafiti huu umetoa mapendekezo kwa wadau mbalimbali kama ifuatavyo:

Mosi, waandishi wa riwaya katika kipindi cha utandawazi watumie lugha ya staha wanapokuwa wanaandika riwaya, jambo hili litasaidia kuzuia mmomonyoko wa maadili kwa vijana.

Vilevile, waandishi watumie utandawazi kukuza na kutangaza utamaduni wa Waswahili katika riwaya. Hii itasaidia utamaduni wa Waswahili kuendelea kujulikana na kuthaminiwa katika kipindi cha utandawazi.

Pili, maafisa utamaduni wanapaswa kutoa elimu kwa jamii kuhusu namna ya kukabiliana na changamoto za utandawazi katika utamaduni wa Waswahili. Hii itasaidia jamii kuona thamani ya utamaduni wao katika kipindi cha utandawazi.

5.4.2 Mapendekezo Kuhusu Tafiti Zijazo

Utafiti huu umechunguza mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi. Matokeo ya utafiti yamekusudia kuziba mapengo ya utafiti yaliyokusudiwa lakini bado kuna uhitaji wa kufanyika kwa tafiti zaidi kuhusu mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili kama ifuatavyo:

Mosi, ufanyike utafiti kuhusu mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika tanzu nyingine za fasihi andishi kama tamthiliya na ushairi. Hii itasaidia kuangalia namna tanzu nyingine za fasihi andishi zilivyosawiri mkengeuko wa utamaduni katika kipindi cha utandawazi. Hivyo, kupanua maarifa zaidi kuhusu mkengeuko wa utamaduni katika tanzu nyingine.

Pili, kufanyike utafiti kuhusu ulinganisho na utofauti wa masuala ya kitamaduni katika riwaya ya mwaka 1970 kurudi nyuma na zile zilizoandikwa miaka ya 1990 mpaka sasa, hii itasaidia kujua jinsi masuala ya utamaduni yanavyofanana na kubadilika katika riwaya hizo.

5.5 Muhtasari wa Sura ya Tano

Sura hii imeeleza kuhusu muhtasari, hitimisho na mapendekezo. Katika muhtasari, sura imechambua kwa kina muhtasari wa tasnifu yote kuanzia sura ya kwanza mpaka sura ya tano. Sehemu ya hitimisho imeshughulikia vipengele viwili ambavyo ni utoshelevu wa nadharia zilizotumika pamoja na mchango mpya wa tasnifu hii. Sehemu ya mwisho ni mapendekezo ambapo mtafiti ametoa mapendekezo katika nyanja mbalimbali pamoja na mapendekezo kwa tafiti zijazo.

MAREJELEO

Ajayi, D. (2003). "Globalization, Social Sciences and Nigeria in The 21st Century". Nigeria Social Scientist. 4.(1). 12-56.

Akpa, A. E. (2002). "The Dynamic of Music and Culture in Traditional Ibibio Society of Nigeria". *An International Multidisciplinary Journal*. 6.(2).

Alderson, G. G. & Beretta, A. (1992). *Evaluating Second Education*: Cambridge applied linguistic, C.U.P.

Arowolo, D. (2010). "Effect of Western Civilization and Culture on Africa". Katika *Afro Asian Journal of Social Sciences*. 1.No1 Quarter IV (Pg 2-22).

Awolalu, J.O. (1976). *What is African Tradition Religion?. Studies in Comparaetive Religion*. 10 (2), 1-10.

Babbie, E. (1992). *The Practice of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Bakari, S. H. (2009). "Mchango wa Maneno katika Kanga katika Kukuza Utamaduni wa Waswahili". Ripoti ya Utafiti. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro.

Beerkens, E. (2006). Globalization. Definitions and Perspectives. *Journal of Political Science*.

Beja, S. K. (1988). "Maudhui ya Ujamaa katika Riwaya za Tanzania*"*. Tasinifu ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Chachage, C. S. L. (2010). *Almasi za Bandia*. Nairobi-Kenya: Vide Muwa Publishers L.t.d

Chiraghdin, S. & Mnyampala, M. (1973) *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Chuachua, R. (2016). “Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu”. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Creswell, J. W. (2007. *Qualitative Inquiry Research Design*: Choosing Among Five Approaches. Thousand Oaks. California: SAGE Publications.

Daramola, I. & Oyinade, B. (2015). “Impact of Culture Globalization on Africa: The Role of Western Media”. *International Journal of Educational Research*. 3. No 3.

Darwson, C. (2002) *Practical Research Methods*: A User Friendly Guide to Mastering Research Technique and Projects. Oxford: How to Book Ltd.

Fafunwa, A. B. (1978). *History of Education in Nigeria*. London: George Allen and Unwin.

Farsy, M. S. (1960). *Kurwa na Doto*. Maelezo ya Makazi katika Kijiji cha Unguja. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Faustine, S. (2017). “Falsafa ya Waafrika na Ujenzi wa Mtindo wa Uhalisia ajabu katika Riwaya ya Kiswahili”. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Galtung, J. (1980). “The True Worlds. A Trans national Perspective”. New York: The Free Press: P.130.

Geertz, C. (1973). *The Interpretation of Cultures*. New York: Basic Books. Inc. Publishers.

Hart, S. M. (2003). “Magical Realism in the Americas: Politicalized Ghosts in One Hundred Years of Solitude. The House of Spirits and Beloved”. *Journal of Liberian and Latin American* Studies 9/2: 115-123.

Isack, Z. K. (2020). *Utamaduni wa Kiswahili Juu ya Mambo yahusuyo Dini, Chakula na Desturi za Mavazi*. Osaka University Knowledge Archieve: Text Version Publishers.

Jean T. (2002). *The Hidden Dimension of Globalization*.What is at stake geoculturally? Global Policy Forum. New York: ATTAC May 29.

John, B. N. (2018). "Usawiri wa Utamaduni wa Hadhira Lengwa katika Riwaya zilizotafsiriwa kwa Kiswahili": Mifano kutoka *Barua Ndefu kama Hii.* Tasinifu Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Jumanne, A (2016). "Mabadiliko ya vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya Kiswahili: Ulinganisho wa riwaya za Shaaban Robert na Said A. Mohamed". Tasinifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kalegeya, T. (2013). "Utandawazi na Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi kifani wa *Makuadi wa Soko Huria na Almasi za Bandia"*. Tasinifu ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kamusi kuu ya Kiswahili (2016). Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004). Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Kevogo, A. U. (2018). Taswira ya Utandawazi Katika Riwaya Mpya ya Kiswahili*:* Mfano wa Riwaya ya *Dunia Yao*. *Katika kioo cha Lugha*. Juz (5). Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Khamis, S. (1980). Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili. *Katika kioo cha Lugha no. (5).* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo kikuu Dar es Salaam.

Khamis, S. (2007). The Swahili Novelist at the Crossroads: The Dilemma of identity and Fecundity. Swahili Forum 14:165-180

Khamis, S. (2007). Utandawazi au Utandawizi? Jinsi Lugha ya Riwaya Mpya ya Kiswahili inavyodai. *Katika Mulika Juzuu ya 70.* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimu Jamii.* Taasisi ya Taaluma za Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kiplang'at . J. & Lagat. C. (2009). Kenya National Heritage: Music and Culture. A research report. Moi University.

Kothari, C. R. (2009). *Research Methodology: Methods and Techniques* (2nd Revised Edt). New Delhi: New Age International Publishers Ltd.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology*: Methods and Technique. New Delhi: Wiley Eastern.

Libui, O. S. (2012). "Riwaya Mpya ya Kiswahili na Masuluhisho ya Changamoto za Utandawazi".Tasnifu ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Little, A. W. (1996). Globalization and Educational Research Whose Counts?. *In International Journal of Development*. 16(4). Pg-427-438.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili*: *Historia na Misingi ya Uchambuzi.* Nairobi: Sitima Printer and Stations L.t.d

Maitaria, N. (2012). *Mwongozo wa Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Masebo, J. A. & Nyangwine, N. (2007). *Nadharia ya lugha*: Kiswahili kidato cha 5 & 6. Dar es salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Masingele, L. (2012*). "*Mabadiliko ya Riwaya ya Kiswahili Kidhamira kuanzia mwaka 1970-2011". Tasnifu kwa ajili ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Massamba D.P.B. (2002) *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mayaka, G. (2012). “Ukengeushi wa Wahusika Wasomi Katika Riwaya za Kezilahabi”. Tasnifu hii imetolewa kutosheleza mahitaji ya Master of Arts: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mazingwa, S. A. (1991). *Fasihi ya Kiswahili*. Ndonda Peramiho: Benedictine Publishing company.

Mazrui, A. A. (1982). Africa Between Nationalism and Nationhood: A political Survey: University of Michigan. 13, (*1*).

Mbaabu, I. (1985). *Utamaduni wa Waswahili*. Nairobi: Kenya Publishing and Marketing.

Mbiti, J. S. (1970). *Concepts of God in Africa*. London: S.P.C.K.

Mbiti, J. S. (2011). *African Religion and Philosophy*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mcleod, R. & Noble, J. (2016). *Listen and Learn*: How Charitises can use Qualitative Research. Paper Presented at NPC.

Mlacha, S. A. K (1996). Utamaduni wa Mwafrika katika Riwaya ya Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka. *Katika Mulika namba* 23. Dar es Salaam: TUKI, kur 24-35.

Mlacha, S. A. K. (1991). *A Linguistic Study of the Novel.* Berlin: Schreiber.

Mlacha, S. A. K & Madumulla, J. S. (1991). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mligo, E. S. (2012) .*Jifunze Utafiti: Mwongozo kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti yenye Mantiki.* Dar es Salaam: Ecumenical Gathering

Momanyi, C. (1998). “Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili”. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Muhando, P. & Balisidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House (TPH).

Mulokozi, M. M. (1985). The Present State of Swahili Literature: A Survey. *African Literature Studies. The Present State / L'état present*, 171-188.

Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi.* Mulika Juz 21. kur. 1-24.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*: Dar es Salaam: TUKI

Mung'ong'o, C. G. (1977).*Mirathi ya Hatari.* Dar es salam: Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

Munyoki, J. (2015). "Familia za Kiafrika katika Njia Panda: Mitagusano na Changamoto za Usasa katika Mhanga Nafsi Yanga ya S.A. Mohammed". Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili. (Haijachapishwa).Chuo Kikuu cha Nairobi.

Murithi, J. J & wengine (2018). "Itikadi katika Riwaya ya Dunia yao na Mhanga Nafsi Yangu za S.A Mohamed". *Journal of Humanities and Social Science.* 23. Issue 9.

Mwagosi, A. & wenzake (2020). "Kuchunguza namna Utandawazi Unavyoakisiwa katika Fasihi ya Kiswahili". *Ruaha Journal of Arts and Social Science*. Volume 6, Issue 2.

Mwansasu, J. (2005). *Confronting New Realities: Reflections on Tanzania Radical Transformation*. Dar es Salaam University Press.

Ndungo, W. C. & Mwai, R. (1991). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili*. Nairobi: Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi-Kenya. Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. & Chimerah, R. (2008) *Ufundishaji wa Fasihi*: Nadharia na Mbinu. Nairobi: The Jomo Kenyata Foundation

Nkwera F. M. V (1978). *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo*: Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi ya Fasihi*. Augustina College. Rock Island, IL 61201.

Nyonje, J. W. (2006). *Mwono Ulimwengu wa Waswahili*. Nairobi: University of Nairobi Press.

Ogbum, W. F. (1922). *Social Change with Respect to Culture and Original Nature*. New York: B.W. Huebsch

Omer, R. (2017) The Modern and The Traditional: African Women and Colonity Morality. *Inquiries Journal*, 9(10). Available at: http://www.inquiries journal.com/a ? id =1655.

Oni, A. A. (2005). Globalization and Its implications on Africa Culture and Development: Challenges for Education. *International Journal of African and African American Studies* 4(2).

Ponera, A. S. (2010). "Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert: Maana yake, Sababu za Kutumiwa na Athari zake Kwa Wasomaji". Tasinifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Ponera, A. S. (2015). "Misemo ya Kwenye Magari kama Nyenzo ya Mawasiliano". *Katika Journal of Humanities*. Chuo Kikuu cha Dodoma. Tol.2 (1) Uk 21-28.

Ponera, A. S. (2019) *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Ramadhani, S. K. (2013) "Usawiri wa Mwanamke Katika Taarab ya Mipasho"*: Mfano Kutoka Nyimbo za Mzee Yussuf Mzee. Tasinifu ya M.A. Kiswahili.* (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.Tanzania.

Said, E. (1978). *Orientation*. United States: Patheon Books Publisher

Samwel, M. (2015).*Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili*: Mwongozo kwa Mwanafunzi na Mwalimu wa Fasihi Simulizi na Andishi. Dar es Salaam:Meveli Publishers.

Sanga, A. N. (2018). "Mkengeuko wa Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi fupi Andishi za Kiswahili Kipindi cha Utandawazi": Mifano kutoka Magazeti ya Habari leo na Nipashe na Mwananchi. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Sankan, S. S. (2006). *The Maasai*. Nairobi: KLB

Sawe, A. (2018). "Usawiri wa Mwanamke katika Ndoa. Mifano kutoka katika Utenzi wa Mwanakupona, Utenzi wa Ayubu na Matini teule za Kidini". Tasinifu ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha MOI.

Selemani, O. (2012). "Riwaya Mpya ya Kiswahili na Masuluhisho ya Changamoto za Utandawazi". Tasinifu ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Sengo, T. S. Y. (1995). Itikadi katika Jamii za Kiswahili. Katika Lugha, Utamaduni na Fasihi. Dar es Salaam: TUKI, kur 79-87.

Sengo, T.S.Y. (1992). *Utamaduni wa Kiswahili* . Wilaya ya Kusini – Unguja. Katika Nordic *Journal of African Studies* 1(1): 53-79

Senkoro, F. E. M. K. (1977). "Riwaya ya Kiswahili na Maendeleo ya Umma". Tasinifu ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Senkoro, F. E. M. K. (1984). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (1988) *Mediocrity and Cretivity in Swahili Literature*: London. James Carrey Publishers.

Shigongo, E. J. (2003). *Rais Anampenda Mke Wangu*. India: Global Publishers & General Enterprises LTD.

Suakei, S. (2013). “Usasa na Mwanamke wa Kisasa katika Nyuso za Mwanamke ya S. A. Mohammed”. Kenya: University of Nairobi Publishers.

Temples, P. (1959) *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.

TUKI, (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ussi. J. U. (2015). “Suala la Utendaji katika Michezo Jadi ya Watoto. Mifano kutoka Bumbwini Zanzibar”. Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa*)*. Chuo Kikuu cha Dodoma.

Wa thiong’o, N. (1986) *Decolonizing the Mind*. The Politics of Language in African Literature. Nairobi: Heinemann Educational Books.

Wade, A. (1997). *Globalization and Its Limits*. Washington D.C: Brooking Institution Press.

Walters, M. (1995).*Globalization. London:* Routledges and Kegan Paul.

Wamitila K. W. (2003) *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books Publishers.

Wilfred, F. (1997). Globalization and Cultures*: The Other Voice in Bulletin of Ecumenical Theology* .9 (1 – 2).

Yakubu, N. (1999). Millenium and Globalization. What is in it for us*? Crystal International News Magazine*: Abuja Heritage pp. 35.

Yin, R. K. (2011) *Qualitative Research from Star to Finish*. New York: The Guilfor Press.

Mbele, J. (2020). Utamaduni na Utandawazi. Iliyosomwa tarehe 15/1/2020 katika https://issamichuzi.blogspot.com/2020/01/utamaduni-na-utandawazi-na-profesa.html

VIAMBATISHO

Sehemu hii imejumuisha miongozo ya ukusanyaji data, majina ya watafitiwa na vibali vya ruhusa kwa ajili ya utafiti.

Kiambatanisho A: Miongozo ya Ukusanyaji Data

Kiambatisho A 1: Miongozo ya Usaili kwa Watafitiwa

Mwongozo wa Usaili kwa Wanafunzi wa Mwaka wa Tatu wa fasihi ya Kiswahili

Jina langu ni Debora Babilas Masimo, mwanafunzi wa Shahada ya Umahiri katika fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Ninafanya utafiti kuhusu "**Mkengeuko wa Utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za Utandawazi: Mifano kutoka Riwaya Teule**: Lengo kuu ni kuchunguza namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi. Kabla ya kuanza, naomba kukujulisha kuwa taarifa utakazotoa kwa mtafiti zitatumika kwa malengo ya utafiti huu na si vinginevyo. Tafadhali, naomba ushirikiano wako katika usaili huu:

1. Je unafahamu nini kuhusu utamaduni wa Waswahili ?
2. Je**,** unadhani ni vipengele gani vinaunda utamaduni wa Waswahili ?
3. Je, katika riwaya ya *Kurwa na Doto na Mirathi ya Hatari* vipengele vya kiutamaduni vimesawiriwaje?
4. Je, unafikiri ni vipengele gani vya utamaduni wa Waswahili vilivyokengeuka katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke wangu* na *Almasi* za *Bandia* ?
5. Je nini athari za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule?
6. Kwa maoni yako unafikiri nini kifanyike kuhakikisha utamaduni wa Waswahili unasawiriwa katika riwaya zinazoandikwa katika zama za utandawazi?

Mwongozo wa Usaili kwa Wahadhiri wa fasihi ya Kiswahili

Jina langu ni Debora Babilas Masimo, mwanafunzi wa Shahada ya Umahiri katika fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Ninafanya utafiti kuhusu " **Mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi. Mifano kutoka riwaya teule"**. Lengo kuu ni kuchunguza mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi. Kabla

ya kuanza naomba kukujulisha taarifa utakazozitoa kwa mtafiti zitatumika kwa lengo la utafiti huu tu. Tafadhali, naomba ushirikiano wako katika usaili huu:

1. Je, unaelewa nini kuhusu mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili?
2. Je, vipengele gani vinaunda katika utamaduni wa Waswahili?
3. Je unafikiri ni vipengele gani vya utamaduni wa Waswahili vilivyokengeuka katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* na *Almasi za Bandia* ? Kivipi ?
4. Je, unafikiri kuna athari gani za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule ya Kiswahili ?
5. Kwa maoni yako unafikiri nini kifanyike kuweza kuhifadhi utamaduni katika riwaya ya Kiswahili ya zama za utandawazi?

Mwongozo wa Usaili kwa Wanafunzi wa Umahiri katika fasihi ya Kiswahili

Jina langu ni Debora Babilas Masimo, mwanafunzi wa Shahada ya Umahiri katika fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Ninafanya utafiti kuhusu "**Mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za Utandawazi".** Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule ya Kiswahili zama za utandawazi. Kabla ya kuanza naomba kukujulisha taarifa utakazozitoa kwa mtafiti zitatumika kwa lengo la utafiti huu tu. Tafadhali, naomba ushirikiano wako katika usaili huu:

1. Je, katika riwaya ya *Kurwa na Doto* na *Mirathi ya Hatari* vipengele vya utamaduni wa Waswahili vimesawiriwaje ?
2. Je, mkengeuko wa utamaduni umejitokezaje katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu* na *Almasi za Bandia* ?
3. Je, kuna athari gani za mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili?
4. Je, una maoni gani kwa waandishi wa kitandawazi kuhusu kuandika riwaya zenye kuhifadhi utamaduni ?

Asante kwa ushirikiano wako.

Kiambatisho A 1: Mwongozo wa Uchanganuzi wa Matini

Katika sehemu hii mtafiti amechanganua vyanzo mbalimbali vya maarifa kuhusiana na mada iliyokuwa inafanyiwa utafiti. Matini zilizochanganuliwa ni kama zifuatazo:

Vyanzo vya maarifa	**Vipengele Vitakavyochanganuliwa**	**Lengo**
• Riwaya ya *Kurwa na Doto* na *Mirathi ya Hatari*	vipengele vya utamaduni wa Waswahili	Kubainisha vipengele vya utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili.
• Riwaya ya *Almasi za Bandia* na *Rais Anampenda Mke wangu*	Mkengeuko katika vipengele vya utamaduni wa Waswahili katika riwaya teule ya Kiswahili	Kuangalia namna mkengeuko wa utamaduni wa Waswahili unavyojitokeza katika riwaya ya Kiswahili.

Kiambatanisho B: Orodha ya Watafitiwa Kutoka Chuo Kikuu Cha Dodoma-Idara ya Kiswahili

Na	JINA	CHEO	TAREHE YA MAHOJIANO	MAHALI
1	Dkt. STELLA FAUSTINE	Mhadhiri wa fasihi ya Kiswahili	29/6/2022	OFISINI
2	Dkt. ABDULMALICK FERUZI	Mhadhiri wa fasihi ya Kiswahili	8/6/2022	OFISINI
3	Dkt. TATU KHAMIS	Mhadhiri wa fasihi ya Kiswahili	17/6/2022	OFISINI
4	ARAFA JUMANNE	Mhadhiri Msaidizi wa fasihi ya Kiswahili	31/6/2022	OFISINI
5	NICE KASOGA	Mwanafunzi wa Shahada ya Umahiri katika fasihi ya Kiswahili	7/6/2022	CHSS
6	EVA ZABRON	Mwanafunzi wa Shahada ya Umahiri wa fasihi ya Kiswahili	18/5/2022	CHSS
7	GABRIELLA NCHIMBI	Mwanafunzi wa Shahada ya Umahiri wa fasihi ya Kiswahili	17/6/2022	CHSS
8	DANIEL NGAO	Mwanafunzi wa Shahada ya Awali wa fasihi ya Kiswahili	30/5/2022	VIBWETA CHSS
9	VELIMUNDA WIKUNGE	Mwanafunzi wa Shahada ya Awali wa fasihi ya Kiswahili	15/5/2022	CHSS
10	ELOI KIHONGOSI	Mwanafunzi wa Shahada ya Awali wa fasihi ya Kiswahili	17/5/2022	CBSL
11	EUNICE MABAWA	Mwanafunzi wa Shahada ya Awali wa fasihi ya Kiswahili	16/5/2022	CBSL
12	ASHA BAKARI	Mwanafunzi wa Shahada ya Awali katika fasihi ya Kiswahili	14/6/2022	CHSS

13	MAHOZA KIVUMI	Mwanafunzi wa Shahada ya Awali katika fasihi ya Kiswahili	3/6/2022	CHSS
14	OMARI ABASI	Mwanafunzi wa Shahada ya Awali katika fasihi ya Kiswahili	28/6/2022	CHSS
15	ALEXANDER ANDREA	Mwanafunzi wa Shahada ya Awali katika fasihi ya Kiswahili	1/6/2022	CBSL
16	MAXWELL LUCAS	Mwanafunzi wa Shahada ya Awali katika fasihi ya Kiswahilio	17/5/2022	CBSL
17	LUSIAN HAULE	Mwanafunzi wa Shahada ya Awali katika fasihi ya Kiswahili	30/5/2022	CBSL
18	SAFINA SHAABANI	Mwanafunzi wa Shahada ya Awali katika fasihi ya Kiswahili	25/5/2022	CHSS
19	TWALHA ABASI	Mwanafunzi wa Shahada ya Awali katika fasihi ya Kiswahili	19/5/2022	CHSS

Kiambatanisho C: Vibali vya Ruhusa vya Utafiti

THE UNIVERSITY OF DODOMA
OFFICE OF THE VICE CHANCELLOR

P.O. Box 259
Dodoma, Tanzania
Tel: +255 026 2310001 | Fax: +255 026 2323011
Email: vc@udom.ac.tz
Website: www.udom.ac.tz

Ref.No. MA.84/261/02/'A'/ 33 — 14th June, 2022

To: All Principals
Deans
Directors
The University of Dodoma

RE: REQUEST FOR RESEARCH CLEARANCE

The purpose of this letter is to introduce to you **Ms. Debora Babilas Masimo**, a student of the University of Dodoma who is required to conduct research. Our students undertake research activities as part of their study programs.

In accordance with Government circular letter Ref. No. MPEC/R/10/1 dated 4th July 1980; the Vice-Chancellor of the University can issue research clearances to staff members and students of the University on behalf of the Government and the Tanzania Commission for Science and Technology (COSTECH). I am pleased to inform you that I have granted a research clearance to **Ms. Debora Babilas Masimo.**

Therefore, I kindly request you to provide the assistance needed for her to conduct the research. Specifically, we request your permission for **Ms. Debora Babilas Masimo** to visit the University of Dodoma to meet and talk to relevant stakeholders in connection with her research.

The title of her research is **"Mkengeuko Wa Riwaya Ya Kiswahili Katika Utamaduni Wa Waswahili Zama Za Utandawazi: Mifano Kutoka Riwaya Teule."** Her research is from June to December 2022, and it will be conducted in Dodoma Region.

Should there be any restrictions, you are kindly requested to advise us accordingly. If you require further information, please do not hesitate to contact us through the Directorate of Research, Publications, and Consultancy. P.O Box 259, Dodoma.Tel. No. + (255) 262310301 Email:drpc@udom.ac.tz

Yours Sincerely,

Prof. Faustine K. Bee
VICE CHANCELLOR

THE UNIVERSITY OF DODOMA
P. O Box 259
DODOMA

THE UNIVERSITY OF DODOMA

OFFICE OF THE DEPUTY VICE CHANCELLOR-ARC

DIRECTORATE OF RESEARCH, PUBLICATIONS AND CONSULTANCY
P.O. Box 259
DODOMA, TANZANIA
TEL: +255-026-2310002 FAX: +255-026-2310012
EMAIL: dvcarc@udom.ac.tz;
Website address:www.udom.ac.tz

Ref. No. MA.84/261/02/ 23th June, 2022

To: Debora Babilas Masimo
The University of Dodoma

RE: REQUEST FOR ETHICAL CLEARANCE

The heading above is concerned,

The Institutional Research Review Ethics Committee (IRREC) held its 55th Meeting on 6th May 2022 and reviewed research proposal titled ***"Mkengeuko Wa Riwaya Ya Kiswahili Katika Utamaduni Wa Waswahili Zama Za Utandawazi: Mifano Kutoka Riwaya Teule."*** I am glad to inform you that the committee has granted ethical clearance on the submitted research proposal.

Furthermore, as the Principal Investigator of the study, the following conditions must be fulfilled:-

- Progress report is submitted to the University of Dodoma.
- Copies of final publications are made available to the University of Dodoma
- Site: **Tanzania.**

Best regards,

Prof. Ambrose Kessy
Chairperson - Institutional Research Review Committee (IRREC)

CC: Deputy Vice Chancellor-Academic, Research and Consultancy